# Mwanduso
## Ulongozi

Chitabu chino chotangigwa Mwanduso kwa viya ni chitabu cha mwanduso muna Dilagano da Umwaka. Nakala ya umwaka ya Chiebulania ya chitabu chino yokwandusa na mbuli “Baho mwanduso.” Chitabu chino cholagusa kuwa vinhu vose vilawa kulihi na viya Mulungu viyatendile na wanhu haumwanduso. Wasomi wengi siku zino wana magesa mengi kusonhela munhu hebu wanhu wowandike chitabu cha Mwanduso, na lusita lulihi chitabu chino vichandikigwe. Wauko wowogesa kuwa chitabu chino chiduganyigwa kwa kulawa senga mbasakanyo za umwaka muna ikaline ya 5 mbaka 6 KK (Ing'hali Chilisito). Wamwenga wotogola na mahokelo yoyotogoligwa mwa iwanhu weli wengi kuwa Musa kandika chitabu cha Mwanduso, iviya na vitabu vimwenga vya Kulawa na Mbuli za Walawi na Peta na Kumbukumbu da Malagilizo muna imiyaka ya 1,300 hebu 1,400, ing'hali Chilisito hana kwelekigwa.

Chitabu cha Mwanduso chimema mbuli zili muhimu ng'hani zowataza Wachilisito kuvimanya hanhu hose hamwenga ha Bibilia, ziwe za Lagano da Umwaka hebu Lagano da Sambi. Chitabu cha Mwanduso cholagusa viya uhasanyi vouwingile muna iisi, na viya wanhu wose vowomulonda mkombola. Iviya chitabu chino chofunula lungilo da Mulungu

da kuwakombola wanhu. Ino yowoneka muna uulotezi wa mwanduso woulotela kumsonhela Yesu, Mwanduso 3:15, iviya ahadi ya Mulungu kwa Abulahamu ya kuzitemela mate nyelesi zose zili mwiisi, Mwanduso 12:3.

**Mbuli zilimuno**

1. Mulungu kalumba isi na iviya kawaumba Adamu na Hawa fana viisimuliligwa muna isula ya 1 na 2.
2. Sula ya 3 mbaka 5 yomulonganya Adamu na Hawa na uhasanyi wao na welesi wao.
3. Sula ya 6 mbaka 9 yomulonganya Nuhu na mbuli za digombo dikulu.
4. Viimalile baho chitabu cha Mwanduso cholonga chiya chochilawile muna ulusita lwa Nuhu na uja ulusita wa Abulahabu na kongeza mbuli za lingo da Babeli muna isula ya 10 mbaka 11.
5. Sula ya 12 mbaka 50 zomsohnela Abulahamu na welesi wake na mwanduso wa Isilaili.
   - Ugima wa Abulahamu na muke wake Sala yosimuliligwa kulawa muna isula ya 12 mbaka 25.
   - Ugima wa Isaka na muke wake Labeka yosimuliligwa kulawa muna isula ya 21 mbaka 28 na udanganiko wake wosimuliligwa muna isula ya 35.
   - Ugima wa Yakobo na wanage na viwasegele kulawa Kanaani kuhita Misili wosimuliligwa muna isula ya 25 mbaka 50.
   - Sula 37 mbaka 50 imema mbuli za Yosefu, mwana nyachende wa Yakobo na iviya viyezile kutendigwa mtawala wa isi ya Misili.

## *Mbuli ya Ulumbaji*

1 Baho mwanduso, Mulungu kalumba ulanga
na isi yose na chila chinhu chili umo, 2 nayo
isi ikala yabule umbo hebu yabule chinhu cho-
chose. Na ziza dikala digubika mchanyha ya mazi,
Muhe wa Mulungu kakala katanda uchany'ha ya
mazi. 3 Maabaho Mulungu kalonga, “Dilawilile
bung'hulo” na bung'hulo dilawilila. 4 Mulungu
kawona kuwa bung'hulo dinoga, na kavigola
bung'hulo na ziza. 5 Bung'hulo kaditanga “Misi”
na ziza kaditanga “Chilo.” Iwa imitondo iwa
ichigulogulo siku ya mwanduso.

6 Maabaho Mulungu kalonga, “Hanhu hagati
ya mazi hayagole yamazi banzi mbili.” 7 Ivo
Mulungu kausa hanhu na kayagola yamazi
yeli mchanyha na yaja yeli hasi. Ilawilila ivo.
8 Mulungu kahatanga hanhu baho “Langa.” Iwa
imitondo iwa ichigulogulo, siku yekaidi.

9 Maabaho Mulungu kalonga, “Mazi yeli
hasi ya ulanga yaiduganye hanhu hamwe,
idahe kulawilila hanhu hanyalile.” Ilawilila
ivo. 10 Mulungu kahatanga hanhu hanyalile
“Isi” na hanhu hayaiduganye yamazi hamwe
kahatanga “Bahali.” Mulungu kawona kuwa
vinoga. 11 Maabaho Mulungu kalonga, “Isi yoteze
chila modeli ya mimeya yoikwima mbeyu zake na
chila modeli ya mibiki yoikwima matunda yeli na
mbeyu zozigendelela koteza mimeya imwenga
ya modeli yake.” Ilawilila ivo. 12 Ivo isi yoteza
chila modeli ya mimeya yoikwima mbeyu na
chila modeli ya mibiki yoikwima matunda yeli na
mbeyu. Mulungu kawona kuwa vinoga. 13 Iwa

imitondo iwa ichigulogulo, siku yetatu.

14 Maabaho Mulungu kalonga, “Mabung'hulo
yalawilile kuulanga, yagole imisi na ichilo,
yalaguse lusita lwa dugila na siku na miyaka,
15 yamwemwese kuulanga muladi isi iwe na
bung'hulo.” Ilawilila ivo. 16 Maabaho Mulungu
katenda mabung'hulo maidi makulu, zua
dimwemwese imisi na mwezi umwemwese
ichilo, iviya kausa nhondo. 17 Mulungu
keka mabung'hulo yayo kuulanga muladi
yamwemwese isi. 18 Yatawale imisi na ichilo na
kuvigola bung'hulo na ziza. Na Mulungu kawona
kuwa vinoga. 19 Iwa imitondo iwa ichigulogulo
siku yekane.

20 Maabaho Mulungu kalonga, “Mazi
yamemezwe vilumbe vili na ugima na langa
dimemezwe ndege woguluka.” 21 Mulungu
kalumba wanyama wakulu ng'hani mwiibahali
na chila modeli mbasakanyo ya vilumbe vili
na ugima vovigenda mwiibahali, na chila
modeli ya ndege. Mulungu kawona kuwa
vinoga. 22 Kavitemela mate na kavilongela
vilumbe va muna yamazi, “Yongezekeni na
yelekeni na muimemeze bahali,” na kawalongela
ndege wongezeke muiisi. 23 Iwa imitondo iwa
ichigulogulo, siku yetano.

24 Maabaho Mulungu kalonga, “Leka isi ilave
chila modeli mbasakanyo ya vilumbe vili na
ugima, wanyama wowofugigwa na wang'onyo
wotambala na wanyama wa kumbago,” ilawilila
ivo. 25 Mulungu kausa chila modeli mbasakanyo
ya wanyama wa kumbago na chila modeli ya

wanyama wowofugigwa na chila modeli ya
wang'onyo wotambala. Mulungu kawona vinoga.
26 Maabaho Mulungu kalonga, “Lelo
chimulumbe munhu yalingile fana cheye.
Yatawale somba wa mwiibahali na ndege
woguluka na wanyama wowofugigwa na isi
yose na wang'onyo wose wowotambala.” 27 Ivo
Mulungu kalumba munhu, yalingile fana yeye
mwenyewo. Kawalumba mulume na muke.
28 Kawatemela mate na kalonga, “Yelekeni wana
wengi, welesi wenu ukale na kuimemeza isi
yose na kuitawala. Muwatawale somba weli
mwiibahali, ndege woguluka na chila chiumbe
chili na ugima chochigenda mwiisi.” 29 Maabaho
Mulungu kalonga, “Lola, nomwing'hani chila
modeli ya mimeya ili na mbeyu na chila modeli
ya mibiki yoikwima matunda yeli na mbeyu muje.
30 Na wanyama wose na ndege wose woguluka na
wang'onyo wose wotambala mwiisi na viumbe
weli na ugima, ndiya yawo izakuwa mayani
ya mimeya.” Ilawilila ivo. 31 Mulungu kalola
chila chinhu chiyatendile, kawona kweli vinoga
ng'hani. Iwa imitondo iwa ichigulogulo, siku
yesita.

# 2

1 Ivo isi na ulanga na vose vili umo
vikomelezeka. 2 Muna isiku yesaba Mulungu
kakomeleza sang'hano yake yose, na siku iyo
yesaba Mulungu kahumula. 3 Mulungu kaitemela
mate siku yesaba na kaitenda iwe kwa ichimu
chake, kwaviya siku iyo Mulungu kakomeleza
sang'hano yake yose ya ulumbaji na kahumula.

4 Vino niivo Mndewa Mulungu viyalumbile ulanga na isi yose.

### *Mgunda wa Edeni*

Lusita ulo Mndewa Mulungu viyalumbile
ulanga na isi, 5 hakukalile na masavu bule
muna iisi na mimeya haisukile kwaviya Mndewa
Mulungu haitonyele mvula iisi na iviya kwabule
munhu wa kulima. 6 Nzasa ilawa hasi ya ulongo
na itapagiza isi yose.

7 Maabaho Mndewa Mulungu kasola ulongo wa isi na kamuusa mulume, kamuhuvila mhumuzi ya ugima muimhula, na mulume iyo kawa mgima.

8 Maabaho Mndewa Mulungu kahanda mgunda
hatangigwe Edeni, ubanzi wa ulawilo wa
zuwa, umo kamwika mulume iyo yoyamuusile.
9 Mndewa Mulungu koteza mibiki kulawa
muna iisi, chila modeli ya mibiki yoinogeza na
yoikwima matunda yofaya kwa ndiya. Hana
uludonho lwa mgunda uwo kukala na mbiki
woulava ugima na mbiki wa kuwatendeza wanhu
wayamanye yanogile na yehile.

10 Lwanda lokuluma kulawa muna mgunda wa
Edeni na mazi yakulumila muna ichizi, kulawa
uko wiigola nyanda nne. 11 Zina da lwanda lwa
mwanduso ni Pishoni, ulo loizunguluka isi ya
Havila ili na zahabu. 12 Zahabu ya isi iyo inoga.
Uko iviya kuna mvumbavumba wounung'hila
goya wotangigwa bedola na mabwe ya bei ng'hulu
yotangigwa oneki. 13 Zina da lwanda lwekaidi
ni Gihoni, ulo loizunguluka isi yose ya Kushi.

14 Zina da lwanda lweketatu ni Tigili, ulo lokulu-
mila banzi ya ulawilo wa zua wa isi ya Ashulu.
Zina da lwanda lwekane ni Efulati.
15 Maabaho Mndewa Mulungu kamsola
mulume iyo na kamwika muna mgunda wa
Edeni yachilime na yachilolese. 16 Mndewa
Mulungu kamulongela, “Kodaha kuja matunda ya
mbiki wowose muna umgunda, 17 mbali sekeuje
matunda ya mbiki wa kuyamanya yanogile na
yehile, mana siku dondauje matunda ya mbiki
uwo, kweli kwizadanganika.”
18 Maabaho Mndewa Mulungu kalonga,
“Havinogile bule munhu kukala yaidumwe.
Nizamuusila mtazi yomfaya.” 19 Ivo Mndewa
Mulungu kasola ulongo wa isi na kausa chila
modeli ya mnyama na ndege woguluka. Maabaho
kamgalila mulume iyo muladi yaweng'he mazina,
nayo kaweng'ha chila chiumbe yeli na ugima
zina jake. 20 Ivo mulume iyo kaweng'ha mazina
wanyama wofugigwa na ndege woguluka na
wanyama wa kumbago, mbali habule hata imwe
yoyofaya kumtaza.
21 Maabaho Mndewa Mulungu kamgalila mu-
lume iyo vuwevuwe da nhongo na viyakalile
muna zinhongo, kasola lubavu lwake lumwe na
kahagubika hanhu baho kwa nyama. 22 Mndewa
Mulungu kamulava muke muna ulubavu lolu-
soligwe kulawa kwa mulume iyo, na kamgala kwa
mulume iyo. 23 Maabaho mulume kalonga,
“Dino niijo divuha da mivuha yangu,
nyama ya nyama zangu,
kezatangigwa muke
kwaviya kalavigwa mwa mulume.”

24 Lekamana mulume kowaleka tati yake na mami
yake na koilumba na muke wake, nawo wokuwa
lukuli lumwe. 25 Mulume na muke wose waidi
wakala ukengele, mbali hawawonile chinyala
bule.

# 3

### *Wanhu woleka kumtegeleza Mndewa Mulungu*

1 Lelo zoka dikala vwizi kufosa wanyama wose
wa kumbago wowalumbigwe na Mndewa Mu-
lungu. Zoka dimuuza imuke, "Vino Mulungu
kawalongela kuwa sekemuje tunda da mbiki
wowose muna umgunda?"

2 Muke ija kamwidika, "Chodaha kuja tunda
da mbiki wowose muna umgunda, 3 mbali Mu-
lungu kachilongela sekechije matunda ya mbiki
uli haludonho hebu kuudalisa. One chahatenda
ivo chizadanganika."

4 Zoka dimwidika muke iyo, "Siyo kweli,
hamwizadanganika." 5 Mana Mulungu
kavimanya kuwa muhaja matunda yayo meso
yenu yezagubuligwa na mwizakuwa fana yeye
na mwizamanya yanogile na yehile.

6 Kawona uja mbiki wounogeza ng'hani na
matunda yake yodaha kudika, na kagesa unoga
ng'hani uhadahile kuwa na ubala, ivo kaha tunda
na kaja. Maabaho kamwing'ha mulumake, nayo
iviya kaja. 7 Bahobaho viwakomeleze kuja, meso
yawo yagubuligwa na wavimanya kuwa wauken-
gele, ivo wasola mayani wayawala.

8 Ichigulogulo mbeho viziholile, mulume na
muke wake wamuhulika Mndewa Mulungu ko-
genda muna umgunda, ivo waifisa hagati ya

mibiki muladi sekeyawawone. 9 Mbali Mndewa
Mulungu kamtanga mulume na kamuuza, “Kwa
kulihi?”
10 Nayo kamwidika, “Nikuhulika muna umgunda, nidumba kwaviya naukengele. Ivo niifisa.”
11 Mndewa Mulungu kamuuza, “Yelihi yoyakulongele weye kwa ukengele? Vino weye kuja tunda da mbiki unikulongele sekeuje?”
12 Mulume kamwidika, “Mwanamke youmwikile hano na niye, youning'hile, iyo yaning'hile tunda da mbiki uwo. Na niye nidija.”
13 Mndewa Mulungu kamuuza mwanamke, “Weye kutenda choni?”

Mwanamke kamwidika, “Zoka dinivwizila, na niye nija ditunda.”

### *Mulungu kowatagusa*

14 Mndewa Mulungu kadilongela dizoka,
“Kwaviya kuyatenda yano,
weye kuduwiligwa kufosa wanyama wose.
Kwizatambala na kwizakuja timbwisi siku zose za ugima wako.
15 Nizatenda weye wiihile na muke ija,
ulelo wake wiihile na ulelo wako.
Yeye kezakuhonda ditwi jako,
Na weye kwizamuluma chisiginho chake.”
16 Na kamulongela mwanamke,
“Nizakongezela usungu vondauwe na wimo na usungu vondawiibasule.
Kwizakuwa na hamu ya kumtawala mulumako,
nayo kezakutawala.”
17 Na kamulongela imulume,
“Kumtegeleza muke wako

na kuja tunda dinikulongele sekeuje.
Kwa chiya chiutendile, isi iduwiligwa.
Kwizatenda sang'hano ndala
siku zose za ugima wako
muladi kupata ndiya ifaya.
18 Isi izakwima miwa na mbigili,
na weye kwizakuja mimeya ya isi.
19 Kwizatenda sang'hano ndala za kulava vuke kuitenda isi ilave ndiya,
mbaka vondaubwele muna ulongo moulawile.
Weye ni ulongo,
na kwizabwela kuwa ulongo kaidi.”

20 Mulume kamtanga muke wake Hawa,
kwaviya niiyo mama wa wanhu wose weli na
ugima. 21 Mndewa Mulungu kawatendela viwalo
va mbende za wanyama Adamu na muke wake,
na kawayawaza.

### *Adamu na Hawa wowingigwa muna umgunda*

22 Maabaho Mndewa Mulungu kalonga, “Lelo
munhu iyo kawa fana imwe wetu, kayamanya
yanogile na yehile. Mbali yolondeka kumgomesa
kuja diya ditunda da mbiki wa ugima, mana
yahadija kezakala siku zose.” 23 Ivo Mndewa
Mulungu kamuwinga Adamu muna umgunda
wa Edeni na kamtendeza yalime muna ulongo
uyalawile. 24 Kamuwinga Adamu, na keka
wasenga wakalizi wa kuulanga ubanzi wa
ulawilo wa zuwa wa mgunda wa Edeni, wakala
na panga da moto dodikalile dohinduka kuno na
kuno muladi waukalize umbiki wa ugima.

# 4

*Kaini na Abeli*

1 Adamu kambandama Hawa muke wake,
na kapata wimo. Kamweleka mwana wa
chilume yatangigwe Kaini, nayo kalonga, “Kwa
kutazigwa na Mndewa Mulungu nipata mwana
wa chilume.” 2 Hamwande kamweleka mwana
imwenga zina jake Abeli. Abeli kakala mdimi
wa ng'hondolo na Kaini kakala mulimi wa isi.
3 Maabaho Kaini kagala mavuno yake yamwenga
na kayalava kuwa nhosa kwa Mndewa Mulungu.
4 Abeli nayo kagala nyama inogile na mavuta
ya ng'hondolo wake wa mwanduso kwelekigwa
kuwa nhosa. Mndewa Mulungu kanogelwa na
Abeli na nhosa yake. 5 Mbali Kaini hatogoligwe
na Mndewa Mulungu na nhosa yake, ivo
Kaini kengilwa na ludoko ng'hani, na kakwesa
ng'hombali. 6 Maabaho Mndewa Mulungu
kamuuza Kaini, “Habali kuna ludoko fana ivo?
Habali kukwesa ng'hombali? 7 Vino uhatenda
yanogile hutogoligwa bule? One uhatenda
yehile, uhasanyi wokusepasepa muna ulwivi
lwako, wokulonda kukutawala mbali kolondeka
uuhume.”

8 Maabaho Kaini kamulongela mdodo
wake Abeli, “Chihite kumgunda.” Viwakalile
kumgunda, Kaini kamzumhila mdodo wake na
kamkoma.

9 Maabaho Mndewa Mulungu kamuuza Kaini,
“Kakulihi mdodo wako Abeli?”

Kamwidika, “Niye sivimanyile bule. Vino niye
ndolezi wa mdodo wangu?”

10 Maabaho Mndewa Mulungu kauza, “Kutenda
choni? Damu ya mdodo wako ilinga fana dizi
donilililila kulawa muna uulongo. 11 Kwaviya
kumkoma mdodo wako na damu yake itika muna
isi, weye koduwiligwa kulawa iisi youkala. 12 One
uhageza kulima ndiya, ulongo hawizakupatila
chinhu chochose. Kwizawegela na kwizakuwa
kwabule ukazi muna iisi.”
13 Kaini kamulongela Mndewa Mulungu, “Nh-
aguso yangu iwa ndala na ibasanya siidaha hata
kuipapa. 14 Lola diyelo kuniwinga muna iisi in-
ogile na kunisegeza haulongozi hako. Nizakuwa
nabule ukazi na nowegela muna iisi yose, na
munhu yoyose yondayaniwone kezanikoma.”
15 Mbali Mndewa Mulungu kamwidika,
“Aka. Munhu yoyose yondayamkome Kaini,
kezalihilizigwa miyanza saba.” Maabaho
Mndewa Mulungu kamwika nhale kumzuma
yoyose yondayaiting'hane nayo, sekeyamkome.
16 Kaini kahasegela ha Mndewa Mulungu na
kakala isi itangigwa “Nodi”, niiyo ili ubanzi wa
ulawilo wa zua wa Edeni.

### *Welesi wa Kaini*

17 Kaini kambandama muke wake, nayo kapata
wimo na kamweleka Henoko. Maabaho Kaini
kazenga bululu na kaditanga Henoko, zina
da mwanage. 18 Henoko kapata mwana na
kamtanga zina jake Iladi; Iladi nayo kamweleka
Mehuyaeli; Mehuyaeli kamweleka Mesusayeli,
Mesusayeli kamweleka Lameki. 19 Lameki
kakala na wake waidi, imwe katangigwa
Ada na imwenga katangigwa Zila. 20 Ada
kamweleka Yabali, yakalile tata wa wafugaji

wokala muna yamahema. 21 Ndugu yake kakala
Yubali, iyo kakala tata wa wose wavina wila na
wotowa vimbeta na vingodongodo. 22 Zila nayo
kamweleka Tubalikaini, yoyakalile muhunzi
wa via vose va shaba na mazuma. Lumbu wa
Tubalikaini katangigwa Nama.

23 Lameki kawalongela wake zake,

"Ada na Zila nitegelezeni,
Mweye wake wa Lameki tegelezeni yonimulongelani
Niye nimkoma munhu kwaviya kaning'ha banha
Nimkoma imbwanga kwaviya kanilumiza.
24 Ihawa Kaini kolihigwa miyanza saba,
Lameki kezalihigwa miyanza malongo saba na saba."

### *Seti na Enosi*

25 Adamu kambandama kaidi muke wake, nayo
keleka mwana wa chilume. Kalonga, "Mulungu
kaning'ha mwana wa chilume badala ya Abeli,
yoyakomigwe na Kaini." Ivo kamtanga Seti. 26 Seti
nayo kapata mwana wa chilume, kamtanga Enosi.
Baho wanhu wandusa kumtambikila Mndewa
Mulungu.

# 5

### *Welesi wa Adamu*

1 Uno uwo ludongo lwa welesi wa Adamu.
Kwandusila Mulungu viyamulumbile munhu,
kamulumba fana yeye mwenyewo, 2 Mulungu
kawalumba mulume na muke, maabaho
kawatemela mate na kaweng'ha zina "Munhu."
3 Adamu viyakalile na miyaka gana na malongo
matatu, kapata mwana yoyalingile yeye, yeli na

chihanga fana chake mwenyewo na kamtanga
zina jake Seti. 4 Viyakomeleze kumweleka Seti,
Adamu kakala miyaka magana manane na keleka
wana wamwenga wa chilume na wa chike.
5 Adamu kadanganika na miyaka magana kenda
na malongo matatu.

6 Seti viyakalile na miyaka gana na tano,
kamweleka mwana zina jake Enosi. 7 Seti
viyamweleke Enosi, kakala miyaka magana
manane na saba na keleka wana wamwenga
wa chilume na wa chike. 8 Seti kadanganika na
miyaka magana kenda na longo na midi.

9 Enosi viyawile na miyaka malongo kenda,
kamweleka mwana zina jake Kenani. 10 Enosi
viyamalile kumweleka Kenani, kakala miyaka
magana manane na longo na tano na kaweleka
wana wamwenga wa chilume na wa chike.
11 Enosi kadanganika na miyaka magana kenda
na mitano.

12 Kenani viyakalile na miyaka malongo
saba, kamweleka mwana zina jake Mahalaleli,
13 maabaho viyamalile kumweleka Mahalaleli
kakala na miyaka magana manane na malongo
mane na kaweleka wana wamwenga wa chilume
na wa chike. 14 Kenani kadanganika na miyaka
magana kenda na longo.

15 Mahalaleli viyakalile na miyaka malongo
sita na tano, kamweleka mwana zina jake Yaledi.
16 Mahalaleli viyamweleke Yaledi, kakala na
miyaka magana manane na malongo matatu,
kaweleka wana wamwenga wa chilume na chike,
17 Mahalaleli kadanganika na miyaka magana
manane na malongo kenda na tano.

18 Yaledi viyakalile na miyaka gana na ma-
longo sita na midi, kamweleka mwana zina
jake Henoko. 19 Maabaho Yaledi viyamalile
kumweleka Henoko kakala na miyaka magana
manane. Kaweleka wana wamwenga wa chilume
na wa chike. 20 Na kadanganika na miyaka mag-
ana kenda na malongo sita na midi.

21 Henoko viyakalile na miyaka malongo
sita na mitano, kamweleka mwana zina jake
Mesusela. 22 Henoko viyamweleke Mesusela
kakala kwa kumnogeza Mulungu kwa miyaka
magana matatu na kaweleka wana wamwenga
wa chilume na wa chike. 23 Henoko kakala miyaka
magana matatu na malongo sita na mitano.
24 Henoko kakala kwa kumnogeza Mulungu
maabaho kasegela, kwaviya Mulungu kamsola.

25 Mesusela viyakalile na miyaka gana na ma-
longo manane na saba, kamweleka mwana zina
jake Lameki. 26 Maabaho viyamalile kumweleka
Lameki, Mesusela kakala na miyaka magana saba
na malongo manane na midi, kaweleka wana
wamwenga wa chilume na wa chike. 27 Mesusela
kadanganika na miyaka magana kenda na mal-
ongo sita na kenda.

28 Lameki viyakalile na miyaka gana na ma-
longo manane na midi, kamweleka mwana wa
chilume. 29 Lameki kamtanga mwana iyo zina
jake Nuhu, na kalonga, “Mwana ino niyo yon-
dayachigele moyo kwa kulawa muna isang'hano
yetu ndala, yochiitenda kwa makono yetu muna
iisi yoyaiduwile Mndewa Mulungu.” 30 Lameki
viyamalile kumweleka Nuhu, kakala na miyaka

magana matano na malongo kenda na mitano na
kaweleka wana wamwenga wa chilume na wa
chike. 31 Lameki kadanganika na miyaka magana
saba na malongo saba na saba.
32 Nuhu viyawile na miyaka magana matano,
kaweleka wana watatu, Shemu na Hamu na
Yafesi.

# 6

### *Wihi wa Munhu*

1 Wanhu viwanduse kongezeka muna iisi
yose, na wana wa chike welekigwa kumwawo,
2 wasenga wa Mulungu* wawawona wandele wa
wanhu kuwa lumondo, na wawasola kuwa wake
zawo fana viwalondile. 3 Maabaho Mndewa
Mulungu kalonga, "Muhe wangu hawizakala
kwa wanhu siku zose, kwaviya wawo ni lukuli.
Kwandusila sambi na kugendelela, hawezakala
miyaka kufosa miyaka gana na malongo maidi."
4 Lusita ulo na kugendelela, kukala na Wanefili
† mwiisi, wawo wakala welesi wa wana wa
Mulungu na wandele wa wanhu. Wawo niiyo
wanhu wakalile magalu, wamanyike ng'hani
baho umwaka. 5 Mndewa Mulungu kawona
wihi mkulu wa wanhu muna iisi na magesa
yawo yehile chila siku, 6 Ivo Mndewa Mulungu
kengilwa usungu ng'hani kwa kumulumba
munhu na kumwika muna iisi, na kawona usungu
ng'hani muna umoyo wake. 7 Mndewa Mulungu

* **6:2** Kwa Chiebulaniya cholongwa, "Wana wa Mulungu," lusita mwingi ina fambulo da viumbe wa chimuhe siyo wanhu. † **6:4** "Wanefili" fambulo jake "mizinhu mitali inenehe."

kalonga, “Nizamsegeza munhu yonimulumbile
muna isi, na iviya nizawasegeza wang'onyo,
waja wotambala na ndege wa kuulanga. Nojuta
kwaviya niwalumba.” 8 Mbali Mndewa Mulungu
kanogelwa na Nuhu.

### *Nuhu*

9 Zino ni mbuli za ugima wa Nuhu yoyakalile
yotenda yanogile haulongozi wa Mulungu,
mkamilifu muna uwelesi wake. Nuhu kakala
kwa kumnogeza Mulungu. 10 Nuhu kaweleka
wana watatu wa chilume, wowatangigwe Shemu
na Hamu na Yafesi. 11 Chila munhu kakala mwihi
haulongozi wa Mulungu, na tibwilitibwili jenela
chila hanhu. 12 Mulungu kawona isi yose imema
wihi, kwaviya wanhu watenda ihe.

13 Mulungu kamulongela Nuhu, “Nilamula
kuwadanganiza wanhu wose kwaviya
waimemeza iisi tibwilitibwili. Kweli
nizawadanganiza ng'hani hamwe na isi. 14 Zenga
safina kwa mabanzi ya mibiki midala. Gola
viheleto na uhake tulasi kunze na mgati. 15 Vino
niivo vondauizenge, utali wake iwe makono
magana matatu na ugalamu wake makono
malongo matano na chimo chake makono
malongo matatu. 16 Utende chisuwili na chiwe
mkono umwe hagati wa digulu maabaho ika
lwivi ubanzi umwe, safina iwe na golofa nhatu.
17 Na niye nizagala gombo muna iisi muladi
kudanganiza chila chiumbe chili na ugima.
Chila chinhu muna iisi chizadanganika. 18 Mbali
nizatenda lagano na weye. Kwizakwingila muna
isafina na muke wako, wanago na wake zawo.
19 Wagale mwiisafina chila modeli ya viumbe

vili na ugima vidi, va chilume na va chike, na
uvilolese vikale. [20] Wingize chila ndege wa
kuulanga, chila wang'onyo wotambala na chila
wanyama, waidi waidi muladi wawe wagima.
[21] Usole chila modeli ya ndiya wiike goya kwa
ichimu chenu na kwa ichimu chawo.” [22] Nuhu
kasang'hana chila chinhu fana viyalagilizigwe na
Mulungu.

# 7

*Gombo*

[1] Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Nuhu, “Ingila mwiisafina weye na wanago
wose, kwaviya nikuwona weye muhala kunoga
haulongozi wangu mwa iwanhu wa isi yose.
[2] Iviya muna iwanyama wodigwa usole malume
saba na mazike saba, mbali wanyama hawadigwa
sola lume dimwe na zike dimwe. [3] Iviya sola
ndege wa kuulanga malume saba na mazike saba,
muladi uwakalize ugima wawo mwiisi. [4] Zihafosa
siku saba kwandusila sambi nizagala mvula
yondaitonye kwa siku malongo mane, imisi na
ichilo, muladi kuvibanaga viumbe vigima vose
vonivilumbile.” [5] Nuhu katenda chila chinhu
choyalagilizigwe na Mndewa Mulungu.

[6] Gombo vidizile muna iisi, Nuhu kakala na
miyaka magana sita. [7] Nuhu na muke wake na
wanage wa chilume na wake zawo, wengila muna
isafina muladi kugomboka na digombo. [8] Wose
wanyama iwe wambule mwiko hebu hawambule
mwiko na wang'onyo na ndege, [9] wengila mwi-
isafina waidi waidi, muke na mulume hamwe

na Nuhu, fana Nuhu viyalagilizigwe na Mulungu.
10 Vizifosile siku saba gombo diza.

11 Nuhu viyawile na miyaka magana sita, muna
isiku ya longo na saba mwezi wekaidi, siku iyo
nzasa zose hasi ng'hani ya isi zilava mazi ng'hani
na mazonzo ya kuulanga yavuguka. 12 Mvula
itonya mwiisi siku malongo mane, imisi na ichilo.

13 Siku iyo iyo Nuhu na muke wake wengila
muna isafina hamwe na wanawe watatu, Shemu
na Hamu na Yafesi na wake zawo. 14 Wahita
hamwe na chila modeli ya wanyama wa kumbago
na chila modeli ya wanyama wofugigwa na chila
modeli ya wang'onyo wotambala na chila mod-
eli ya ndege na chila chiumbe chili na mabawa.
15 Chila viumbe waidi waidi walume na wake,
chila chilumbe chili na ugima chingila muna isa-
fina hamwe na Nuhu, 16 fana Mulungu viyamulag-
ilize. Maabaho Mndewa Mulungu kahinda ulwivi
hachisogo cha Nuhu.

17 Gombo digendelela kwa siku malongo mane,
na yamazi yamema mbaka safina iyengeluka
uchanyha ya mazi. 18 Mazi yawa na china chi-
tali na safina iyengeluka muna yamazi. 19 Mazi
yakala mengi ng'hani muna iisi, yaigubika mil-
ima mitali chila hanhu. 20 Mazi yamema mbaka
yaigubika milima utali wa makono longo na
mitano. 21 Vilumbe vose vili na ugima muna
iisi vidanganika, ndege wose na wanyama wose
wofugigwa na wanyama wose wa kumbago na
wang'onyo wose wotambala na wanhu wose.
22 Chila chilumbe chikala muna iisi inyalile chi-
danganika. 23 Mndewa Mulungu kavinanga vi-
umbe vose vigima mwiisi, wanhu na wanyama

wang'onyo wotambala na ndege woguluka. Kasi-
gala Nuhu muhala na waja wowakalile hamwe
nayo muna isafina. 24 Mazi yakala muna iisi siku
gana na malongo matano.

# 8

### *Uhelelo wa Gombo*

1 Mbali Mulungu kamkumbuka Nuhu na
wanyama wose wa kumbago na wanyama
wose wofugigwa wowakalile hamwe nayo muna
isafina. Ivo Mulungu kahembelula beho muna
iisi na mazi yandusa kuhunguka. 2 Nzasa zose za
mazi hasi ng'hani ya isi na mazonzo ya kuulanga
vihindigwa, na mvula ileka kutonya. 3 Mazi
yagendelela kuhunguka ugalugagaluga muna
iisi. Viifikile siku gana na malongo matano, mazi
yahunguka ng'hani. 4 Muna isiku ya longo na saba
ya mwezi wa saba, safina ifika muna imilima
ya Alalati na ikala baho. 5 Mazi yagendelela
kuhunguka ugalugagaluga, na siku ya mwanduso
ya mwezi wa longo, vidonho va milima viwoneka.

6 Vizimalile siku malongo mane, Nuhu
kavugula zonzo da isafina yoyaitendile, 7 na
kamtuma howe kunze, na kaguluka kuno na kuja,
mbaka mazi viyanyalile mwiisi. 8 Maabaho Nuhu
kamtuma nziwa yawone one mazi yahunguka
muna iisi. 9 Mbali kwaviya mazi yakala yang'hali
yaigubika isi yose, nziwa hapatile hanhu ha
kwima bule. Kabwela kwa Nuhu kuna isafina,
Nuhu kaugolosa mkono wake kamsola na
kumbweleza muna isafina. 10 Nuhu kagozela
siku zimwenga saba, maabaho kamtuma kaidi

nziwa. 11 Nziwa kabwela kwa Nuhu ichigulogulo
kuno kana tambi bisi da mzaituni muna umulomo
wake. Ivo Nuhu kavimanya kuwa mazi yakala
yahunguka muna iisi. 12 Maabaho kagozela siku
zimwenga saba, kamtuma kaidi nziwa, mwanza
uno nziwa habwelile bule.
13 Nuhu viyakalile na miyaka magana sita na
umwe, siku ya mwanduso ya mwezi mosi, ka-
wona mazi yakala yanyala muna iisi. Nuhu
kagubula chigubiko cha safina, kalola na kuwona
isi ikala inyala. 14 Siku ya malongo maidi na saba
ya mwezi wekaidi, isi ikala inyala ng'hani.
15 Maabaho Mulungu kamulongela Nuhu,
16 “Lawa mwiisafina weye na muke wako na
wanago na wake zawo. 17 Sola chila chiumbe chili
na ugima chili na weye, ndege na wanyama wose
na wang'onyo ulawe nawo kunze muladi weleke
na kwenela muna iisi yose.” 18 Nuhu kalawa
kunze muna isafina hamwe na muke wake na
wanage na wake zawo. 19 Wanyama wose na
vilumbe weli na ugima viya vitambala muiisi na
chila modeli wa ndege walawa muna isafina, kwa
kusondelela modeli wawo.

### *Nuhu kolava nhosa za kutimbula*

20 Nuhu kamzengela Mndewa Mulungu lu-
pango, kalava nhambiko wanyama wamwenga
wodigwa na ndege wodigwa, kamtimbulila Mu-
lungu mchanyha ya ulupango. 21 Mnung'ho un-
ogile wa nhosa iyo umnogeza Mndewa Mulungu,
nayo kalonga muna umoyo wake, “Sizaiduwila
kaidi isi kwa ichimu cha wanhu. Kwaviya magesa
ya wanhu yeha kwandusila kuudodo wawo. Ivo
sizainanga kaidi isi fana vinitendile. 22 Chipindi

isi viikalile, msimu wa kuhanda na kugobola,
lusita lwa chihuhe na vuke na masika na zua,
chilo na misi, havizamala.”

# 9

*Mulungu kokwika lagano na Nuhu*

1 Mulungu kamtemela mate Nuhu na wan-
age na kawalongela, “Yelekeni na mongezeke na
muimemeze isi yose. 2 Wanyama wose muna
iisi na ndege woguluka na wang'onyo wotam-
bala na somba wose muna ibahali wezawad-
umbani. Wawo wose mwizawatawala. 3 Chila
chinhu chili na ugima na chitambala molondeka
kuchija. Fana vinimwing'hileni mibiki isuka,
sambi nomwing'hani chila chinhu. 4 Mbali seke-
muje nyama ili na damu, kwaviya ugima wake
waumo muna idamu. 5 One munhu yoyose hebu
mnyama yahamkomani, nizamtagusa. Na one
munhu yahamkoma miyage, kezatagusigwa.
6 “Munhu yoyose yondayamkome miyage,
iviya nayo kezakomigwa na munhu,
Mana munhu kalumbigwa yalingile fana Mu-
lungu mwenyewo.
7 Yelekeni na kwenela isi yose.”
8 Maabaho Mulungu kamulongela Nuhu na
wanage, 9 “Lelo nokwika lagano jangu na mweye
na welesi wenu, 10 na vilumbe vili na ugima vose
vili na weye, ndege na wanyama wofugigwa na
chila mnyama wa kumbago yoyalawile muna isa-
fina hamwe na weye. 11 Nodikanhamiza lagano
jangu na mweye, vilumbe vose vili na ugima hav-
izanangigwa na gombo, hebu gombo hadizalaw-
ilila kaidi kuinanga isi.” 12 Mulungu kalonga,

“Chino niicho chilaguso cha lagano dinikwika
hagati ya niye na mweye na chila chilumbe
chili na ugima chikala hamwe na mweye kwa
welesi wose mbaka welesi ukwiza, 13 nokwika
pinde da Mulungu kuna yamawingu. Chiza-
kuwa chilaguso cha lagano jangu na isi yose.
14 Chila nahayatanda mawingu muna uulanga na
pinde da Mulungu dizalawilila muna yamawingu,
15 Nizadikumbuka lagano jangu na mweye na
vilumbe vose vili na ugima. Mazi hayezagaluka
kaidi kuwa gombo kuvinanga vilumbe vose vili
na ugima. 16 Baho pinde da Mulungu von-
dadiwoneke kuna yamawingu, nizadiwona na
kudikumbuka lagano jangu na vilumbe vili na
ugima mwiisi.” 17 Mulungu kamulongela Nuhu,
“Chino ni chilaguso cha lagano donitendile na
vilumbe vose vili na ugima muna iisi.”

### *Nuhu na Wanage*

18 Wanage Nuhu wowalawile muna isafina
wakala Shemu na Hamu na Yafesi. Hamu kakala
niiyo tata wa Kanani. 19 Kufosela wanhu wawo
watatu wa Nuhu, wanhu wenela muiisi yose.

20 Nuhu kakala wa mwanduso kuhanda
mgunda wa mizabibu. 21 Kang'wa divai na
kakoligwa, maabaho kagona ukulunge muna
dihema jake. 22 Hamu tata wa Kanani kauwona
ukengele wa tati yake, kalawa kunze na
kuwalongela ndugu zake waidi. 23 Maabaho
Shemu na Yafesi wasola walo na waigeleka
mmayega yawo na wahita chisengelenyuma
na kuugubika ukengele wa tati yawo. Walola
mumgwazo na hawauwonile bule ukengele

wa tati yawo. 24 Nuhu upele viukunguzuke
kavimanya viyatendiligwe na mwanage imdodo,
25 kalonga,
"Nayaduwiligwe Kanani.
Kezakuwa mtumwa kwa ndugu zake."
26 Iviya kalonga, "Yatunhizigwe Mndewa Mulungu, Mulungu wa Shemu.
Kanani yawe mtumwa wa Shemu.
27 Mulungu yamwing'he wana wengi Yafesi,
yakale hamwe na Shemu
na Kanani yawe mtumwa wake."
28 Vidimalile gombo, Nuhu kakala miyaka magana matatu na malongo matano 29 Nuhu kadanganika na miyaka magana kenda na malongo matano.

# 10

*Welesi wa Nuhu*

1 Uno niuwo welesi wa wana wa Nuhu, Shemu na Hamu na Yafesi. Wano watatu weleka wana vidimalile digombo.

2 Wana wa Yafesi wakala Gomeli na Magogu na
Madayi na Yavani na Tubali na Mesheki na Tilasi.
3 Wana wa Gomeli wakala Ashikenazi na Lifazi
na Togoma. 4 Wana wa Yavani wakala Elisha na
Talishishi na Kitimu na Dodanimu. 5 Kufosela
wawo wanhu wa mhwani wapwililika muna izisi zawo hamwe na ulonzi wawo na ng'holo zawo na makabila yawo.

6 Wana wa Hamu wakala Kushi na Misili na
Puti na Kanani. 7 Wana wa Kushi wakala Seba
na Havila na Sabita na Lama na Sabuteka. Wana
wa chilume wa Lama wakala Sheba na Dedani.
8 Kushi kamweleka Nimulodi, yoyakalile galu

wa mwanduso mwiisi yose. 9 Kakala galu wa
kusaka wanyama haulongozi ha Mndewa Mu-
lungu, lekamana wanhu wolonga, “Uwe fana
Nimulodi yakalile galu wa kusaka haulongozi ha
Mndewa Mulungu.” 10 Mwanduso wa ufalume
wake ukala Babeli na Eleki na Akadi na Kalinehi
muna iisi ya Shinali. 11 Nimulodi viyalawile uko,
kahita Ashulu kazenga mabululu ya Ninawi na
Lehobosi na Kala, 12 na Leseni ili hagati ya Ninawi
na Kala, bululu dikulu.

13 Welesi wa Misili ukala Waludima na Wanami
na Walehabi na Wanafutuhima 14 na Wapatilusi
na Wakashuhi na Wakafitoli, Wafilisiti niiyo
mwanduso wa Wakashuhi.

15 Kanani kakala tata wa Sidoni, mwanage
chaudele, na imwenga katangigwa Hiti, 16 na
Kanani iviya ni tata wa Wayebusi na Waamoli
na Wagiligashi, 17 na Wahivi na Waaliki na
Wasini, 18 na Waavadi na Wazemali na Wahamati.
Hamwande wanhu wa welesi wa Wakanaani
waimwaga. 19 Hanhu ha Wakanaani handusila
Sidoni kuhita Gelali mbaka kufika Gaza na nzila
ya kuhita Sodoma na Gomola na Adima na Se-
boimu mbaka Lasha. 20 Uno niuwo welesi wa
Hamu muna yamakabila yawo na ulonzi wawo na
hanhu howokala na ng'holo zawo.

21 Nayo Shemu niiyo sekulu wa Yafesi, na kakala
wasaho wa wana wose wa Ebeli. 22 Wana wa
Shemu wakala Elamu na Ashulu na Alifakisadi na
Ludi na Alamu. 23 Wana wa Alamu wakala Usi na
Huli na Geteli na Mashi. 24 Alifakisadi kamweleka
Shela, na Shela kamweleka Ebeli. 25 Ebeli keleka
wana waidi wa chilume, zina da wa mwanduso
ni Pelegi, kwaviya muna ulusita lwake isi iigola,

na imwenga zina jake Yokitani. 26 Yokitani kakala
tata wa Alimodadi na Shelefu na Hasalimaweti na
Yela, 27 na Hadolamu na Uzali na Dikila, 28 na Obeli
na Abimayeli na Sheba 29 na Ofili na Havila na
Yobabu. Wawo wose wakala welesi wa Yokitani.
30 Isi yowakalile yenela kulawa Mesha mbaka
Sifali kuna mulima wa isi ya ulawilo wa zua.
31 Uno niuwo welesi wa Shemu muna izisi zawo
na ulonzi wawo na makabila yawo na ng'holo
zawo.

32 Zino ni ng'holo za wana wa Nuhu, kusondelela ludongo lwa welesi wawo hamwe na zisi
zawo. Wanhu wano wapwililika mwiizisi zose
vidimalile digombo.

# 11

## *Lingo da Babeli*

1 Umwaka wanhu wa zisi zose wakala na
ulonzi umwe muhala na walonga mbuli zimwe
muhala. 2 Wanhu viwagendile kulawa ulawilo wa zua, wafika bawe da Shinali, wakala.
3 Wailongela, "Izoni! Chitende matafali chiyasome moto vinogile." Wakala na matafali badala
ya mabwe, na tulasi badala ya ulongo. 4 Maabaho
walonga, "Lelo chiizengele bululu jetu na lingo
dizafika mbaka kuulanga, muladi zina jetu dimanyike ng'hani na sekechiimwage muna iisi."

5 Mbali Mndewa Mulungu kahumuluka na
kudiwona bululu na lingo dodikalile dizengigwa
na wanhu. 6 Na Mndewa Mulungu kalonga,
"Lola wanhu wano wose ni wamwe na wolonga
ulonzi umwe, uno ni mwanduso wa sang'hano
yawo. Lelo wezadaha kutenda chinhu chochose

chiwoilungila. [7] Leka chihumuluke na kutibula
ulonzi wawo muladi sekewaitegeleze.” [8] Ivo
Mndewa Mulungu kawapwililisa muna iisi yose,
nawo waleka kuzenga dibululu. [9] Lekamana bu-
lulu ijo ditangigwa Babeli, kwaviya Mndewa Mu-
lungu katibula ulonzi wa isi yose, na kulawa uko
Mndewa Mulungu kawapwililisa wanhu mwiisi
yose.

### *Welesi wa Shemu*

[10] Uno uwo ludongo lwa welesi wa Shemu.
Shemu viyakalile na miyaka gana kamweleka
Alifakisadi, iyo ikala miyaka midi vidimalile
digombo. [11] Shemu viyamweleke Alifakisadi
kakala miyaka magana matano, na keleka wana
wamwenga wa chilume na wa chike.

[12] Alifakisadi viyakalile na miyaka malongo
matatu na mitano, kamweleka Shela.
[13] Alifakisadi viyamweleke Shela, kakala miyaka
magana mane na mitatu, na keleka wana
wamwenga wa chilume na wa chike.

[14] Shela viyakalile na miyaka malongo matatu,
kamweleka Ebeli. [15] Shela viyamweleke Ebeli
kakala miyaka magana mane na mitatu, na keleka
wana wamwenga wa chilume na wa chike.

[16] Ebeli viyakalile na miyaka malongo matatu
na mine kamweleka Pelegi. [17] Ebeli viyamweleke
Pelegi kakala miyaka magana mane na malongo
matatu, na keleka wana wamwenga wa chilume
na wa chike.

[18] Pelegi viyakalile na miyaka malongo matatu,
kamweleka Lewu. [19] Pelegi viyamweleke Lewu
kakala miyaka magana maidi na kenda, na keleka
wana wamwenga wa chilume na wa chike.

20 Lewu viyakalile na miyaka malongo matatu
na midi kamweleka Selugi. 21 Lewu viyamweleke
Selugi kakala miyaka magana maidi na saba, na
keleka wana wamwenga wa chilume na wa chike.
22 Selugi viyakalile na miyaka malongo matatu,
kamweleka Naholi. 23 Selugi viyamweleke Naholi
kakala miyaka magana maidi, na keleka wana
wamwenga wa chilume na wa chike.
24 Naholi viyakalile na miyaka malongo maidi
na kenda kamweleka Tela. 25 Naholi viyamweleke
Tela kakala miyaka gana na longo na kenda, na
keleka wana wamwenga wa chilume na wa chike.
26 Tela viyakalile na miyaka malongo saba
kaweleka Abulamu na Naholi na Halani.

### *Welesi wa Tela*

27 Uno niuwo welesi wa Tela. Tela kaweleka
Abulamu na Naholi na Halani. Nayo Halani
kamweleka Lutu. 28 Halani kadanganika
Ulu kuna iisi ya Wakalidayo kuyavumbukile
chipindi Tela tati yake yang'hali kokala uko.
29 Abulamu na Naholi wasola wake. Muke wa
Abulamu katangigwa Salayi na muke wa Naholi
katangigwa Milika, mndele wa Halani. Halani
iviya niiyo tati yawo Milika na Isika. 30 Mbali
Salayi kakala kabule wana kwaviya kakala
mgumba.
31 Tela kamsola Abulamu mwanage, na Lutu
mzukulu wake yoyelekigwe mwanage Halani, na
Salayi muke wake Abulamu, na wasegela wose
hamwe kulawa Ulu, bululu da Wakalidayo, kuhita
kuna iisi ya Kanaani. Viwafikile Halani wakala
uko. 32 Tela viyakalile na miyaka magana maidi
na mitano, kadanganika uko Halani.

# 12

## *Mulungu komtanga Abulamu*

1 Mndewa Mulungu kamulongela Abulamu,
“Segela muna iisi yako, leka ndugu zako na kaye
ya tati yako na uhite kuna iisi yondanikulagusile.
2 Nizakutenda uwe kabila kulu
na nizakutemela mate
na nizaditenda zina jako dimanyike ng'hani,
na kwizawatemela mate wamwenga.
3 Nizawatemela mate wose wowokutemela mate weye,
Mbali yoyose yokuduwila, nizamduwila,
na ng'holo zose muna iisi
zizatemeligwa mate kufosela weye.”
4 Abulamu viyasegele Halani kakala na miyaka
malongo saba na tano, fana Mndewa Mulungu
viyamulongele kutenda. Na Lutu kahita hamwe
nayo. 5 Abulamu kamsola Salayi muke wake, na
mwihwage Lutu na vinhu vake vose na wanhu
wose wowawapatile uko Halani. Wasegela kuhita
isi ya Kanaani.

Viwafikile muna iisi ya Kanani, 6 Abulamu
kafosa muna iisi ya Shekemu, hanhu heli na
mbiki mkulu uko Mole. Lusita ulo Wakanaani
wakala wokala muna iisi iyo. 7 Mndewa Mulungu
kamulawilila Abulamu na kamulongela,
“Ino iyo iisi yondaniweng'he welesi wako.”
Maabaho Abulamu kamzengela lupango Mndewa
Mulungu, yoyamulawilile. 8 Viyafosile yayo,
kasegela mbaka kuna mulima uli ubanzi wa
ulawilo wa zua wa Beseli, kasimika hema jake
hagati ya Beseli ubanzi wa uswelo wa zua na
bululu da Ayi ubanzi wa ulawilo wa zua. Baho

iviya kamzengela Mndewa Mulungu lupango na
kamtambikila. 9 Maabaho Abulamu kagendelela
kulawa hanhu mbaka hanhu ubanzi wa Negebu.

### *Abulamu uko Misili*

10 Kuna iisi ya Kanani kukala na nzala.
Ivo Abulamu kahita Misili kukala uko fana
mgeni, kwaviya nzala ikala ng'hulu muna iisi.
11 Viyakalile habehi kufika Misili, kamulongela
Salayi muke wake, "Novimanya kuwa weye
kwa muke lumondo. 12 Lusita Wamisili
vondawakuwone, wezalonga kuwa weye
muke wangu, ivo wezanikoma na kukuleka.
13 Uwalongele kuwa weye kwa lumbu jangu,
muladi kwa ichimu icho wezanitendela yanogile
na kunileka mgima kwa ichimu chako."
14 Abulamu viyengile Misili, Wamisili wamuwona
muke wake kakala lumondo. 15 Wakulu womtaza
mfalume viwamuwone Salayi, wamtogoza kwa
mfalume na kagaligwa muna imhongono ya
mfalume. 16 Kwa ichimu cha Salayi, mfalume
kamtendela yanogile Abulamu na kahokela
ng'hondolo na ng'ombe na vihongwe wa chilume
na wa chike na watumwa wa chilume na wa chike
na ngamiya.

17 Mbali Mndewa Mulungu kamgaza mfalume
na wanhu wose weli muimhongono yake kwa
matamu makulu kwa ichimu cha Salayi muke wa
Abulamu. 18 Maabaho mfalume kamtanga Abu-
lamu na kamuuza, "Chino choni chounitendele?
Habali hunilongele kuwa kakala muke wako?
19 Habali kulonga kuwa ino mwali wako na niye
nimsola kuwa muke wangu? Lelo ayo muke wako,
msole na msegele hano." 20 Maabaho mfalume

kawalongela wanhu wake wamuleke Abulamu yasegele hamwe na muke wake na vinhu vake vose.

# 13

## *Abulamu na Lutu woigola*

1 Abulamu kabwela kulawa Misili kengila
ubanzi wa Negebu. Kakala na muke wake na
vinhu vake vose hamwe na Lutu. 2 Abulamu
kakala tajili ng'hani. Kakala na fugo na hela na
zahabu. 3 Kagendelela kugenda kulawa hanhu ha
Negebu mbaka Beseli, kafika hanhu hoyakalile
kasimika hema baho haichanduso hagati ya
Beseli na Ayi, 4 hanhu hoyakalile yazengile
lupango. Baho Abulamu kamtambikila Mndewa
Mulungu.
5 Iviya Lutu yoyagendile na Abulamu, kakala
na ng'ombe na ng'hondolo na mahema. 6 Isi
haiwafaiye wose waidi kukala hamwe kwaviya
wakala na fugo nyingi. 7 Kwa ivo kulawilila nd-
wagi hagati ya wadimaji wanyama wa Abulamu
na wadimaji wa Lutu. Chipindi icho Wakanaani
na Wapelizi wakala wokala muna iisi ija.
8 Maabaho Abulamu kamulongela Lutu, "Ch-
eye cha ndugu, sekechigombe, hebu wadimaji
wako sekewagombe na wadimaji wangu. 9 Lola
isi ino yose haulongozi wako, chiigole. Uhahita
ukumoso niye nizahita ukulume, hebu uhahita
ukulume niye nizahita ukumoso."
10 Lutu kenula meso yake na kadiwona bawe
da lwanda lwa Yoludani, kawona dina mazi ya
kufaya chila hanhu, fana viya mgunda wa Mn-
dewa Mulungu na iviya fana isi ya Misili ubanzi

wa Soali. Mndewa Mulungu kakala hanayananga
mabululu ya Sodoma na Gomola. 11 Kwa ivo Lutu
kasagula bawe jose da lwanda lwa Yoludani, na
kahita ubanzi wa ulawilo wa zua. Ivo waigola.
12 Abulamu kakala muna iisi ya Kanaani, mbali
Lutu kakala muna yamabululu yaja ya dibawe na
kahamila Sodoma. 13 Wanhu wa Sodoma wakala
weha na wamuhasanya Mndewa Mulungu.

### *Abulamu kohamila Hebuloni*

14 Abulamu viyakomeleze kwiigola na Lutu,
Mndewa Mulungu kamulongela, “Inula chihanga
chako ulole banzi zose. 15 Isi ino yose yowii-
wona, nizakwing'ha weye na welesi wako siku
zose. 16 Welesi wako wizakuwa fana msanga,
habule munhu yondayadahe kuupeta. 17 Lelo
hita na ukaizunguluke isi ija, kwaviya nizak-
wing'ha.” 18 Ivo Abulamu kahamiza hema jake,
kahita kukala habehi na mibiki mikulu ya Ma-
mule kuja Hebuloni, na uko kamzengela lupango
Mndewa Mulungu.

## 14

### *Abulamu komkombola Lutu*

1 Siku izo mfalume Amilafeli wa Shinali na
Aliyoki wa Elasali na Kedolilaoma wa Elamu na
Tidali wa Goimu, 2 wahita kwiitowa ng'hondo na
wafalume wano. Wafalume wawo ni Belo wa
Sodoma na Bilisha wa Gomola na Shinabu wa
Adima na Shebeli wa Seboimu na mfalume wa
Bela iviya yotangigwa Soali. 3 Wafalume wawo
wayahanganya majeshi yawo yose hana dibawe
da Sidimu, vino sambi ni Bahali ya Munyu. 4 Kwa

lusita lwa miyaka longo na midi, wakala wolan-
gulizigwa na mfalume Kedolilaoma, mbali vi-
ifikile mwaka wa longo na tatu, wamuhinduka.
5 Muna umwaka wa longo na nne, mfalume Kedo-
lilaoma na wafalume wayage weza na kuwahuma
Walefai wa uko Ashiteloshi Kiliasaimu na Wazuzi
uko Hamu na Waemi uko Shawe Kiliyasaimu.
6 Iviya wawahuma Waholi uko kuna mulima wa
Seili, wawawinga kutali mbaka Elipalani habehi
na dibwilingu. 7 Maabaho wabwela kuchisogo
mbaka Enimishipati iviya yotangigwa Kadeshi,
waihuma isi yose ya Waamaleki na kuwahuma
Waamoli wowakalile Hasasoni Tamali.

8 Maabaho wafalume wa Sodoma na Gomola
na Adima na Seboimu na Bela iviya yotangigwa
Soali, watenda ng'hondo na wehi wawo
kuna dibawe da Sidimu 9 waitoa na mfalume
Kedolilaoma wa Elamu na Tidali wa Goimu
na Amilafeli wa Shinali na Aliyoki wa Elasali,
wafalume wane waitowa na wafalume watano.
10 Bawe da Sidimu dikala dimemile makombo ya
lami, na baho wafalume wa Sodoma na Gomola
viwagezile kukimbila ng'hondo, watumbukiya
umo na wamwenga waibangila muna ivigongo.
11 Wafalume wawo wane wahumile wasola chila
chinhu cha Sodoma na Gomola na ndiya zawo
zose, maabaho wasegela. 12 Wamgwila Lutu,
mwihwa wa Abulamu, yoyakalile yokala Sodoma,
wasola na vinhu vake vose, maabaho wasegela.

13 Munhu imwe yoyasulupuke kahita kumulon-
gela ija Muebulaniya Abulamu yoyakalile kokala
habehi na mibiki mikulu ya Mamule Muamoli,
yoyakalile ndugu yake Eshikoli na Aneli. Wose
wakala wailumba na Abulamu. 14 Abulamu

viyahulike ndugu yake kagwiligwa, kawatanga
wanhu wose wa muna ikaye yake wadahile kwi-
itowa, wakala magana matatu na longo na nane.
Wawasondelela wafalume waja mbaka bululu da
Dani. 15 Ichilo Abulamu kawagola wanhu wake
kuna yamabumbila waitowe na wafalume waja,
nayo kawatowa na kuwawinga mbaka Hoba, ili
ubanzi wa kasikazi wa Damasiki. 16 Kavibweleza
vinhu vose visoligwe na wafalume waja, na
kambweleza Lutu mwihwage, vinhu vake hamwe
na wanaake na wanhu wamwenga.

### *Abulamu kotemiligwa mate na Melikizedeki*

17 Abulamu viyabwelile kulawa kuwahuma
Kedolilaoma na wafalume wamwenga, mfalume
wa Sodoma kahita kuiting'hana nayo hana
dibawe da Shawe, iviya ditangigwa Bawe da
mfalume. 18 Melikizedeki yoyakale mfalume
wa Salemu yoyakalile mkulu wa nhambiko wa
Mulungu Yeli Uchanyha, kamgalila Abulamu
gate na divai. 19 Kamtemela mate Abulamu na
kalonga,

“Abulamu yatemeligwe mate na Mulungu Yeli
Uchanyha,
yalumbile ulanga na isi.
20 Yatunhizigwe Mulungu Yeli Uchanyha,
yoyakutendile uwahume wehi wako.”

Abulamu kamwing'ha Melikizedeki chinhu
chimwe muna ichila vinhu longo viyapatile kuna
ing'hondo.

21 Na mfalume wa Sodoma kamulongela Abu-
lamu, “Niye ning'he wanhu, mbali vinhu ivo sola
weye.”

22 Abulamu kamwidika mfalume wa Sodoma,
“Noilaha haulongozi wa Mndewa Mulungu
Yeli Uchanyha, yalumbile ulanga na isi yose,
23 sizasola lusingija hebu luzabi lwa chilatu, hebu
chinhu chako chochose, muladi sekeulonge kuwa
kunitendeza niwe tajili. 24 Ivo sizasola chochose,
ila ndiya ziya muhala ziwadile wanike na vinhu
viwapatile kuna ing'hondo. Wowolondeka waja
wowakalile hamwe na niye, Aneli na Eshikoli na
Mamule uwaleke wawe na vinhu vawo.”

# 15

### *Mulungu kokwika Lagano na Abulamu*

1 Maabaho mbuli ya Mndewa Mulungu
imwezila Abulamu kwa malaguso, ilonga,
“Sekeudumbe. Niye ni ngawo yako na
nizakugweka.”

2 Mbali Abulamu kamwidika, “Weye Mndewa
Mulungu, kwizaning'ha choni na kuno nogendelela kukala bila mwana na muhazi wangu ni
Eliyazali wa Damasiki?” 3 Abulamu kalonga,
“Lola huning'hile mwana, mtumwa yavumbuke
muna ikaye yangu kezakuwa muhazi wangu.”

4 Maabaho kahulika mbuli ya Mndewa
Mulungu imwizila kaidi: “Ino mtumwa wako
Eliyazali hezakuwa muhazi wako, mbali
mwanago yondaumweleke mwenyewo niiyo
yondayawe muhazi wako.” 5 Mndewa Mulungu
kamulava kunze na kumulongela “Lola kuulanga
na geza kuzipeta nhondo, kwizakuwa na welesi
mwingi fana nhondo izo.”

6 Abulamu kamuhuwila Mndewa Mulungu, na kwa ichimu icho Mndewa Mulungu kanogezigwa nayo na kamtogola kanoga haulongozi hake.

7 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela Abulamu, “Niye niiyo Mndewa Mulungu yonikulavile kulawa Ulu bululu da Wakalidayo, muladi nikwing'he isi ino iwe yako.”

8 Mbali Abulamu kalonga, “Weye Mndewa Mulungu nizavimanyaze kuwa isi ija izakuwa yangu?”

9 Mndewa Mulungu kamulongela Abulamu,
“Nigalile ng'ombe muke wa miyaka mitatu na
mwana luti muke wa miyaka mitatu na bebelu
da ng'hondolo da miyaka mitatu na huwa na
kinda da nziwa.” 10 Abulamu kamgalila Mn-
dewa Mulungu wanyama wawo wose, kabalula
chila mnyama vihande vidi, keka chila chihande
kwa kusonhela miyage, mbali ndege hawakan-
hile. 11 Vilele weza na wema muna imitufi, mbali
Abulamu kawawinga.

12 Zuwa vidikalile doswa, Abulamu kakala na
vuwevuwe da nhongo, ziza totolo dimgubika.
13 Mndewa Mulungu kamulongela Abulamu,
“Uvimanye kuwa welesi wako wezakuwa
nyambenyambe muna iisi siyo yawo na
wezakuwa watumwa na wezagazigwa kwa
miyaka magana mane. 14 Mbali nizawatagusa
wanhu wondawawasang'hanile fana watumwa
na hamwande wezasola vinhu vingi. 15 Weye
mwenyewo kwizakala miyaka mingi, maabaho
kwizadanganika kwa tindiwalo na kuwandigwa.
16 Welesi wako wizabwela hano muna uwelesi

wekane, kwaviya uhasanyi wa Waamoli
haunakuwa mwingi muladi niwataguse.”
17 Zuwa vidiswile na ziza disonga, tanuli di-
fuka yosi na wenge diwoneka na difosa hagati
ya maunde ya nyama. 18 Maabaho Mndewa Mu-
lungu katenda chilagano na Abulamu, kalonga,
“Nolagana kuweng'ha ino welesi wako wose ku-
songela lwanda lwa Misili mbaka lwanda lukulu
lwa Efulati, 19 isi ya Wakeni na Wakenizi na
Wakadimoni 20 na Wahiti na Wapelizi na Walefai
21 na Waamoli na Wakanaani na Wagiligashi na
Wayebusi.”

# 16

*Salayi na Hajili*

1 Salayi muke wake Abulamu kakala
hanakweleka mwana. Kakala na mtumwa wa
chike Mmisili yoyatangigwe Hajili. 2 Salayi
kamulongela Abulamu, “Kuvimanya Mndewa
Mulungu haninogele kupata wana. Lelo
kambandame mtumwa wangu muladi niwapate
wana kufosela yeye.” Abulamu katogola chiya
choyalongile Salayi. 3 Maabaho Salayi kamsola
Hajili mtumwa wake kulawa Misili kamwing'ha
Abulamu yawe fana muke wake. Yano yalawilila
lusita Abulamu viyakalile kuna isi ya Kanaani
miyaka longo. 4 Abulamu kambandama Hajili
nayo kapata wimo. Hajili viyawonile kapata
wimo, kandusa kumwehula Salayi.

5 Salayi kamulongela Abulamu, “Wihi uno uni-
tendiligwa kwizahusika nawo. Niye nikugolela
mtumwa wangu wa chike, mbali viyawile na

wimo kanyehula. Mndewa Mulungu nayahumize
hagati ya niye na weye.”
6 Abulamu kamulongela Salayi, “Mtumwa
wako kahasi yako weye, mtendele choulonda.”
Maabaho Salayi kamgaza Hajili mbaka kaibanga.
7 Msenga wa Mndewa Mulungu kamvika Hajili
kudibwilingu kuna inzasa ya mazi, nzila ya kuhita
Shuli. 8 Na kalonga, “Hajili msang'hani wa Salayi,
kulawa kulihi na kohita kulihi?”

Kamwidika, “Nomkimbila Salayi yonimsang'hanila.”

9 Msenga ija wa Mndewa Mulungu
kamulongela, “Bwela kwa youmsang'hanila
ukamtegeleza.” 10 Maabaho msenga wa Mndewa
Mulungu kamulongela, “Nizakwing'ha welesi
mwingi habule munhu yondayadahe kuwapeta.”
11 Msenga wa Mndewa Mulungu kamulongela,

“Weye kuna wimo na kwizakweleka mwana wa chilume
na zina jake kwizamtanga Ishumaili*,
kwaviya Mndewa Mulungu kohulika manhesa yako.
12 Ishumaili kezakala fana mhunda mbago,
kezakuwa mwihi wa chila munhu,
na chila munhu kezakuwa mwihi wake.
Kezaigola na ndugu zake.”

13 Hajili kamwing'ha zina Mndewa Mulungu
yoyalongile nayo, “Weye ni Mulungu yoniwona.”
Na kalonga, “Kweli niye nimuwona yeye yoni-
wona.” 14 Lekamana nzasa ija yotangigwa Beeli

* 16:11 Ishumaili fambulo jake Mulungu kohulika.

Laha Iloi[†]. Nzasa iyo yahagati ya Kadeshi na
Beledi.
15 Hajili kamwelekela Abulamu mwana wa
chilume. Abulamu kamtanga zina jake Ishumaili.
16 Hajili viyamweleke Ishumaili, Abulamu kakala
na miyaka malongo manane na sita.

# 17

*Lagano na Ulungwana*

1 Abulamu viyakalile na miyaka malongo
kenda na kenda, Mndewa Mulungu kamulawilila
na kamulongela, “Niye ni Mulungu mwene
Udaho. Nitegeleze siku zose na ukale bila ya
kutenda yehile. 2 Nizatenda lagano jangu na
weye na kukwing'ha welesi mwingi.” 3 Abulamu
katumbala mavindi mbaka chihanga chidalisa
hasi. Mulungu kamulongela, 4 “Notenda
lagano dino na weye. Nokulongela kwizakuwa
tata wa makabila mengi. 5 Kwandusila
sambi, hwizatangigwa Abulamu kaidi, mbali
kwizatangigwa Bulahimu, kwaviya nikutenda
uwe tata wa makabila mengi. 6 Nizakwing'ha
welesi mwingii na makabila mengi na wafalume
wezalawa kumwako.
7 “Lagano jangu na weye na welesi wako dabule
uhelelo. Ivo nizakuwa Mulungu wako na Mu-
lungu wa welesi wako. 8 Nizakwing'ha weye na
welesi wako isi ino imuli nyambenyambe sambi.
Isi yose ya Kanaani izakuwa yenu siku zose, na
niye nizakuwa Mulungu wawo.”

[†] **16:14** Beeli Laha Iloi fambulo jake nzasa ya Mulungu yolola na yeli mgima.

9 Maabaho Mulungu kamulongela Bulahimu,
“Weye iviya kolondeka wamhe lagano jangu,
weye na welesi wako wose. 10 Vino niivo
vimulondeka kutenda weye na welesi wako,
chila mulume kolondeka yengizigwe ulungwana.
11 Mwizakwingizigwa ulungwana, na ino
izakuwa chilaguso cha lagano da mweye na
niye. 12 Chila mwana wa chilume wa siku nane
vimuli kolondeka yengizigwe ulungwana na
chila mulume wa welesi wenu, yawe mtumwa
yelekigwe muna ikaye yenu hebu yoyaguligwe
kwa hela zenu kulawa kwa manyambenyambe
13 na chila mwana wa chilume yelekigwe muna
ikaye yako hebu yaguligwe kwa hela kolondeka
yengizigwe ulungwana. Chino chizakuwa
chilaguso muna ulukuli kulagusa kuwa lagano
donikile na weye ni da siku zose. 14 Mulume
yoyose hengizigwe ulungwana kezabaguligwa
na wanhu wake, kwaviya hadikile lagano jangu
bule.”

15 Maabaho Mulungu kamulongela Bulahimu,
“Mke wako hwizamtanga kaidi Salayi, kwan-
dusila sambi zina jake Sala. 16 Nizamtemela
mate, nayo kezakwelekela mwana wa chilume.
Nizamtemela mate Sala, nayo kezakuwa mama
wa makabila mengi na wafalume wa zisi nyingi
wezalawa kumwake.”

17 Bulahimu katumbala mavindi mbaka chi-
hanga chake chidalisa hasi, kaseka na kalonga
muna umoyo wake, “Vino mulume yeli na miyaka
gana kodaha kupata mwana? Vino Sala ko-
daha kupata mwana na miyaka malongo kenda?”
18 Bulahimu kamuuza Mulungu, “Habali hu-

muleka Ishumaili yahazi chiya chounilaganile?”
19 Mulungu kedika, “Siyo. Muke wako Sala keza-
kwelekela mwana wa chilume, nayo kwizam-
tanga Isaka. Nizakwika lagano jangu kumwake
na welesi wake. Ijo ni lagano da siku zose.
20 Nihulika pulo jako kusonhela Ishumaili, ivo
nizamtemela mate na kumwing'ha wana wengi
na welesi mwingii. Kezakuwa tata wa wafalume
longo na waidi, na nizakutenda uwe kabila kulu.
21 Mbali nizakwika lagano jangu kwa mwanago
Isaka, yondayelekigwe na Sala lusita fana luno
mwaka ukwiza.” 22 Mulungu viyakomeleze ku-
longa na Bulahimu, kahita kuchanyha kuulanga.
23 Bulahimu kawasola Ishumaili mwanage
na walume wamwenga wose, wowelekigwe
mwiikaye yake na wowaguligwe kwa hela
zake, kawengiza ulungwana fana Mulungu
viyamulagilize. 24 Bulahimu viyengizigwe
ulungwana kakala na miyaka malongo kenda
na kenda, 25 na Ishumaili mwanage viyengizigwe
ulungwana kakala na miyaka longo na mitatu.
26 Bulahimu na Ishumaili mwanage wengizigwa
ulungwana siku iyo. 27 Walume wose weli muna
ikaye ya Bulahimu, wowelekigwe muna ikaye
yake na wowaguligwe kwa hela, wengizigwa
ulungwana hamwe nayo.

# 18

### *Mulungu kolagusa chilagano chake*

1 Mndewa Mulungu kamulawila Bulahimu heli
na mibiki mikulu ya Mamule. Bulahimu kakala
yakalile hana ulwivi lwa dihena jake lusita lwa

vuke da imisi. 2 Kalola uchanyha na kawawona
wanhu watatu wema habehi nayo. Kawakim-
bilila hima hima kuwahokela, kadulisa ditwi jake
mbaka chihanga chidalisa hasi, 3 na kalonga,
“Wenevale, one munogelwa na niye sekemuifose
kaye yangu bila kwima, nahano muladi nidahe
kuwasang'hanila. 4 Niwagalileni mazi muladi
mudahe kuguma nhende na kuhumula hasi hana
umbiki uno. 5 Kuno mohumula niifunganye ndiya
chidogo muladi muje mpate nguvu ya kugen-
delela na mwanza wenu, kwaviya munizila niye
mtumwa wenu.”

Nawo wamwidika “Vinoga, sang'hana fana
viulongile.” 6 Bulahimu kabwela hima kuna
ihema kamulongela Sala, “Lopola, sola mhishi
tano za usage unogile na uhonde magate.”
7 Maabaho Bulahimu kakimbila kuna dibumbila
da zing'ombe kasagula dang'ang'a dimwe
ng'ombe dinenehe, kamwing'ha msang'hani,
yoyadisasale hima hima. 8 Maabaho Bulahimu
kasola matombo, matombo yagandile na ija
inyama ifunganyigwe, kawasasalila ndiya
manyambenyambe na kawekila, nayo kema
habehi viwakalile woja haja hasi hana umbiki.

9 Maabaho wamuuza, “Kakulihi muke wako
Sala?”

Kawedika, “Kakuja kugati kuna ihema.”

10 Imwe wa nyambenyambe waja kamulon-
gela Bulahimu, “Lusita fana luno mwaka ukwiza
nizakubwelela, na muke wako Sala kezakuwa na
mwana wa chilume.”

Sala kakala hachisogo chake hana ulwivi lwa
ihema kotegeleza. 11 Bulahimu na Sala wakala

walala ng'hani, na Sala kafosa lusita lwa kweleka.
12 Kwa ivo Sala kaseka chimoyomoyo na ka-
longa, “Sambi niye namulala. Lelo nodahaze
kudeng'helela kupata wimo kwa mulumangu yeli
mulala?”
13 Baho Mndewa Mulungu kamuuza Bulahimu,
“Habali Sala kaseka na kalonga, ‘Kweli izadahika
nyeleke mwana na niye mulala?’ 14 Vino kuna
jojose hadidahika kwa Mndewa Mulungu? Lusita
fana luno mwaka ukwiza nizabwela, na Sala keza-
kuwa na mwana wa chilume.”
15 Ivo Sala kadumba, kabela na kalonga, “Sisek-
ile bule.”

Mndewa Mulungu kamulongela, “Ona, kuseka.”

### *Bulahimu kowapulila wanhu wa Sodoma*

16 Maabaho wanhu wawo wasegela wahita
hanhu howadahile kudiwona bululu da Sodoma,
na Bulahimu kawasindikiza. 17 Mndewa Mu-
lungu kalonga, “Nimfise Bulahimu mbuli zondan-
itende? 18 Bulahimu kezakuwa tata wa kabila
kulu, kufosela yeye wanhu wa zisi zose weza-
temeligwa mate. 19 Nimsagula yeye muladi yawa-
fundize wanage na waja wokala muna ikaye
yake kusondelela nzila ya Mndewa Mulungu kwa
kutenda yanogile haulongozi wangu. Na niye
nizamtendela Bulahimu chiya chonimulaganile.”

20 Maabaho Mndewa Mulungu kalonga, “Ni-
hulika kuna mbuli zihile nyingi kwa wanhu wa
Sodoma na Gomola, na uhasanyi wawo ubasanya.
21 Nihumuluke nihite uko nikalole mwenyewo
fana yoniyahulike ni kweli.”

22 Maabaho wanhu waja wasegela na
wahita kusonhela Sodoma mbali Mndewa
Mulungu kasigala na Bulahimu. 23 Bulahimu
kamkwenhukila Mndewa Mulungu kamuuza,
“Vino weye kwizawananga wanhu wanogile
hamwe na wehile? 24 Yahawa muna dibululu
muna wanhu wanogile haulongozi wa Mulungu,
vino kwizadinanga bululu ijo jose? Vino
kwizadinanga bululu jose badala ya kudileka
kwa ichimu cha wanhu wanogile malongo
matano weli umo? 25 Sigesa kuwa kwizatenda ivo,
kuwakoma wanhu wanogile hamwe na wehile,
kuwatendelela wanhu wanogile na wehile. Vino
msemi wa isi yose hatenda yanogile?”

26 Mndewa Mulungu kamwidika, “Nahawafika
wanhu wanogile malongo matano kuja kudibululu da Sodoma nizadileka bululu jose kwa ichimu chawo.”

27 Bulahimu kamulongela kaidi, “Nolamba
unilekelele nilonge na Mndewa, niye nili
matimbwisi na maivu. Niye ni munhu muhala
na sifaya kulonga chinhu chochose. 28 Mbali
huwenda wopatika wanhu wanogile malongo
mane na tano. Ivo kwizadinanga bululu jose
kwaviya waswela wanhu watano?”

Mndewa Mulungu kedika, “Sizadinanga bule bululu one nahawafika wanhu wanogile malongo mane na tano.”

29 Bulahimu kalonga kaidi, “Huwenda kwizakuwa na wanhu wanogile malongo mane?”

Kamwidika, “Sizadinanga bule one kuna wanhu malongo mane.”

30 Bulahimu kalonga, “Nokulamba Mndewa, sekeuwe na ludoko mbali leka nilonge kaidi. One wahawafika wanhu malongo matatu?”

Kamwidika, “Sizatenda ivo bule one nahawafika wanhu malongo matatu.”

31 Bulahimu kalonga, “Kwaviya nikulamba bila ya ludumbo, nokulamba kaidi Mndewa. One wahawafika wanhu malongo maidi muhala?”

Kamwidika, “Sizadinanga bule one nahawafika wanhu malongo maidi.”

32 Bulahimu kalonga, “Nokulamba Mndewa sekeuwe na ludoko, mbali nolamba nilonge kaidi mwanza umwe muhala. Yokuwaze wahawafika wanhu longo muhala?”

Mndewa Mulungu kalonga, “Sizadinanga bule
dibululu ijo one nahawafika wanhu longo.”
33 Mndewa Mulungu viyakomeleze kulonga na
Bulahimu, kasegela, Bulahimu kabwela ukaye.

# 19

### *Wihi wa Sodoma*

1 Wasenga wa kuulanga waidi wafika Sodoma
ichigulogulo, Lutu kakala yakalile hana ulwivi
lwa dibululu. Viyawawone, kahita kuwahohela
na kuwatumbalila mavindi mbaka chihanga chi-
dalisa hasi. 2 Kalonga, “Wenevale wangu, in-
gileni muna ikaye yangu niye msang'hani wenu. Modaha kunawa nhende na kugona chilo cha diyelo, igolo imitondo modaha kusegela na kugendelela na mwanza wenu.”

Mbali wawo wamwidika, “Bule, chizakala chilo chose hano hana ulubuga.”

3 Lutu kawabembeleza ng'hani mbaka
watogola, wahinduka na kwingila muna ikaye
yake. Lutu kawasasalila magate hayagumigwe
lusu na kasasalila dugila kwa manyambenyambe.
Manyambenyambe waja zindiya zisasaligwe.

4 Nyambenyambe wang'hali hawanagona,
walume wa Sodoma waizunguluka kaye ya
Lutu. Walume wose wa bululu diya, wakulu
na wadodo wakala baho. 5 Wamtanga Lutu
kunze na wamuuza, “Wakulihi walume waja
wezile kumwako? Chilavile kunze muladi
chiwabandame.”

6 Lutu kalawa kunze na kahinda ulwivi.
7 Kawalongela, “Mbwiya zangu, nowalamba
sekemutende wihi uno. 8 Mbali ninawo wali waidi
wang'hali mhambe. Lekeni nimwing'heni wawo
na mweye mwizawatenda chochose chimulonda
kuwatenda. Mbali wanhu wano sekemuwatende
chochose, kwaviya wano ni nyambenyambe
wangu, nolondeka niwakalize.”

9 Mbali wawo walonga, “Teng'hu segela hano!
Weye kwa nyambenyambe, na weye kwa yelihi
kochilongela cha kutenda? Koitenda weye kwa
msemi wetu? Ivo chokutenda yehile kufosa wawo
wafosanzila wako.” Wamsung'ha Lutu kuchisogo
wamsegeza mbaka walonda kulubena ulwivi
lwake. 10 Mbali waja iwanhu waidi wowakalile
mgati, wagolosa makono yawo, wamkwesa
Lutu mgati mwa ikaye na kuluhinda ulwivi.
11 Maabaho kawatenda wanhu wose wowakalile
haulwivi watulike yameso, wakulu kwa wadodo,
mbaka hawadahile bule kulupata ulwivi.

### *Lutu kosegela Sodoma*

12 Wanhu waja iwaidi wamulongela Lutu, “One
kuna munhu yoyose yokala hano, wanago wa
chilume na wandele zako na wakoyi hebu ndugu
imwenga yokala muna dibululu, uwalave hanhu
hano himahima. 13 Chizahananga hanhu hano,
kwaviya kuiyalala kwa wanhu wa hano kumfikila
Mndewa Mulungu, nayo kachituma chidinange
bululu da Sodoma.”

14 Maabaho Lutu kawagendela wakoyi zake
wowolonda kuwasola wandele zake na kawa-
longela, “Segeleni hano himahima, Mndewa Mu-
lungu kohananga hanhu hano.” Mbali wawo
wamuwona fana viya kehuka.

15 Vikuchile wasenga waja wa kuulanga
wamulongela Lutu, “Lopola na umsole muke
wako na wano wandele zako waidi muladi
sekemwize kunangigwa lusita bululu dino
vondaditagusigwe.” 16 Mbali Lutu kakalama.
Kwaviya Mndewa Mulungu kamuwonela
ubazi, waja iwasenga wa kuulanga wawamha
Lutu na muke wake na wandele zake waidi,
wawalava mudibululu. 17 Viwakomeleze
kuwalava, imwe wa wasenga waja wa kuulanga
kalonga, “Kimbileni muladi muhonyeke.
Sekemulole kuchisogo na sekemwime muna
dibawe, kimbilileni muna imilima muladi
sekemukomigwe.”

18 Mbali Lutu kamwidika, “Siyo, wenevale
wangu. 19 Muninogela na kunihonya ugima
wangu kwa kunilagusa ulondo. Mbali mil-
ima yakutali, ivo kunangigwa kuno kwizanifika
ning'hali sinafika uko na nizadanganika. 20 Loleni
kuja kuna bululu dodo nodaha kudikimbilila

kwaviya dahabehi. Lelo nilekelele nikimbilile
uko. Diya ni bululu dodo muhala na uko nizaho-
nyeka.”
21 Nayo kamwidika, “Vinoga, nitogola
chiupulile, sizadinanga bululu diya. 22 Kimbila!
Himahima! Sizadaha kutenda chochose mbaka
vondaufike uko.”

Lutu kaditanga bululu ijo “Soali” fambulo jake
“Dodo.”

### *Kunangigwa kwa Sodoma na Gomola*

23 Zuwa dikala dilawile lusita Lutu viyafikile
Soali. 24 Maabaho Mndewa Mulungu kagala
makala ya moto kulawa kuulanga muna yamabu-
lulu ya Sodoma na Gomola. 25 Kayananga mabul-
ulu yayo na bawe jose na wanhu wose wowakalile
uko na mimeya yose yoikalile muna isi. 26 Mbali
muke wake Lutu kalola kuchisogo na kagaluka
mhanda ya munyu.
27 Igolo yake imitondo, Bulahimu kahita
himahima hoyakalile kema haulongozi ha
Mndewa Mulungu. 28 Viyakalile baho, kalola
Sodoma na Gomola na banzi zose za dibawe,
kalola na kawona yosi dofuka kulawa muna isi,
yosi fana viya da tanuli kulu. 29 Baho Mulungu
viyanangile mabululu ya dibawe Lutu hoyakalile
kokala, kamkumbuka Bulahimu kwa kumulava
Lutu muna yamabululu yano, muladi Lutu
sekeyanangigwe.

### *Mwanduso wa Wamowabu na Waamoni*

30 Kwaviya Lutu kakala kodumba kukala Soali,
yeye na wandele zake waidi wasegela kuna
na wahita kukala kuna dituka kuna imilima.
31 Imndele imkulu kamulongela mdodo wake,

“Sambi tati yetu mulala na muna iisi habule mu-
lume wa kuchisola chipate wana fana viili muna
isi. 32 Lelo chimng'wize upele tati yetu muladi
chidahe kwiibandama nayo chimwelekele wana.”
33 Ichilo icho wamng'wiza upele tati yawo, na
imndele imkulu kahita kaibandama nayo. Mbali
tati yake havimanyile bule lusita imndele wake
viyaibandame nayo, kwaviya kakala yakoligwe.

34 Igolo yake imndele imkulu kamulongela im-
dodo, “Niibandama na tata ichilo, Lelo leka
chimng'wize upele kaidi maabaho weye wiiban-
dame nayo, ivo chose chizakweleka nayo wana.”
35 Ivo ichilo icho wamng'wiza upele tati yawo,
maabaho ija imndele imdodo, kahita kaibandama
nayo. Mbali tati yake havimanyile bule lusita mn-
dele wake viyaibandame nayo, kwaviya kakala
yakoligwe. 36 Kwa nzila ino wandele wose wa
Lutu weng'higwa wimo na tati yawo. 37 Imndele
imkulu keleka mwana na zina jake kamtanga
Moabu, iyo niiyo wasaho yawo Wamoabu mbaka
diyelo. 38 Imndele imdodo iviya keleka mwana
na zina jake kamtanga Benami. Iyo niiyo wasaho
yawo Waamoni mbaka diyelo.

# 20

### *Bulahimu na Abimeleki*

1 Bulahimu kasegela kahita ubanzi wa Negebu,
kakala Gelali hagati ya Kadeshi na Shuli kwa
lusita. 2 Bulahimu kalonga kuwa Sala kakala
lumbu jake. Ivo mfalume Abimeleki wa Gelali
kamsola Sala. 3 Mbali ichilo Mulungu kamulaw-
ilila Abimeleki muna zinzozi na kamulongela,

“Kwizadanganika kwaviya kumsola muke ino,
yoyamalile kusoligwe.”

4 Mbali Abimeleki hambandame Sala na
kalonga, “Mndewa, niye ninoga haulongozi
wako! Vino kwizaninanga niye na kabila jangu?
5 Bulahimu mwenyewo kalonga kuwa kakala
lumbu jake, Sala iviya kalonga ivo ivo. Nitenda
voilondeka na sisang'hane wihi.”

6 Mulungu kamwidika Abimeleki muna zin-
zozi, “Vinoga, novimanya kuwa yayo youtendile
yanoga muumoyo, ivo nikugomesa sekeuniten-
dele uhasanyi na sikulekile umdalise muke iyo.
7 Mbali lelo mbweleze muke iyo kwa mulumake,
Bulahimu ni mulotezi wa Mulungu nayo kezaku-
tosela, hwizadanganika bule. Mbali one humb-
weleze, nokuzuma uvimanye kwizadanganika
weye na wanhu wako wose.”

8 Imitondo ng'hani Abimeleki kawatanga
wasang'hani wake wose na kawalongela mbuli
zose zozilawilile, nawo wadumba ng'hani.
9 Maabaho Abimeleki kamtanga Bulahimu na
kamuuza, “Kuchitendela choni? Nikubananga
choni mbaka kunitenda niwe habehi na
kutenda uhasanyi niye na ufalume wangu?
Kunitendela mbuli za mdukula hazifaya bule
kusang'hanigwa.” 10 Abimeleki kamuuza
Bulahimu, “Habali kusang'hana ivo?”

11 Bulahimu kamwidika, “Nitenda ivo kwaviya
nigesa hanhu hano habule munhu yomdumba
Mulungu, iviya mwahadahile kunikoma muladi
mumsole muke wangu. 12 Iyo kweli ni lumbu
jangu. Yeye ni mwana wa tati yangu, mbali siyo

mwana wa mami yangu, na nimsola. 13 Lusita Mu-
lungu viyanisegeze muna ikaye ya tati yangu na
kunigala kuna iisi imwenga, nimulongela muke
wangu, ‘One uhanilonda, hohose hondachihite
umulongele chila munhu kuwa weye ni lumbu
jangu.’ ”
14 Maabaho Abimeleki kambweleza Sala kwa
Bulahimu, iviya kamwing'ha ng'hondolo na
ng'ombe na watumwa wa chilume na watumwa
wa chike. 15 Maabaho Abimeleki kamulongela
Bulahimu, “Lola isi ino yose yangu, kala hohose
houlonda.” 16 Maabaho Abimeleki kamulongela
Sala, “Nomwing'ha lumbu jako vihande magana
longo va hela, kuwalagusa wose weli hamwe
na weye kuwa kunoga haulongozi wa Mulungu.
Chila munhu yavimanye kuwa kwabule wihi.”
17 Maabaho Bulahimu kampula Mulungu, na
Mulungu kawahonya Abimeleki na muke wake
na watumwa wake wa chike, ivo weleka wana.
18 Mana Mndewa Mulungu kawatenda wanhu wa
kaye ya Abimeleki sekeweleke wana, kwa ichimu
cha Sala muke wa Bulahimu.

# 21

### *Kwelekigwa kwa Isaka*

1 Mndewa Mulungu kamtemela mate Sala
fana viyamulongele. 2 Sala kapata wimo na
kamwelekela Bulahimu mwana viyakalile
mulala. Imwana kelekigwa lusita luja Mulungu
loyalongile kezakwelekigwa. 3 Bulahimu
kamtanga zina jake Isaka, 4 Isaka viyakalile na
siku nane, Bulahimu kamwingiza ulungwana
fana Mulungu viyamulagilize. 5 Bulahimu

kamweleka Isaka viyakalile na miyaka gana.
6 Sala kalonga, “Mndewa Mulungu kanigalila
deng'ho na seko. Chila yondayahulike mbuli ino
kezaseka na niye.” 7 Maabaho Sala kongezela
kulonga, “Yelihi yahadahile kumulongela
Bulahimu kuwa niye Sala nizakong'heza wana?
Mbali nimwelekela mwana wa chilume muna
ulala wake.”
8 Imwana kakula, na siku viyalekezigwe
kong'ha, Bulahimu katenda dugila kulu.

### *Hajili na Ishumaili wowingigwa*

9 Siku dimwe Sala kamuwona Ishumaili mwana
wa Bulahimu yoyelekigwe na Hajili Mmisili,
koseka. 10 Sala kawawona na kamulongela
Bulahimu, “Msegeze mtumwa ino na mwanage.
Mwana wa mwanamke mtumwa hadaha kuhazi
hamwe na mwanangu Isaka.” 11 Mbuli ino
imguma luholozi ng'hani Bulahimu, kwaviya
Ishumaili nayo iviya kakala mwanage. 12 Mbali
Mulungu kamulongela Bulahimu, “Sekeuwe na
luholozi kwa ichimu cha mwana ino na Hajili
mami yake. Mbuli yoyose yondayakulongele
Sala uitende, kwaviya kufosela Isaka kwizakuwa
na welesi wonikulaganile. 13 Iviya nizampatila
wana wengi, mwana wa mtumwa wako wa chike,
nizamwing'ha makabila mengi kwaviya iyo nayo
mwanago.”
14 Igolo yake imitondo Bulahimu kamwing'ha
Hajili ndiya na nongo imemile mazi. Kamtwika
mwanage mdiyega na kumuwinga hamwe na
mami yake. Wasegela na wengila muna dib-
wilingu da Belisheba. 15 Mazi viyamalile yose
muna inongo, kamuleka imwana hasi ya mbiki

mguhi. 16 Nayo kahita kumgwazo utali wa mag-
ulu gana. Kuno kolongelela kuna umoyo wake,
“Sidaha bule kumuwona mwanangu viyodan-
ganika.” Hajili viyakalile kumgwazo kandusa
kulila kwa dizi kulu.
17 Mulungu kamuhulika imwana kolila, msenga
wa Mulungu kulawa kuulanga kamulongela Ha-
jili, “Kuna uzidilwa waki Hajili? Sekeudumbe kwa
viya Mulungu kahulika imbwanga viyolila. 18 Ima
na umwinule imwana vinogile, mana nizamtenda
yawe wasaho wa makabila mengi.” 19 Maabaho
Mulungu kamgubula yameso Hajili, nayo kawona
sima da mazi. Kahita na kaimemeza mazi in-
ongo na kamwing'ha mwanage. 20 Mulungu kawa
hamwe na imwana, nayo kakula, kakala muna
dibwilingu da Palani, iviya kakala galu wa kutowa
misale. 21 Kakala kuna dibwilingu da Palani,
mami yake kamsolela muke kulawa isi ya Misili.

*Lagano da Bulahimu na Abimeleki*

22 Chipindi icho Abimeleki hamwe na
Fikoli mkulu wa wakalizi wake, kamulongela
Bulahimu, “Mulungu kahamwe na weye kwa
chila chinhu chiutenda. 23 Ivo ilahile kwa
zina da Mulungu kuwa hwizanivwizila niye
na wanangu na welesi wangu. Fana niye
viniwile mwaminika kumwako, ivo na weye
uwe mwaminika kumwangu na kwa isi yuukala.”
24 Bulahimu kalonga, “Noilaha.”
25 Maabaho Bulahimu kamulongela Abimeleki
kwa ichimu cha sima diya dowamuhokile wa-
tumwa wa Abimeleki. 26 Mbali Abimeleki kamu-
longela, “Niye sivimanyile bule yelihi yoyatendile
vino. Na weye hunilongele bule mbuli zino, hebu

sinahulika mbuli zino mbaka diyelo.” 27 Maabaho
Bulahimu kasola ng'hondolo na ng'ombe lume na
kamgolela Abimeleki, nawo waidi weka lagano.
28 Bulahimu kawabagula wanang'hondolo wa
chike saba, 29 Abimeleki kamuuza Bulahimu, “Ha-
bali kutenda ivo?”

30 Bulahimu kamwidika, “Wanang'hondolo
wano wa chike saba, nokwing'ha kwa mkono
wangu mwenyewo muladi iwe ukalangama
kuwa niye iyo nihimbile sima dino.” 31 Hanhu
baho hatangigwa Belisheba, fambulo jake, “Sima
da kuilahila.”

32 Viwakomeleze kutenda lagano uko
Belisheba, Abimeleki na Fikoli yakalile mkulu
wake wa wakalizi wasegela kubwela kuna
iisi ya Wafilisiti. 33 Bulahimu kahanda mbiki
woutangigwa tamalisiki uko Belisheba na
katambika kwa zina da Mndewa Mulungu,
Mulungu wa siku zose. 34 Bulahimu kakala muna
iisi ya Wafilisiti kwa siku nyingi.

# 22

### *Mulungu komgeza Bulahimu*

1 Viyafosile yayo Mulungu kamgeza Bulahimu.
Kamulongela, “Bulahimu!” Nayo Bulahimu
kamwidika, “Nabaha!”

2 Mulungu kamulongela, “Umsole Isaka
mwanago nyachende youmulonda na
uhite mbaka isi ya Moliya na umulave
nhosa ya kutimbuliga muna mulima uja
wondanikulongele.”

3 Imitondo ng'hani Bulahimu kalamka na kam-
papiza mbahasha chihongwe wake na kawa-
sola wasang'hani wake waidi na Isaka mwanage,
kahita kukanha ngodi kwa ichimu cha nhambiko
ya kutimbula. Maabaho wahita hanhu hoyalon-
geligwe na Mulungu. 4 Siku yetatu Bulahimu
kenula yameso yake na kahawona hanhu baho
kwa kutali. 5 Maabaho Bulahimu kawalongela
wasang'hani wake, “Kaleni hano hamwe na ichi-
hongwe, niye na ino imbwanga chohita kuja
mchanyha kutosa maabaho chizawabwelela mw-
eye.”

6 Bulahimu kasola zingodi kamtwika Isaka
mwanage kwa ichimu cha nhosa ya kutimbu-
ligwa na Bulahimu kasola moto na mwele, wose
waidi wahita hamwe. 7 Isaka kamulongela tati
yake, “Tata!”

Bulahimu kamwidika, “Aino mwanangu, ko-
longaze?”

Isaka kamuuza, “Moto na ngodi ivo vino,
mbali ng'hondolo wa nhambiko ya kutimbula
kakulihi?”

8 Bulahimu kamwidika, “Mulungu mwenyewo
kezaning'ha ng'hondolo wa nhambiko ya kutim-
bula.” Wawo waidi wagendelela na umwanza.

9 Viwafikile hanhu baho Mulungu hoyamu-
longele, Bulahimu kazenga lupango na kwika
ngodi uchanyha yake. Maabaho kamfunga Isaka
mwanage na kamtambalisa uchanyha ya zingodi
muulupango. 10 Bulahimu kawinula mwele wake
kumchinja mwanage. 11 Mbali msenga wa Mn-
dewa Mulungu kamtanga kulawa kuulanga, “Bu-
lahimu, Bulahimu!”

Bulahimu kamwidika, “Nabaha.”
12 Msenga wa Mndewa Mulungu kamulongela, “Sekeumulumize imwana, hebu sekeumtendele chinhu chochose,” Lelo nivimanya weye komtegeleza Mulungu, kwaviya hunimile bule mwanago nyachende.

13 Bulahimu kenula meso na kawona bebelu da ng'hondolo dinamata mhembe zake kuna ichisolo, Bulahimu kahita na kamsola, kamulava nhambiko ya kutimbula badala ya mwanage.
14 Bulahimu kahatanga hanhu baho, “Mndewa Mulungu kaning'ha.” Mbaka diyelo wanhu wolonga, “Muna mulima wa Mndewa Mulungu wanhu wokwing'higwa.”

15 Msenga wa Mndewa Mulungu kulawa kuulanga kamtanga Bulahimu mwanza wekaidi,
16 kamulongela, “Mndewa Mulungu kolonga vino, ‘Niilaha kwa zina jangu mwenyewo kuwa kwaviya kutenda vino, hebu hunimile mwanago yaidumwe, 17 ivo nizakutemela mate na nizawongezela welesi wako fana viya nhondo za kuulanga na fana viya msanga uli mumgwazo ya bahali. Welesi wako wezayasola mabululu ya wehi wawo. 18 Kufosela welesi wako makabila yose yezatemeligwa mate, kwaviya kunitegeleza.’
” 19 Bulahimu kawabwelela wasang'hani wake, na wabwela wose hamwe mbaka Belisheba, hanhu hoyakalile Bulahimu.

*Wana wa Naholi*
20 Viyafosile yayo Bulahimu kalongiligwa kuwa Milika kamwelekela wana Naholi sekulu wake, 21 mwanage chaudele katangigwa Usi na wamwenga Busi na Kemueli tati yake Alamu,

22 Kesedi na Hazo na Pilidashi na Yidilafu na
Besueli. 23 Besueli kamweleka Lebeka, Milika
kamweleka Naholi, ndugu yake Bulahimu, wana
wawo wanane. 24 Na Leuma mtumwa wa chike
wa Naholi yoyamtendile fana muke wake, iviya
kamwelekela wana, Teba na Galamu na Tahalashi
na Maaka.

# 23

*Ifa ya Sala*

1 Sala kakala miyaka gana na malongo maidi na
saba. 2 Sala kadanganika uko Kiliasi Aliba, iviya
yotangigwa Hebuloni, muna iisi ya Kanaani, na
Bulahimu kamtendela tanga na kamulililа.

3 Bulahimu kasegela hanhu hautambalisigwe
ulukuli lwa muke wake, kahita kwa Wahiti na
kawalongela, 4 “Niye nyambenyambe, yonikala
hano hamwe na mweye, nichuuzileni hanhu
ha kuwandila muladi nidahe kumuwanda muke
wangu na wanhu wa kabila jangu.”

5 Wahiti wamwidika Bulahimu, 6 “Mwenevale
chitegeleze, weye ni mulangulizi mkulu yousag-
uligwe na Mulungu kumwetu. Muwande muke
wako muna dileme jojose dondaudisagule. Hab-
ule munhu yoyose yondayakwime leme jake,
hebu kukugomesa sekeumuwande muke wako.”

7 Maabaho Bulahimu kema na kainama haulon-
gozi ha Wahiti, wanhu wa isi ija 8 kawalongela,
“Yahawa munitogolela niwawande wanhu wa
kabila jangu, nolamba mpuleni Efiloni mwana
wa Sohali 9 yanichuuzile tuka da Makipela dili
habehi na imhaka ya mgunda wake. Mulonge-
leni yanichuuzile nitende maleme yanichuuzile
kwa beyi yoilondeka hano hano kuno molola.”

10 Efiloni mwenyewo kakala imwe wa Wahiti
wawo wowakalile waiting'hana hana ulwivi lwa
dibululu. Ivo Efiloni Muhiti kamwidika Bulahimu
haulongozi ha wanhu wose wowakalile baho,
11 "Unitegeleze, mwenevale, nokwing'ha mgunda
wose na tuka dili umo, ivo nokugolela kuno
wakaya wayangu wolola, udahe kuwawanda
wanhu wa kabila jako."

12 Bulahimu kainama haulongozi ha wanhu wa
isi ija 13 na kamulongela Efiloni kuno wanhu
wose wohulika, "Unihulike nokulamba, nizagula
mgunda wako, nokulamba uhokele maliho yano,
nidahe kuwawanda wanhu wa kabila jangu."

14 Efiloni kamwidika Bulahimu, 15 "Mwenevale
nitegeleze, mgunda wa magana sehekeli* mag-
ana mane ya hela. Ni choni hagati yako na
niye? Wawande wanhu wa kabila jako umo."
16 Bulahimu waitogolela na Efiloni, kamulingila
chibugulu cha hela chiyalondile kuno Wahiti
wose wolola, shekeli magana mane ya hela,
chiyasi cha wachuluzi wa chipindi icho.

17 Ivo mgunda wa Efiloni uli uko Makipela
habehi na Mamule, tuka dodikalile umo muun-
gunda na mibiki yose ikalile hamwe na mwela
wose diwa jake 18 Bulahimu haulongozi wa Wahiti
wose wowaiting'hane hana ulwivi wa dibululu.

19 Maabaho Bulahimu kamuwanda Sala muke
wake muna dituka ijo dili Makipela habehi na isi
ya Mamule, niiyo Hebuloni, muna iisi ya Kanaani.
20 Mgunda na tuka dodikalile umo, itogoleka na
Wahiti ni hanhu ha Bulahimu ha kuwandila.

* **23:15** Shekeli imwe sawa na gilamu longo na imwe na nusu.

# 24

*Isaka kosola muke*

1 Bulahimu kakala mulala ng'hani, na Mndewa
Mulungu kamtemela mate kwa chila chinhu choy-
atendile. 2 Bulahimu kamulongela msang'hani
wake yoyakalile mulala, iviya ndolezi wa vinhu
vake vose, “Nokulamba wike mkono wako hasi
ya mawambo yangu*, nikulahize. 3 Nolonda
kukulahiza kwa Mndewa Mulungu, Mulungu wa
ulanga na isi, kuwa hwizamsolela mwanangu
muke kulawa kwa Wakanaani wonikala nawo.
4 Kolondeka uhite kuna isi ija yonyelekiligwe na
umsolele muke mwanangu Isaka kulawa mwa
ndugu zangu.”

5 Ija imsang'hani kamuuza, “Fana imndele
hezatogola bule kwiileka kaye na kunisondelela
kwiza kuno kwiisi ino, lelo nimgale mwanago
kuna isi youlawile?”

6 Bulahimu kamwidika, “Uteganye, sekeumb-
weleze mwanagu uko! 7 Mndewa Mulungu, Mu-
lungu wa ulanga kanigala kulawa kaye ya tati
yangu na kulawa isi ya ndugu zangu, kanilon-
gela na kanilahila kuwa kezaweng'ha isi ino we-
lesi wangu. Kezamtuma msenga wake wa kuu-
langa kuulongozi wako, ivo kwizampatila muke
mwanangu kulawa kuna iisi iyo. 8 One imn-
dele halonda kwiisondelela na weye, basi kwiz-
alekeleligwa chilaho icho. Mbali kwa vovose
mwanangu sekeumbweleze uko.” 9 Msang'hani
keka mkono wake hasi ya diwambo da Bulahimu
mwenevale wake, na kumulahila kwa mbuli iyo.

---

* **24:2** Vino niivo viwatendaga wanhu wa umwaka wahaikila
chilaho.

10 Maabaho msang'hani kasola wanyama
wotangigwa ngamiya longo wa Bulahimu, na
ndolendole zinogile mbasakanyo, na kahita
kuna dibululu da Mesopotamiya mbaka buluu
da Naholi. 11 Viyafikile, kawatumbaliza mavindi
iwangamiya habehi na disima kunze ya dibululu,
ikala ichigulogulo, chipindi wanaake wohita kuna
disima kudeha mazi. 12 Kampula Mulungu, "Weye
Mndewa Mulungu, Mulungu wa mwenevale
wangu Bulahimu, diyelo nolonda ufanikiwe
na ulaguse ulondo wa kufunya umoyo kwa
mwenevale wangu. 13 Nahano hamgwazo ha
inzasa ya mazi hanhu wandele wakaya wa
bululu howokwiza kudeha mazi. 14 Ija imndele
yondanimulongele yanenule nongo yake ya
mazi na kuning'ha ning'we, nayo yahaning'ha
ning'we niye na ngamiya wangu, iyo niiyo
youmsagulile msang'hani wako Isaka. One
ihawa ivo, nizavimanya kulagusa ulondo wako
wa kufunya umoyo kwa mwenevale wangu."

15 Yang'hali hanakomeleza kulonga, Lebeka
kafika na kuno kaitwika nongo ya mazi muna
diyega jake. Mwana wa chike wa Besueli mwana
wa Milika, muke wa Naholi, Naholi ni ndugu
wa Bulahimu. 16 Mndele iyo kakala lumondo
na kakala mhambe yang'ali hanaibandama na
mulume yoyose. Ivo kagidimila muna disima,
kadeha nongo yake na kalawa. 17 Msang'hani
kakimbila himahima kuiting'hana nayo na ka-
longa, "Nokulamba uning'he mazi ning'we ku-
lawa muna inongo yako."

18 Imndele kamwidika, "Haya, ing'wa

mwenevale," bahobaho kanenula nongo yake,
kayamhilila na kumng'wiza. 19 Viyakomeleze
kumwing'ha yamazi, kamulongela, "Iviya
nizawadehela mazi ngamiya wako wang'we
mbaka ng'hilu imale." 20 Chahimahima
kayaguma yamazi ya inongo yake muna diziga da
kung'wila zingamiya, na kakimbila kuna inzasa
kudeha mazi yamwenga na kaweng'ha ngamiya
wake wose. 21 Msang'hani ija wa Bulahimu
halongile mbuli yoyose, mbali kakala yomulola
yawone fana Mndewa Mulungu kautemela mate
mwanza wake.

22 Viyakomeleze kuweng'ha ngamiya mazi,
msang'hani wa Mndewa Mulungu kasola mhete
ya zahabu iguligwe hela ng'hulu na kamwing'ha
Lebeka, na makung'u maidi ya zahabu yazamile
ng'hani, kamvaza muna yamakono yake.
23 Kalonga, "Nokulamba unilongele, vino weye
tati yako yelihi? Vino muna ikaye ya tati yako
muna chiheleto cha kugona?"

24 Lebeka kamwidika, "Tati yangu ni Besueli
mwana wa Milika muke wa Naholi. 25 Iviya
kumwetu kuna mgina na hanhu ha kuchungila na
chiheleto cha kugona."

26 Maabaho msang'hani wa Bulahimu
kainama na katambikila kwa Mndewa Mulungu.
27 Kalonga, "Yatunhizigwe Mndewa Mulungu,
Mulungu wa mwenevale wangu Bulahimu niiyo
yang'hali hanazimiza ulondo wake wa kufunya
umoyo na kwaminika kwake kwa mwenevale
wangu. Mndewa Mulungu kanilanguliza mbaka
kwa ndugu wa mwenevale wangu."

28 Mndele ija kakimbila kuhita kuna ikaye ya
mami yake na kumulongela mbuli zose. 29 Lebeka
kakala na lumbu jake yatangigwe Labani, Labani
kakimbila kuhita kuna inzasa kuja kuyakalile
msang'hani wa Bulahimu. 30 Labani viyaiwonile
ija imhete na dikung'hu muna yamakono ya
mwali wake, na kuzihulika mbuli Lebeka ziya-
longiligwe na munhu iyo. Labani kamfika munhu
iyo kema habehi na ngamiya wake hamgwazo
wa inzasa. 31 Labani kamulongela, "Izo. Weye
munhu utemeligwe mate na Mndewa Mulungu.
Habali kokwima hano hanze? Nisasala chiheleto
na hanhu ha kukala ngamiya wako."

32 Msang'hani iyo wa Bulahimu kengila
muikaye, nayo Labani kawafungula iwangamiya
wake na kaweng'ha mgina na hanhu ha kugona.
Maabaho kamwing'ha mazi ya kuguma nhende
yeye na wanhu wake. 33 Viwamgalile ndiya,
msang'hani ija kalonga, "Sizakuja bule mbaka
nilonge mbuli yangu."

Labani kamwidika, "Haya longa."

34 Ivo kalonga, "Niye namsang'hani wa
Bulahimu. 35 Mndewa Mulungu kamtemela mate
mwenevale wangu, na kamtenda munhu tajili
ng'hani. Kamwing'ha mabumbila ya ng'hondolo
na luti na ng'ombe na hela na zahabu, wanaake na
walume na watumwa na ngamiya na vihongwe.
36 Sala, muke wa mwenevale wangu, viyakalile
mulala kamwelekela mwana mwenevale wangu,
kamwing'ha mwana iyo vinhu vake vose.
37 Mwenevale wangu kanilahiliza kwamha
lagilizo jake. Kalonga, 'Sekeumsolele muke
mwanangu kulawa muna iisi ya Kanaani

yonikala. 38 Mbali hita kwa wanhu wa tati
yangu na kwa ndugu zangu umsolele muke
mwanangu.’ 39 Na nimuuza mwenevale wangu,
‘One yahalema kwiza na niye?’ 40 Kedika,
‘Mndewa Mulungu, yonimtegeleza siku zose,
kezakugalila msenga wa kuulanga na kukutenda
ufanikiwe. Kwizamsolela muke mwanangu
kulawa muna ikaye ya tati yangu na ndugu
zangu. 41 Kuna nzila imwe muhala ya kukutenda
uilegehe na chilaho chako, one uhahita kwa
ndugu zangu na wahakulema, kwizakuwa
kuilegeha.’

42 “Diyelo vinifikile hana inzasa, nitosa, ‘Mn-
dewa Mulungu, Mulungu wa mwenevale wangu
Bulahimu, unitende nipate choniwinzile muna
umwanza wangu. 43 Hano nahana inzasa. One
mndele yaheza kudeha mazi, nizampula mazi
ya kung'wa kulawa muna inongo yake. 44 Nayo
one yahaning'ha na kuwadehela mazi ngamiya
wangu, iyo niiyo yasaguligwe na Mndewa Mu-
lungu kuwa muke wa mwana wa mwenevale
wangu.’ 45 Ning'hali sinakomeleza kutosa muna
umoyo wangu, lola! Lebeka kalawilila na nongo
yake ya mazi muna diyega, kagidimila muna in-
zasa na kudeha mazi. Na niye nimpula, ‘No-
lamba uning'he mazi ning'we.’ 46 Nayo ka-
nenula nongo yake himahima na kalonga, ‘Haya
ing'wa na nizawang'wiza mazi iviya ngamiya
wako.’ Ivo niye ning'wa na ngamiya wangu
iviya wang'wizigwa. 47 Ivo nimuuza mndele iyo,
‘Vino weye tati yako yelihi?’ Nayo kanidika,
‘Tati yangu ni Besueli mwana wa Milika muke

wa Naholi.' Maabaho nimwing'ha mhete ndodo
ya kwika muna imhula na kumvaza kung'hu
muna yamakono. 48 Niidulika mbaka chihanga
chidalisa hasi na kumwing'ha hewela Mndewa
Mulungu na Mndewa Mulungu kamtemela mate,
Mulungu wa mwenevale wangu Bulahimu, yoy-
anilongoze vinogile muinzila kumsola mndele ino
kwa ichimu cha mwana wa mwenevale wangu.
49 Lelo nilongeleni one mutogola kumtendela
mwenevale wangu kwa uwaminika na voilon-
deka na one siivo longeni, na niye nizavimanya
cha kutenda."

50 Maabaho Labani na Besueli wamwidika,
"Mbuli ino ilawa kwa Mndewa Mulungu, cheye
chabule cha kukulongela chihile hebu chinogile.
51 Lebeka iyo baho, umsole uhite nayo. Yakawe
muke wa mwana wa mwenevale wako, fana viya
Mndewa Mulungu viyalongile." 52 Msang'hani
wa Bulahimu viyahulike mbuli izo, kainama na
kamtambikila Mndewa Mulungu. 53 Msang'hani
iyo wa Bulahimu kalava viwalo na via va hela na
mahambo ya zahabu na kamgolela Lebeka. Iviya
kamgolela ndolendole za hela ng'hulu lumbu jake
na mami yake Lebeka.

54 Maabaho msang'hani wa Bulahimu na
wanhu wowezile nayo waja wang'wa na wakala
na kugona ichilo chose. Viwalamuke imitondo,
msang'hani kalonga, "Nilekeni nibwele kwa
mwenevale wangu."

55 Mbali lumbu jake Lebeka na mami yake wa-
longa, "Muleke imndele yakale na cheye kwa
juma dimwe hebu siku longo, maabaho kodaha
kuhita."

56 Mbali msang'hani kawalongela, “Nolamba sekemunikalamize, kwaviya Mndewa Mulungu kautemela mate mwanza wangu kamala, lekeni nibwele kwa mwenevale wangu.” 57 Wawo
walonga, “Leka chimtange mndele mwenyewo
chimuuze.” 58 Ivo wamtanga Lebeka na wamuuza, “Kolonda kuhita na munhu ino?”

Nayo kedika, “Ona nizahita.” 59 Ivo wamuleka Lebeka yahite na msang'hani wa Bulahimu na wanhu wake. Iviya waisondelela na yaya wa
Lebeka. 60 Wamtemela mate Lebeka kwa mbuli ino, “Weye mwali wetu uwe mama wa wanhu wengi ng'hani! Welesi wako wasole mabululu ya wehi wawo!”
61 Maabaho Lebeka na wasang'hani wake wa chike waisasala na wakwela ngamiya na kumsondelela iyo imsang'hani wa Bulahimu, nawo wose wasegela.

62 Lusita ulo Isaka kakala kasegela uko Beeli laha iloi, kakala kokala ubanzi wa Negebu.
63 Ichigulogulo Isaka kasegela na kahita kumgunda kugesa na kawona ngamiya wokwiza.
64 Lebeka viyamuwone Isaka, kahumuluka muna
ingamiya wake 65 na kamuuza msang'hani wa Bulahimu, “Munhu ija yelihi yogenda mumgunda yokwiza kuchihowela?”

Msang'hani kamwidika, “Ni mwenevale wangu.” Maabaho Lebeka kasola chitambala kaigubika ichihanga.

66 Msang'hani wa Bulahimu kamulongela Isaka
chila chinhu choyatendile. 67 Maabaho Isaka kamsola Lebeka mbaka muna ihema da Sala

mami yake, na kawa muke wake. Isaka ka-
mulonda Lebeka yoyamsangalaze viyadanganike
mami yake.

# 25

### *Welesi umwenga wa Bulahimu*

1 Bulahimu kasola muke imwenga, zina jake Ke-
tula. 2 Muke iyo kamwelekela Bulahimu Zimulani
na Yakishani na Medani na Midiani na Ishibaki na
Shuwa. 3 Yakishani kamweleka Sheba na Dedani,
wana wa Dedani ni Waashulu na Waletusi na
Waleumi. 4 Wana wa Midiani wakala Efa na Efeli
na Henoki na Abida na Elidawa. Wose wawo
wakala welesi wa Ketula.
5 Bulahimu kamwing'ha Isaka vinhu vake vose,
6 mbali wana wa watumwa wake wakalile fana
wanaake zake wowamwelekele wana kawagolela
ndolendole viyakalile yang'hali hanadanganika,
kawagala kuna iisi ya ulawilo wa zuwa, kutali na
mwanage Isaka.

### *Ifa ya Bulahimu*

7 Bulahimu viyadanganike kakala na miyaka
gana na malongo saba na tano. 8 Bulahimu kadan-
ganika mulala ng'hani na kakala na deng'ho,
kahita kuilumba na wasaho zake. 9 Wanage,
Isaka na Ishumaili wamuwanda umo muna di-
tuka da Makipela ulawilo wa zuwa wa Mamule
mumgunda woukale wa Efiloni, mwana wa So-
hali Muhiti. 10 Bulahimu na Sala muke wake
wawandigwa kuna umgunda uja Bulahimu uyag-
ulile kwa Wahiti. 11 Viifosile ifa ya Bulahimu,

Mulungu kamtemela mate Isaka mwana wa Bulahimu, yoyokalile kakala habehi na disima da Beeli laha iloi.

### *Wana wa Ishumaili*

12 Uno uwo ludongo lwa welesi wa Ishumaili
mwana wa Bulahimu yoyelekigwe na Hajili
Mmisili, yoyakalile msang'hani wa chike wa Sala.
13 Yano yayo yamazina ya wana wa Ishumaili kwa
kusondelela kwelekigwa kwawo, chaudele wa
Ishumaili ni Nebayoti na wamwenga ni Kedali na
Abideli na Mibisamu 14 na Mishima na Duma na
Masa 15 na Hadadi na Tema na Yetuli na Nafishi
na Kedema. 16 Wano ni wana wa Ishumaili,
wowakalile walangulizi wa makabila longo na
waidi. Ukazi na vibululu vawo vimanyika kwa
mazina yawo. 17 Ishumaili viyadanganike kakala
na miyaka gana na malongo matatu na saba,
kahita kuiting'hana na wasaho zake. 18 Welesi
wa Ishumaili wakala hagati ya Havila na Shuli,
habehi na Misili mwiinzila ya kuhita Ashulu.
Wakala kwa kuigola na welesi umwenga za
Bulahimu.

### *Kwelekwa kwa Esau na Yakobo*

19 Uno ulo ludongo lwa welesi wa Isaka
mwana wa Bulahimu. Bulahimu kamweleka
Isaka 20 Isaka kakala na miyaka malongo mane
viyamsolile Lebeka mwana wa Besueli, Mwalamu
wa Padani Alamu. Lebeka kakala lumbu wa
Labani. 21 Lebeka kakala halela, ivo Isaka
kampula Mndewa Mulungu, nayo Mndewa
Mulungu kamwidika chiyapulile, ivo Lebeka
kapata wimo. 22 Wimo uwo ukala na mambasa,
wana wawo waihuma muinda ya Lebeka. Nayo

kalonga, “Chino choni chochinilawilila?” Ivo kahita kumuuza Mndewa Mulungu.
23 Mndewa Mulungu kamulongela Lebeka,
“Muinda yako muna makabila maidi,
Makabila maidi yondayelekigwe na weye yezaigola.
Dimwe dizakuwa na nguvu kufosa dimwenga;
Imkulu kezamsang'hanila imdodo.”
24 Lusita lwake lwa kuvumbula vilufikile,
kavumbula mambasa. 25 Chaudele kelekigwa
na mbende ndung'hu na lukuli lwake lose lukala fana walo dili na mazoya, ivo zina jake kamtanga
Esau. 26 Wekaidi kavumbuka kuno kamhilila
chisiginho cha Esau, ivo zina jake katangigwa Yakobo. Esau na Yakobo viwavumbuke Isaka kakala na miyaka malongo sita.

### *Esau kochuuza haki ya uchaudele wake*

27 Wana wawo wakula. Esau kakala mkala, yoyolonda kukala muna ivyuwala, na Yakobo
kakala yaholile yolonda kukala hakaye. 28 Mbali
Isaka kamulonda Esau, kwaviya kanogelwa kuja wanyama woyawakomile Esau, mbali Lebeka kamulonda Yakobo.
29 Siku dimwe Yakobo kakala yokwambika ndiya, Esau keza kulawa kuukala kuno kana
nzala, 30 ivo kamulongela Yakobo, “Nina
nzala ng'hani, nokulamba uning'he ndiya iyo indung'hu.” Lekamana Esau katangigwa Edomu fambulo jake ndung'hu.
31 Yakobo kamwidika, “Nizakwing'ha one uhanichuuzila haki ya uchaudele wako.”
32 Esau kamulongela, “Vinoga! Nahabehi kudanganika. Haki yonifaya choni?”

33 Yakobo kamwidika, “Teng'hu ilahile kuwa
kwizanichuluzila haki yako.”

Esau kailaha na kamwing'ha Yakobo haki yake.
34 Maabaho Yakobo kamwing'ha gate na nzugu.
Kaja na kang'wa na maabaho kenuka na kasegela.
Ivo niivo Esau viyaizehile haki yake ya uchaudele.

# 26

*Isaka kokala Gelali*

1 Maabaho kulawilila nzala muna iisi, nzala iyo
haikalile ija yoikalile lusita lwa Bulahimu. Isaka
kahita kwa Abimeleki mfalume wa Wafilisiti, uko
Gelali. 2 Mndewa Mulungu kamulawilila Isaka
na kamulongela, “Sekeuhite Misili, mbali kala
muna iisi iyo mbaka vondanikulongele. 3 Kala
hano, na niye nizakuwa na weye na nizakutemela
mate. Nizakwing'ha zisi zino zose kuwa zako na
welesi wako. Nizakwika goya chilagano choni-
ilahile na tati yako Bulahimu. 4 Nizakwing'ha
welesi mwingi fana viya nhondo zili kuulanga
na kuweng'ha zisi zino zose. Kufosela welesi
wako wanhu wa makabila yose wezatemeligwa
mate. 5 Nizakutemela mate kwaviya Bulahimu
kanitegeleza na kamha malagilizo yangu na ndag-
ilizi zangu.”

6 Ivo Isaka kakala uko Gelali. 7 Wanhu wa uko vi-
wamuuzile mbuli za muke wake, Isaka kawedika
kuwa iyo ni lumbu jake. Kwaviya kadumba ku-
longa iyo ni muke wake mana kadumba wanhu
wa uko sekewamkome kwa ichimu cha Lebeka,
yoyakalile lumondo. 8 Isaka viyakalile uko kwa

lusita lutali, Abimeleki mfalume wa Wafilisiti ka-
sungulila muna dizonzo na kamuwona Isaka ka-
muhagatila Lebeka. [9] Abimeleki katuma usenga
kwa Isaka na kalonga, “Humbe iyo ni muke wako!
Habali kulonga ni lumbu jako?”

Isaka kedika, “Nigesa one nilongile kuwa ni
muke wangu, nihakomigwe.”

[10] Abimeleki kalonga, “Kuchitendela choni?”
“Imwe wa wanhu wangu one yambandame
muke wako, weye uhachitendile chihasanye.”
[11] Abimeleki kawazuma wanhu wose, “Munhu
yoyose yondayamdalise munhu ino hebu muke
wake kolondeka yakomigwe.”

[12] Isaka kahanda mbeyu muna iisi ija, na
mwaka uwo kagobola ng'hani kwaviya Mndewa
Mulungu kamtemela mate. [13] Isaka kawa tajili
na utajili wake ugendelela kongezeka mbaka
kawa tajili ng'hani. [14] Isaka kawa na mabum-
bila ya ng'hondolo na ng'ombe na wasang'hani
wengi mbaka Wafilisiti wamuwonela migongo.
[15] Wafilisiti wazisiliza nzasa zose zozihimbigwe
na wasang'hani wa Bulahimu tati yake, lusita Bu-
lahimu viyakalile yang'hali mgima.

[16] Abimeleki kamulongela Isaka, “Segela muna
iisi yetu, mana weye kuna nguvu ng'hani kufosa
cheye.” [17] Ivo Isaka kasegela uko na kazenga
lago jake muna dizanda da Gelali, na kakala
uko. [18] Isaka kahimba kaidi masima yaja yahim-
bigwe na Bulahimu tati yake viyakalile mgima.
Masima yaja yasilizigwa na Wafilisiti lusita Bu-
lahimu viyadanganike. Isaka kayagolela mazina
yaja yaja yoyayatangile tati yake.

19 Wasang'hani wa Isaka wahimba chisima
muna dizanda na wafika sima da mazi ya ugima.
20 Wadimi wa kuja Gelali wagomba na wadimi
wa Isaka na walonga, “Mazi yano yetu.” Ivo
Isaka kachitanga chisima icho “Eseki,” fambulo
jake “Ndwagi” 21 Wasang'hani wa Isaka wahimba
chisima chimwenga, icho nacho wachigombela,
ivo Isaka kachitanga chisima icho “Sitina,” fam-
bulo jake “Kulema”. 22 Maabaho kasegela hanhu
baho na kahimba chisima chimwenga. Baho ha-
hakalile na ndwagi, ivo kachitanga zina “Leho-
bosi”. Kalonga, “Lelo Mndewa Mulungu kach-
ing'ha ulegeho wa kukala muna isi, na chizakala
hano na kongezeka.”

23 Isaka kasegela na kahita Belisheba. 24 Chilo
icho Mndewa Mulungu kamulawila na kamulon-
gela, “Niye ni Mulungu wa tati yako Bulahimu.
Nahamwe na weye, sekeudumbe. Nizakutemela
mate na kukongeza welesi mwingi kwa ichimu
cha msang'hani wangu Bulahimu.” 25 Isaka
kazenga lupango uko na kamtambikila Mndewa
Mulungu. Uko kasimika hema na wasang'hani
wake wahimba sima uko.

### *Isaka na Abimeleki woilumba*

26 Abimeleki keza kulawa Gelali hamwe na
Ahuzati, mbwiyake ng'hani, na Fikoli mkulu wa
wakalizi wake, kumulola Isaka. 27 Ivo Isaka
kawauza, “Habali mwiza kumwangu kunilola, na
kuno munihila na muniwinga muna iisi yenu?”

28 Wawo wamwidika, “Lelo chovimanya Mn-
dewa Mulungu kahamwe na weye. Ivo chi-
itogolela yofaya chiilahile na kutenda lagano

na weye, 29 kuwa weye hwizachilumiza na ch-
eye iviya hachizakulumiza weye. Chikutendela
yanogile na chikuleka usegele kwa tindiwalo na
sambi weye kutemeligwa mate na Mndewa Mu-
lungu.” 30 Isaka kawasasalila ndiya ya dugila,
nawo waja na wang'wa. 31 Igolo yake imitondo
ng'hani, chila munhu keka lagano jake kwa kwi-
ilaha. Maabaho Isaka kawalaga mbwiya zake na
waileka kwa tindiwalo.
32 Siku ija wasang'hani wa Isaka wamwizila
na wamulongela mbuli ya chisima chowachihim-
bile. Wamulongela, “Chiyafika mazi.” 33 Isaka ka-
chitanga chisima icho “Siba,” fambulo jake “Chi-
laho.” Ivo bululu ijo dotangigwa Belisheba mbaka
diyelo.

*Waanake wa Esau*

34 Esau viyawile na miyaka malongo mane, ka-
sola wanaake waidi Wahiti, Yudisi mwana wa
Beeli na Basemati mwana wa Eloni. 35 Wanaake
wawo wawatenda Isaka na Lebeka wakale kwa
usungu.

# 27

*Isaka komtemela mate Yakobo*

1 Isaka viyakalile mulala meso yake yawa hay-
alola bule. Ivo kamtanga Esau mwanage chaudele
na kamulongela, “Mwanangu!”

Nayo kamwidika, “Aino hano.”

2 Isaka kalonga, “Lola niye namulala, na siku
yangu ya kudanganika siimanyile bule. 3 Sola
msale na upinde wako na uhite kumbago na
ukanisakile mnyama wa mwiimbago kwa ichimu
changu. 4 Nyambikile ndiya inogile ija yoniilonda,

na unigalile. Nahamala kuja, niye mwenyewo
nizakutemelela mate ning'hali sinadanganika.”
5 Humbe Isaka viyakalile kolonga na Esau,
Lebeka kakala yotegeleza. Ivo Esau viyahi-
tile kusaka kwiimbago, 6 Lebeka kamulongela
Yakobo, “Nimuhulika tati yako viyamulongele
sekulu wako Esau, 7 ‘Nigalile mnyama na unyam-
bikile ndiya inogile. Nahakomeleza kuja niza-
kutemela mate haulongozi wa Mndewa Mulungu
ning'hali sinadanganika.’ ” 8 Lebeka kagen-
delela kulonga, “Lelo mwanangu, nitegeleze na
utende chinikulongela. 9 Hita kuna dibumbila
da iwaluti unigalile wanaluti waidi wanogile mu-
ladi nimwambikile tati yako ndiya inogile yoy-
ailondaga ng'hani. 10 Na kwizamgalila tati yako
yaje muladi yakutemele mate yang'hali hanadan-
ganika.”
11 Mbali Yakobo kamulongela Lebeka mami
yake, “Kuvimanya kuwa sekulu wangu Esau
ni munhu mwene upipi, mbali niye nabule.
12 Yodahika tati yangu kezalonda kunibabasa, na
niye nizawoneka fana viya nomvwizila, kwa ivo
nizaigalila duwilo badala ya kutemeligwa mate.”
13 Mami yake kamulongela, “Duwilo jako
dimhate niye, mbali weye mwanangu tenda
fana viya vinikulagiliza, na hita ukanigalile
wanaluti.” 14 Ivo Yakobo kahita na kawasola
iwanaluti waidi na kamgalila mami yake, nayo
kasasala ndiya inogile yoyailondile tati yake.
15 Maabaho Lebeka kalava viwalo vinogile va
Esau mwanage imkulu, voyavikile muna ikaye,
na kamuyawaliza Yakobo mwanage imdodo.
16 Iviya kamuyawaliza mbende za iwanaluti waja

mmakono na muna ulukuli lutelebuke ulibule
upipi muna isingo yake. 17 Lebeka kamwing'ha
Yakobo indiya inogile, hamwe na diya digate
doyadisasale.

18 Maabaho Yakobo kahita kwa tati yake na
kamtanga, “Tata!”

Nayo kedika, “Aino.” Tati yake kamuuza, “Weye
mwanangu yelihi?”

19 Yakobo kamwidika, “Niye Esau chaudele
wako. Nisang'hana fana viunilagilize. Nolamba
tata ukale uje nyama yonikugalile, muladi udahe
kunitemela mate.”
20 Isaka kamuuza, “Mwanangu iwaze kupata
himahima fanile ivo?”

Yakobo kamwidika, “Mndewa Mulungu, Mulungu wako kanitaza kupata ivo.”

21 Isaka kamulongela Yakobo, “Mwanangu
kwenhuka haguhi nidahe kukubabasa muladi
nivimanye fana kweli weye kwa Esau mwanangu
hebu siyo.” 22 Yakobo kamkwenhukila tati
yake, nayo kambabasa na kalonga, “Dizi
jako dohulikika fana viya dizi da Yakobo,
mbali makono yalinga fana makono ya Esau.”
23 Isaka hammanyile Yakobo kwaviya makono
yake yakala na upipi fana Esau. Ivo kakala
kokwandusa kumtemela mate. 24 Mbali kamuuza
kaidi, “Weye kweli mwanangu Esau?”

Yakobo kamwidika, “Iyo niye.”

25 Isaka kalonga, “Nigalile nyama muladi
nije na kukutemela mate.” Yakobo kamgalila
na kaja, nayo iviya kamgalila divai kang'wa.
26 Maabaho Isaka tati yake kamulongela,
“Mwanangu, nikwenhukile uninonele.”

27 Yakobo kamkwenhukila na kamnonela, Isaka
viyahulike mnung'ho wa viwalo vake, kamtemela
mate na kalonga,
"Lola mnung'ho wa mwanangu
ulinga fana mnung'ho wa mgunda woutemeligwe
mate na Mndewa Mulungu.
28 Mulungu yakwing'he mvula kulawa kuulanga
na yakwing'he ulongo unogile ulava nafaka na
divai nyingi.
29 Makabila yose wezakusang'hanila,
na wezakutumbalila mavindi,
kwizakuwa mulangulizi wa wandugu zako wose
na welesi wa mami yako wakutumbalile mavindi,
wanhu wokuduwila weye waduwiligwe na
wokutemela mate wezatemeligwa mate."
30 Isaka viyakomeleze kumtemela mate Yakobo,
lusita Yakobo viyasegele, Esau sekulu wake kab-
wela kulawa kuukala.
31 Iviya Esau kambika
ndiya inogile na kamgalila tati yake. Kamulon-
gela, "Haya tata, kala uje nyama yonikugalile,
muladi udahe kunitemela mate."
32 Isaka kamuuza, "Weye kwa yelihi?"
Nayo kamwidika, "Niye niiyo Esau mwanago
chaudele."
33 Isaka kagudemeka ng'hani na kalonga,
"Humbe yelihi yoyalawile kuukala na kanigalila
nyama, na niye nija yose nimala ung'hali
hunakwiza? Iviya nimtemela mate nimala, ivo
katemeligwa mate kamala!"
34 Esau viyahulike ivo kalila kwa dizi kulu na
giyogiyo ng'hani na kalonga, "Tata, na niye iviya
nitemele mate!"

35 Mbali Isaka kamwidika, “Mdodo wako
kanizila na kunivwizila. Na kasola kutemeligwa
mate kwako.”
36 Esau kalonga, “Lekamana kotangigwa
Yakobo kwaviya kanivwizila miyanza midi. Mosi kasola haki yangu ya uchaudele, maabaho kasola kutemeligwa mate kwangu.” Esau kalonga, “Hunisigazile kutemeligwa mate kwangu?”
37 Isaka kamwidika Esau, “Nimala kumtenda
Yakobo kuwa mulangulizi wako na nimwing'ha ndugu zake wose kuwa wasang'hani wake. Nimpatila nafaka na divai. Lelo nikutendele choni weye mwanagu?”
38 Esau kamulongela tati yake, “Kodaha
kutemela mate mwanza umwe muhala tati yangu? Tati yangu na niye iviya nhemele mate!” Kandusa kulandula dizi na kalila.
39 Maabaho Isaka tati yake kamwidika,

“Kwizakala kutali na mgunda unogile ulava nafaka na divai nyingi
na kutali na mvula ya kuulanga.
40 Kwizakala kwa kuwakoma wanhu kwa sengo,
Kwizamsang'hanila ndugu yako.
Mbali uhalema,
kwizatenda voulonda mwenyewo.”

41 Esau kamwihila Yakobo kwa ichimu cha
kutemeligwa mate koyatemeligwe na tati yake. Kagesa, “Siku za matanga ya tata zaabehi, zihamala nizamkoma mdodo wangu Yakobo.”
42 Mbali Lebeka viyavimanyile chiyailungile
Esau, kamtumila usenga kumtanga Yakobo na kalonga, “Wiiteganye, sekulu wako Esau koiguma
moyo kwa kulonda kukukoma. 43 Lelo mwanangu

tegeleza chonikulongela na uchitende. Hima kim-
bilila kwa lumbu jangu Labani uko Halani, 44 kala
nayo kwa lusita, mbaka ludoko lwa sekulu wako
luhunguke. 45 Ludoko lwa sekulu wako von-
daluhunguke na vondayazimize youmtendele,
nizamtuma munhu yakubweleze. Habali nidan-
ganikiligwe na mweye wose waidi siku dimwe?"

### *Isaka komtuma Yakobo kwa Labani*

46 Lebeka kamulongela Isaka, "Niye
ndegezigwa na wanaake wano Wahiti wa Esau.
One Yakobo iviya yahasola muke kulawa mwa
wanaake wano Wahiti, muhavu nidanganike."

# 28

1 Isaka kamtanga Yakobo, kamtemela mate
na kamulongela, "Sekeusole mwanamke yoyose
Mkanaani. 2 Hita kuna iisi ya Padani Alamu,
muna ikaye ya wasaho yako Besueli, na uka-
sole imwe wa wana wa mtumba wako Labani.
3 Mulungu mwene Udaho yaitemele mate sola
yako na yakwing'he wana wengi, ivo kwizakuwa
tata wa makabila mengi. 4 Yakutemele mate
weye na welesi wako fana viya viyamtemele mate
Bulahimu muladi udahe kuhazi isi ino youkala
fana nyambenyambe, Mulungu yoyamwing'hile
Bulahimu!" 5 Isaka kamtuma Yakobo yahite kwi-
isi ya Padani Alamu kwa Labani, yoyelekigwe na
Besueli, Mwalamu, Labani lumbu jake Lebeka
yeli mami yawo Yakobo na Esau.

### *Esau kosola muke weketatu*

6 Esau kavimanya kuwa Isaka kamala
kumtemela mate Yakobo na kumtuma yahite

Padani Alamu yakasole muke. Iviya kavimanya
kuwa Isaka viyamtemele mate, kamulongela
sekeyasole muke Mkanaani. 7 Kavimanya kuwa
Yakobo kawategeleza tati yake na mami yake na
kahita Padani Alamu. 8 Esau kavimanya kuwa
Isaka tati yake hanogeligwa bule na wanaake
wa Kanaani. 9 Esau kahita kwa Ishumaili
mwana wa Bulahimu na kamsola muke imwenga
yotangigwa Mahalati, lumbu jake Nebayoti.

### *Nzozi ya Yakobo uko Beteli*

10 Yakobo kasegela Belisheba na kuhita Ha-
lani. 11 Kafika hanhu hamwe ha kugona chilo
chimwe kwaviya zuwa dikala diswa. Kasola
dibwe dimwe da hanhu baho kadika hasi ya iditwi
jake, kagona. 12 Kalota kuwa kawona vidando
vimizigwa kulawa muna iisi mbaka kuulanga,
wasenga wa kuulanga wokwela na kuhumuluka
hasi kwa ividando ivo. 13 Mndewa Mulungu kema
habehi nayo kamulongela, "Niye niiyo Mndewa
Mulungu, Mulungu wa tati yako Bulahimu na
Isaka," kalonga, "Nizakwing'ha weye na welesi
wako isi ino yuwiigonela. 14 Welesi wako wiza-
kuwa mwingi fana msanga wa isi. Wezakwenela
chila hanhu, ulawilo wa zuwa na uswelo wa
zuwa, kasikazi na kusi. Kufosela weye na welesi
wako wanhu wose wezatemeligwa mate. 15 Niye
nahamwe na weye na kukukaliza hohose houhita,
na nizakubweleza muna iisi ino. Sizakuleka
mbaka vondanikutendele yose yonikulaganile."

16 Yakobo kalamka na kalonga, "Kweli Mndewa
Mulungu ka hanhu hano, niye sivimanyile bule!"

17 Nayo kadumba na kalonga, “Hanhu hano ho-
dumbiza ng'hani! Kweli ni kaye ya Mulungu na
lwivi lwa kuulanga.”
18 Igolo yake imitondo ng'hani Yakobo kala-
muka, kasola idibwe dodikalile hasi ya ditwi
jake, kadisimika fana mhanda ya ukumbuso na
kudigidila mavuta. 19 Kahatanga hanhu baho
Beseli. Umwaka bululu ijo ditangigwa Luzu.
20 Maabaho Yakobo kailaha kwa Mndewa Mu-
lungu, “One wahawa hamwe na niye, na ku-
nikaliza muna umwanza wangu na kuning'ha
ndiya na viwalo, 21 na one nahabwela vinogile
kuna ikaye ya tati yangu, ivo Mndewa Mulungu
kwizakuwa Mulungu wangu. 22 Dibwe dino doni-
disimike hano fana mhanda ya ukumbuso, diza-
kuwa kaye ya Mulungu, na niye nizakwing'ha
chinhu chimwe muna ichila vinhu longo von-
dauning'he.”

# 29

### *Yakobo kofika kuna ikaye ya Labani*

1 Yakobo kagendelela na mwanza wake na
kafika muna iisi ya ulawilo wa zuwa. 2 Kalola
na kawona chisima mwiichuwala na mumgwazo
yake mabumbila matatu ya ng'hondolo wagona.
Ng'hondolo wakala wong'wizigwa muna
ichisima icho chochigubikigwe na dibwe kulu.
3 Mabumbila yose ya ng'hondolo yahaiduganya,
wadimaji wobimbilisa idibwe ijo kwa hamwe
kulawa hana ichisima na kuwang'wiza
iwang'hondolo. Maabaho wogubika kaidi
ichisima kwa dibwe ijo.

4 Yakobo kawauza waja iwadimi, “Wambwiya
zangu, mweye mulawa kulihi?”

Wamwidika, “Cholawa Halani.” 5 Kawauza
kaidi, “Vino mummanya Labani mwana wa Na-
holi?”

Wamwidika, “Ona chimmanya.” 6 Yakobo ka-
gendelela kuwauza, “Vino mgima?”

Nawo wamwidika, “Mgima! Lola mndele wake
Laheli iyo ija kokwiza na ng'hondolo zake.”

7 Yakobo kalonga, “Nowona ing'hali misi na siyo
lusita lwa kuwaduganya ng'hondolo hamwe, ivo
wang'wizeni mazi muhite mukawadime.”

8 Nawo wamwidika, “Hachidaha bule mbaka
ng'hondolo wose wawe hano, na dibwe dibimbil-
iswe mwiichisima, maabaho chowang'wiza mazi
ng'hondolo.”

9 Yakobo viyakalile yang'hali kolonga nawo,
Laheli yakalile mdimi wa ng'hondolo, kafika na
ng'hondolo wa tati yake. 10 Yakobo viyamu-
wone Laheli mndele wa mtumba wake Labani
hamwe na zing'hondolo, kahita hana disima na
kudibimbilisa idibwe kulawa hana disima na
kuwang'wiza mazi iwang'hondolo wa mtumba
wake. 11 Maabaho Yakobo kamnonela Laheli
na kandusa kulila kwaviya kakala na deng'ho.
12 Yakobo kamulongela Laheli, “Niye ni ndugu wa
tati yako, na mwana wa Lebeka.”

Maabaho Laheli kakimbila kumulongela tati
yake. 13 Labani viyahulike mbuli ya Yakobo mwi-
hwage, kahita yokimbila kumuhowela, viyamfik-
ile kamuhagatila na kamnonela na kamkalibisha
ukaye yake. Yakobo kamulongela mbuli zose zozi-
lawilile. 14 Labani kalonga, “Ivo weye ni lukuli

lumwe na damu imwe na niye." Yakobo kakala na
Labani mwezi umwe.

### *Yakobo kowasola Laheli na Leya*

15 Labani kamulongela Yakobo, "Weye kwa
ndugu yangu hudaha kunisang'hanila bila
kukuliha. Lelo nikulihe hela nyingahi?" 16 Labani
kakala na wandele waidi, imkulu zina jake Leya
na imdodo Laheli. 17 Leya kakalayanogile, mbali
Laheli kakala lumondo ng'hani.

18 Yakobo kamulonda Laheli, ivo kamulongela
Labani, "Nizakusang'hanila miyaka saba, one
uhanitogolela kumsola Laheli."

19 Labani kamwidika, "Muhavu nikwing'he
weye Laheli sembuse kumwing'ha munhu
imwenga yoyose. Gendelela kukala hano na
niye." 20 Yakobo kamsang'hanila Labani miyaka
saba muladi yampate Laheli, mbali kumwake
miyaka saba ni fana viya siku ndodo, kwaviya
kamulonda Laheli.

21 Maabaho Yakobo kamulongela Labani,
"Lusita lwangu lufika, ning'he muke wangu."
22 Ivo Labani kasasala dugila na kawagoneka
wanhu wose wa hanhu haja. 23 Mbali viifikile
ichigulogulo, Labani kamulava Leya mwanage
imkulu na kumgala kwa Yakobo, nayo Yakobo
kagona nayo. 24 Labani kamwing'ha Zilipa
mtumwa wake wa chike yawe mtumwa wa Leya
mwanage. 25 Igolo yake imitondo, Yakobo katola
kuwa ni Leya. Kamgendela Labani na kamuuza,
"Choni chino chounhendele? Nikusang'hanila
muladi nimpate Laheli. Habali kunivwizila?"

26 Labani kamwidika, “Chino siyo chihendo
chetu kusoligwa imndele imdodo kuno imkulu
yang'ali hanasoligwa. 27 Gozela mbaka siku saba
za dugila, maabaho nizakwing'ha Laheli kwa us-
ang'hano wa miyaka saba imwenga.”

28 Yakobo katogola, viifikile juma da dugila,
Labani kamwing'ha Laheli mwanage yawe muke
wake. 29 Labani kamulava Biliha mtumwa wake
wa chike, yawe mtumwa wa Laheli. 30 Yakobo
kagona na Laheli iviya, na Yakobo kamulonda
kufosa Leya. Maabaho Yakobo kamsang'hanila
Labani miyaka saba imwenga.

### *Wana wa Yakobo*

31 Mndewa Mulungu kawona kuwa Leya
halondigwa goya, ivo kamtenda yeleke, mbali
Laheli heleke bule. 32 Leya kapata wimo na
kaibasula mwana wa chilume na kamtanga zina
jake Lubeni kwa viya kalonga, 'Mwana aino'. Leya
kalonga, “Mndewa Mulungu kawona manhesa
yangu na lelo mulume wangu kezanilonda.”
33 Maabaho kapata wimo kaidi na kaibasula
mwana imwenga wa chilume. Kalonga, “Mndewa
Mulungu kahulika kuwa nokwihilwa.” Ivo Leya
kamtanga zina jake Simeoni. 34 Leya kapata
wimo kaidi na kaibasula mwana imwenga wa
chilume, nayo kamtanga zina jake Lawi. Leya
kalonga, “Lelo mulume wangu kezailumba
vinogile na niye, kwaviya nimwelekela wana
wa chilume watatu.” 35 Maabaho kapata wimo
kaidi na kaibasula mwana imwenga wa chilume
na kalonga, “Lusita luno nizamtogoza Mndewa

Mulungu." Kamtanga zina jake Yuda, maabaho
Leya kaleka kweleka.

# 30

1 Mbali Laheli hamwelekele Yakobo wana
wowose, na ivo kamuwonela migongo mwali
wake na kamulongela Yakobo, "Ning'he wana,
buleivo nizadanganika." 2 Yakobo kamuwonela
ludoko Laheli na kalonga, "Sidaha kusola hanhu
ha Mulungu. Yeye muhala niiyo yakukimilile
weye sekeupate wana."
3 Laheli kamulongela, "Ino hano mtumwa
wangu Biliha, ibandame nayo muladi yapate
wana kwa ichimu changu. Ivo nizakuwa
mama kufosela yeye." 4 Laheli kamwing'ha
mulumake Yakobo mtumwa wake Biliha yawe
fana muke wake, nayo Yakobo kambandama.
5 Biliha kapata wimo na kamwelekela Yakobo
mwana wa chilume. 6 Laheli kalonga, "Mulungu
kanigombela, kauhulika usungu wangu na
kuning'ha mwana wa chilume." Ivo Laheli
kamtanga zina jake Dani. 7 Biliha mtumwa wake
wa chike kapata wimo kaidi na kamwelekela
Yakobo mwana imwenga wa chilume. 8 Laheli
kalonga, "Nikala na ugomvi mkulu na mwali
wangu, mbali nihuma." Ivo kamtanga mwana
iyo Nafutali.
9 Leya viyawonile kuwa kaleka kulela, kamsola
Zilipa mtumwa wake wa chike na kamwing'ha
Yakobo yawe fana muke wake. 10 Maabaho
Zilipa kamwelekela Yakobo mwana wa chilume.
11 Leya kalonga, "Nipata sudi," ivo kamtanga
zina jake Gadi. 12 Zilipa mtumwa wake wa

Leya kamwelekela Yakobo mwana imwenga wa
chilume, 13 Leya kalonga, “Nodeng'helela! Lelo
wanaake wezalonga kuwa kanadeng'ho” Kam-
tanga zina jake Asheli.
14 Lusita lwa kuhuna ngano, Lubeni kahita
kuchuwala, uko kapata makalanga* na kam-
galila Leya mami yake. Laheli kamulongela
Leya, “Nopula uning'he makalanga yamwenga ya
mwanago.”
15 Leya kamwidika, “Vino kogesa mbuli ndodo
kunihoka mulumangu? Lelo kolonda kusola
makalanga ya mwanangu.”

Laheli kalonga, “One wahaning'ha makalanga
ya mwanago, Yakobo kezagona kumwako chilo
cha diyelo.”
16 Ichigulogulo Yakobo viyakalile kobwela ku-
lawa kuchuwala, Leya kahita kumuhokela na
kamulongela, “Chilo cha diyelo uhite kugona
kumwangu kwaviya nikwing'ha makalanga ya
mwanangu.” Ivo chilo icho kagona nayo.
17 Mulungu kahulika nhosa ya Leya, na kapata
wimo na kamwelekela Yakobo mwana wetano
wa chilume. 18 Leya kalonga, “Mulungu kan-
ing'ha yombe jangu, kwaviya nimwing'ha mu-
lume wangu msang'hani wangu wa chike”; Ivo
kamtanga zina jake Isakali. 19 Leya kapata wimo
kaidi na kamwelekela Yakobo mwana wa sita
wa chilume. 20 Leya kalonga, “Mulungu kan-
ing'ha chitumetume chinogile. Lelo mulumangu
kezanitogola, kwaviya nimwelekela wana sita wa
chilume.” Ivo kamtanga zina jake Zabuloni.

* **30:14** Wahuwila kuwa mwanamke yahaja makalanga kezalela ng'hani.

21 Hamwande Leya kapata mwana wa chike, na
kamtanga zina jake Dina.
22 Maabaho Mulungu kamkumbuka Laheli na
kahulika chiyapulile, ivo kamtenda yadahe ku-
pata wana. 23 Laheli kapata wimo na kaiba-
sula mwana wa chilume na kalonga, "Mulungu
kanisegezela chinyala changu." 24 Kamtanga
zina jake Yosefu, kalonga, "Mndewa Mulungu un-
ing'he mwana imwenga."

### *Yakobo woitogolela na Labani*

25 Laheli viyamweleka Yosefu, Yakobo
kamulongela Labani, "Unileke nibwele ukaye
yangu. 26 Uning'he wake zangu na wanangu
woniwapatile kwa ichimu cha usang'hano
wonikusang'hanile, nisegele nawo, kwaviya
kuvimanya nikusang'hanila vinogile."
27 Labani kamulongela Yakobo, "Leka na niye
nilonge. Niifunza kwa usawi wangu kuwa Mn-
dewa Mulungu kanitemela mate kwa ichimu
chako. 28 Longa yombe jako na niye nizakuliha."
29 Yakobo kedika, "Weye mwenyewo
kuvimanya viya vinikusang'hanile, kuvimanya
viniwekile goya wanyama wako. 30 Kwaviya
vinizile kukala na vinhu vidodo, mbali kusongela
nifike vinhu vako vongezeka ng'hani na
Mndewa Mulungu kakutemela mate chila hanhu
honihitile. Mbali lelo kaye yangu nizailola goya
zuwaki?"
31 Labani kamuuza, "Nikulihe choni?"
Yakobo kamwidika, "Silonda yombe jojose.
One chihaitogolela, nizagendelela kwika goya
wanyama wako. 32 Nilekele nifose hagati

ya wanyama wako wose diyelo nigole muna dibumbila chila mnyama yeli na uzegenha na uzolizoli, chila mnyama mtitu na luti weli na uzegenha na uzolizoli. Ijo niijo yombe donilonda.
33 Siku zikwiza, kwaminika kwangu kwizawoneka funhulafunhula vondawize kulola yombe jangu. One yahawoneka luti yoyose yelibule uzegenha hebu uzolizoli, hebu ng'hondolo yoyose heli na utitu muna dibumbila jangu, iyo kezakuwa kabawigwa."

34 Labani kedika, "Vinoga. Chizatenda fana viulongile."
35 Mbali siku iyo Labani kahita kayagola mabebelu yose yeli na mindilizi na uzegenha na luti wose mizike wowakalile na uzolizoli na uzegenha, chila luti wowakalile na uzelu muna ulukuli na chila ng'hondolo yeli na utitu, kaweka hasi ya ulolezi wa wanage,
36 Maabaho Bumbila da Labani dikala kutali na bumbila da Yakobo kwa siku nhatu. Yakobo kadilolesa bumbila da wanyama wa Labani dodisigale.

37 Yakobo kasola mango mbisi za mibiki mitatu mbasakanyo, kazigomola yamagome muladi mindilizi mizelu iwoneke muna zimango izo.
38 Maabaho kazisimika zimango izo haulongozi wa iwanyama hana zimbaluti za kung'wila mazi iwanyama. Ivo wanyama wezile kung'wa mazi wapata wimo uko.
39 Wapata wimo haulongozi wa mango izo, weleka wanyama weli na mindilizi hebu uzolizoli hebu uzegenha.

40 Yakobo kawagola wanang'hondolo wawo, maabaho kawalagusila kuna iwanyama weli na uzolizoli na mindilizi na weli na utitu muna dibumbila da Labani. Kwa ichimu icho Yakobo

kapata bumbila jake mwenyewo hadihanganye
na diya da Labani.

41 Wanyama wanenehe viwatizile, Yakobo keka
zimango haulongozi hawo hana zimbaluti za
kung'wizila mazi muladi wapate wimo habehi
na mango izo. 42 Mbali Yakobo hekile zimango
izo haulongozi wa wanyama wasokile viwap-
atile wimo. Ivo wanyama wasokile wawa wa
Labani na wanenehe wawa wa Yakobo. 43 Ivo
Yakobo kawa tajili ng'hani na kawa na mabum-
bila makulu ya wanyama na wasang'hani wa
chilume na wa chike na ngamiya na vihongwe.

# 31

*Yakobo komkimbila Labani*

1 Yakobo kawahulika wanage Labani wolonga,
“Yakobo kasola chila chinhu cha tati yetu. Uta-
jili wake wose ulawa kwa tati yetu.” 2 Yakobo
kavimanya kuwa Labani hamgesile fana baho
haumwaka. 3 Maabaho Mndewa Mulungu kamu-
longela Yakobo, “Bwela kuna iisi ya wasaho zako
na kwa ndugu zako. Na niye nizakuwa hamwe na
weye.”

4 Yakobo katuma wanhu wakawatange La-
heli na Leya kwiichuwala koyakalile kowadima
iwang'hondolo wake. 5 Yakobo kawalongela,
“Nowona kuwa tati yenu hanigesa fana umwaka,
mbali Mulungu wa tati yangu kahamwe na niye.
6 Muvimanya kuwa nimsang'hanila tati yenu kwa
nguvu zangu zose. 7 Hata ivo kanivwizila na
kasakanya yombe jangu miyanza longo. Mbali
Mulungu hamulekele yanilumize. 8 Haja tati yenu

viyalongile, 'Wanyama wose weli na mawolama-
wola wezakuwa yombe jako,' ivo bumbila jose
dilela wanyama weli na mawolamawola. Na haja
viyalongile, 'Wanyama wose weli na uzolizoli
wezakuwa yombe jako,' ivo bumbila jose dilela
wanyama weli na uzolizoli. 9 Mulungu viyasolile
wanyama wa tati yenu kaning'ha niye.
10 "Lusita lwa wanyama kupata wimo vilufikile
nilota nzozi, na niwona mabebelu yose yoyak-
welile mazike yakala na mindilizi na mawolama-
wola na uzolizoli. 11 Msenga wa kuulanga kalonga
na niye muna zinzozi na kanitanga, 'Yakobo,'
nimwidika, 'Aino.' 12 Na kalonga, 'Inula meso
yako na ulole mabebelu yose yeli na miliya na ma-
wolamawola. Mbuli iyo iwa ivo kwaviya niwona
viyakutendile Labani. 13 Niye ni Mulungu yoyaku-
lawilile kuja Beseli, hanhu haja houitilile mavuta
imhanda ya ukumbuso, na weye kunilahila. Lelo
isasale na ubwele muna iisi yako yowelekigwe.' "
14 Laheli na Leya wamwidika Yakobo, "Ch-
eye chabule kaidi hanhu ha vinhu hebu uhazi
wowose muna ikaye ya tati yetu. 15 Tati yetu
kachitenda fana nyambenyambe. Kachichuuza,
na lelo kasang'hanila hela zose zoyalihigwe kwa
ichimu chetu. 16 Utajili uno wose Mulungu woy-
ausolile kulawa kwa tati yetu ni wetu cheye na
wanetu. Tenda vovose viyakulongele Mulungu."
17 Yakobo kalamka na kaisasala kusegela
kwa kuwakweza wanage na wake zake muna
ingamiya, 18 Kasola wanyama wake wose
na vinhu vake vose viyavipatile kuja Padani
Alamu, kandusa mwanza kubwela kuna iisi
ya Kanaani kwa Isaka tati yake. 19 Labani

viyahitile kuwakanha mazoya ng'hondolo wake,
Laheli kabawa nyang'hiti za milungu ya tati
yake. 20 Yakobo kamvwizila Labani Mwalamu,
hamulongele bule kuwa kosegela. 21 Kasola chila
chinhu chake na kasegela chahimahima. Kaloka
ulwanda lwa Efulati na kahita kuna mulima wa
isi ya Gileadi.

### *Labani komsondelela Yakobo*

22 Siku nhatu hamwande Labani kalongiligwa
kuwa Yakobo kakimbila. 23 Labani kawasola
ndugu zake, kamsondelela Yakobo kwa siku
saba. Kamfika kuna mulima wa isi ya Gileadi.
24 Muna zinzozi ichilo Mulungu kamwizila Labani
Mwalamu na kamulongela, “Uiteganye, seke
umtemele mate Yakobo hebu sekeumduwile.”
25 Labani kamfika Yakobo lusita ulo Yakobo
viyekile lago jake kumulima, Labani na ndugu
zake weka lago jawo muna iisi ya mulima wa
Gileadi.

26 Labani kamulongela Yakobo, “Habali
kutenda vino, habali kunivwizila na kuwasola
wandele wangu fana mateka kuna ing'hondo?
27 Habali kunivwizila na kunikimbila? One
uhanilongele, nahadahile kukulaga kwa deng'ho
na nyila na ngoma na vilongelonge. 28 Habali
huning'hile nyafasi ya kuwanonela wanangu na
wazukulu zangu? Yayo youtendile ya chibozi!
29 Ninawo udahi wa kukulumiza, mbali chilo
chifosile Mulungu wa tati yako kanizuma
kalonga, ‘Seke umtemele mate Yakobo hebu
sekeumduwile.’ 30 Novimanya kukimbila
kwaviya kukala na hamu ng'hulu ya kubwela

ukaye kwa tati yako. Mbali habali kubawa
nyang'hiti za milungu yangu?”
31 Yakobo kamwidika Labani, “Nidumba
kwaviya nigesa uhanihokile wandele wako.
32 Mbali one munhu yoyose uhamfika na
nyang'hiti za milungu yako, umkome. Zahila
haulongozi ha wanhu wetu, one uhawona chinhu
chako uchisole.” Yakobo havimanyile bule fana
Laheli kabawa nyang'hiti za milungu ya Labani.
33 Ivo Labani kahita na kazahila nyang'hiti izo
muna dihema da Yakobo, maabaho kengila hema
da Leya na hema da wasang'hani waja waidi wa
chike, mbali hawonile bule nyang'hiti za milungu
yake. Maabaho kengila muna dihema da Laheli.
34 Laheli kakala yasolile nyang'hiti izo za milungu
na kazifisa hasi ya chigoda cha kukalila uchanyha
ya ngamiya, na kakala mchanyha yake. Mbali
Labani kazahila muna dihema jose, mbali hazi-
patile bule. 35 Laheli kamulongela tati yake, “Tata,
sekeuniwonele ludoko, mbali sizakwinuka bule
haulongozi wako kwaviya namzisiku zangu.” La-
bani kazizahila nyang'hiti za milungu yake, mbali
hazipatile bule.
36 Maabaho Yakobo kehilwa na kagomba na
Labani, kalonga “Nihasanya choni mbaka unison-
delele vino? 37 Vino kupekula vinhu vangu vose,
chinhu chako chilihi chouchipatile kumwangu?
Chike haulongozi wa ndugu zako na ndugu zangu
wadahe kulola muladi wadahe kulamula fana
imwe wetu kagolosa. 38 Nikala na weye miyaka
malongo maidi, ng'hondolo wako hebu luti wako
hawatengule wimo, na sidile mabebelu kulawa
muna dibumbila jako. 39 Niye hata mwanza

umwe sikugalile mnyama wako yoyakomigwe na
mnyama wa kumbago, mbali niliha ubananzi
uwo niye mwenyewo. Weye kunilonda nilihe
bila kugesa fana kabawigwa imisi hebu ichilo.
40 Imisi nifunyila umoyo zuwa na ichilo nifuny-
ila umoyo mbeho, sidahile kupata nhongo hata
chidogo. 41 Miyaka malongo maidi yose nikala
hamwe na weye. Nikusang'hanila miyaka longo
na mine kwa ichimu cha wandele zako waidi
na miyaka sita kwa ichimu cha wanyama wako,
mbali weye kwasakanya yombe jangu miyanza
longo. 42 Mulungu wa tati yangu na Mulungu
wa Bulahimu na Mulungu yoyamtendile Isaka
yamdumbe, one sigambeyawe hamwe na niye,
wahaniwingile mikono muhala. Mbali Mulungu
kayawona manhesa yangu na sang'hano yoni-
itendile, na ichilo chifosile kakubwakila.”

### *Yakobo na Labani woitogolela*

43 Labani kamwidika Yakobo, “Wanaake
wano ni wandele wangu, na wana wawo ni
wanangu, wanyama wano ni wangu. Chila
chinhu chouwona hano ni changu. Mbali niye
nodaha kutendaki diyelo kwa iwano iwandele
wangu na iwana wowaweleke? 44 Izo chitende
lagano niye na weye, iwe ukalangama hagati ya
weye na niye.”

45 Yakobo kasola dibwe kulu na kudisimika
fana mhanda ya ukumbuso. 46 Yakobo
kawalongela ndugu zake waduganye mabwe,
nawo waduganya mabwe na weka chibugulu.
Maabaho waja ndiya habehi na chibugulu chiya
cha mabwe. 47 Labani kachitanga chibugulu icho
Yegasahadusa, mbali Yakobo kachitanga Galedi.

48 Labani kamulongela Yakobo, “Chibugulu chino
cha mabwe chizakuwa ukalangama kwa cheye
waidi.” Kwa ivo lekamana chibugulu icho
chotangigwa Galedi, 49 na iviya hatangigwa
Misipa, mana kalonga, “Mndewa Mulungu
yachikalize weye na niye lusita vichiwa kutali bila
kuiwona.” 50 Labani kagendelela kulonga, “One
uhawagaza wandele zangu, hebu uhasola wake
wamwenga, one ihawa siimanyile mbuli ino,
uvimanye kuwa Mulungu ni mkalangama wetu.”
51 Labani kamulongela Yakobo, “Chibugulu
cha mabwe yano ya luwe na mhanda ya
ukumbuso yoniisimike hagati ya weye na niye
ni ukalangama wa dibwe.” 52 Chibugulu chino
na mhanda ni ukalangama kuwa niye sizafosa
chibugulu chino kwiza kumwako hebu weye
hwizafosa chibugulu chino na mhanda ino kwiza
kumwangu kwa wihi. 53 Mulungu wa Bulahimu
na Mulungu wa Naholi, kezachihumiza niye
na weye. Maabaho Yakobo kailaha kwa zina
da Mulungu yoyamtendile Isaka yamdumbe.
54 Maabaho Yakobo kalava nhambiko ya
kutimbula kuna mulima na kuwagoneka ndugu
zake waje ndiya, viwakomeleze wasigala
uko chilo chose. 55 Imitondo ng'hani Labani
kawanonela wazukulu zake na wanage na
kawatemela mate, maabaho kawalaga, kawaleka
na kabwela ukaye.

# 32

*Yakobo koisasala kwiiting'hana na Esau*

1 Yakobo kahita na mwanza wake, wasenga wa
kuulanga waiting'hana nayo. 2 Yakobo viyawa-
wone kalonga, “Dino ni lago da Mulungu.” Ka-
hatanga hanhu haja Mahanaimu.

3 Yakobo katuma wasenga kumulongolela kwa
sekulu wake Esau uko Seili kuna iisi ya Edomu.
4 Kawalagiliza wakamulongele mwenevale wake
Esau, “Msang'hani wako Yakobo kolonga vino
‘Nikala kuugeni kwa Labani mbaka sambi. 5 Niye
nina ng'ombe na vihongwe na ng'hondolo na luti
na wasang'hani wa chilume na wa chike. Nogala
mbuli yangu kumwako mwenevale muladi nito-
goleke haulongozi wako.’ ”

6 Wasenga viwabwelile kwa Yakobo, walonga,
“Chihita kwa sekulu wako Esau, nayo kamzila
kokwiza kukuhokela. Kokwiza na walume ma-
gana mane.” 7 Yakobo kadumba ng'hani na
kengiligwa na luholozi. Kawagola mabumbila
maidi wanhu wowakalile nayo, iviya ng'hondolo
zake na luti zake na ng'ombe zake na ngamiya
zake. 8 Yakobo kagesa, “One Esau yaheza na
kuditowa bumbila da mwanduso, bumbila don-
dadisigale dizaibanga.”

9 Maabaho Yakobo katosa, “Mulungu wa tati
yangu Bulahimu na Mulungu wa tati yangu
Isaka, nihulike niye! Mndewa Mulungu ku-
nilongela nibwele kuna isi yangu kwa ndugu
zangu, na kezanitendela chila chinhu chinogile
kumwangu. 10 Niye sifaya hata chidogo sang'hano
zako za ulondo wa ufunya umoyo na ubazi wouni-
laguse msang'hani wako. Vinilokile lwanda
lwa Yoludani nikala nabule chinhu ila mhome
muhala, mbali lelo ninayo mabumbila maidi.

11 Nikombole kwa sekulu wangu Esau. Nodumba
kwaviya kezakwiza kuchitowa na kuchinanga ch-
eye chose na wanaake na wana. 12 Kulonga
kuwa kwiza nitendela yanogile na kutenda welesi
wangu uwe mwingi fana msanga wa mwiibahali,
haupeteka bule."

13 Yakobo kagona baho chilo chose,
maabaho kabagula vinhu vake vimwenga viwe
chitumetume kwa Esau sekulu wake, 14 mizike
ya luti magana maidi na mabebelu ya luti
malongo maidi, mizike ya ng'hondolo magana
maidi na mabebelu yang'ondolo malongo maidi,
15 ngamiya wokong'heza malongo matatu hamwe
na madang'ang'a yawo, mang'ombe mazike
malongo mane na malume longo, mhunda
mazike malongo maidi na malume longo,
16 kawagola wasang'hani wake, chila munhu
bumbila jake. Kawalongela, "Longoleni, kuno
muleka nyafasi hagati ya bumbila dimwe
na dimwenga." 17 Kamulagiliza msang'hani
yalongole, "Wahaiting'hana na sekulu wangu
Esau, yahakuuza, 'Weye kwa msang'hani
wa yelihi? Kohitahi? Wanyama kuulongozi
wako wa yelihi?' 18 Kolondeka umwidike,
'Ni wa msang'hani wako Yakobo. Komgalila
chitumetume mwenevale wake Esau. Yakobo
mwenyewo kahachisogo chetu kokwiza.' "
19 Kalagiliza ivoivo kwa msang'hani wa bumbila
dekaidi na deketatu na wamwenga wose kwa
kulonga, "Mwizamulongela Esau mbuli izo izo
vondamwiiting'hane nayo. 20 Iviya mumulongele,
'Msang'hani wako Yakobo kahachisogo chetu
kokwiza.' " Yakobo katenda ivo kagesa,

“Huwenda nizamuhoza kwa vitumetume
ivo vonimulongozela, na hamwande nodaha
kuiwona nayo chihanga kwa chihanga, huwenda
kezanihokela.” 21 Vitumetume va Yakobo vikala
vimulongolela, mbali yeye chilo icho kakala
mudilago.

22 Uko chilo icho Yakobo kalamuka kawasola
wake zake waidi na watumwa zake wa chike
waidi na wanage longo na imwe, na kawalosa
lwanda lwa Yaboki. 23 Viyakomeleze kuwalosa
umwambu, iviya kalosa vinhu vose viyakalile
navo, 24 mbali Yakobo kakala yaidumwe.

Munhu imwe keza na wagomba mbaka imi-
tondo. 25 Munhu iyo viyawonile kuwa hadaha
kumuhuma Yakobo, kamdalisa ichigudi mbaka
kasiguka. 26 Munhu iyo kalonga, “Nileke nihite
kwaviya kokunguzuka.”

Yakobo kamwidika, “Sikuleka bule mbaka
unitemele mate.” 27 Munhu iyo kamuuza, “Zina
jako nani?”

Nayo kamwidika, “Yakobo.”

28 Munhu iyo kamulongela, “Zina jako hadiza-
kuwa Yakobo kaidi. Mbali zina jako dizakuwa
Isilaili, kwaviya kugomba na Mulungu na wanhu,
na kufunya umoyo.”

29 Yakobo kamuuza, “Lelo nilongele zina jako.”

Mbali yeye kamwidika, “Habali kolonda ku-
manya zina jangu?” Maabaho kamtemela mate
Yakobo.

30 Yakobo kalonga, “Nimuwona Mulungu chi-
hanga kwa chihanga na ning'hali mgima.”. Ka-
hatanga hanhu baho Penueli. 31 Yakobo viyafosile

Penueli, zuwa dikala dosomoza, kakala yonjum-
bila kwaviya kasiguka ichigudi. 32 Niivo ili mbaka
diyelo Waisilaili hawaja bule muge wa chigudi,
kwaviya imunhu ija kamdalisa Yakobo hana
umuge wa ichigudi chake viwakalile wogomba.

# 33

## *Yakobo koiting'hana na Esau*

1 Yakobo kayenula meso yake na kamuwona
Esau kokwiza na walume magana mane, ivo
kawagola wanage kwa Leya na Laheli, na
wasang'hani wake wa chike waidi. 2 Kaweka
kuulongozi iwasang'hani wa chike na wanawo,
maabaho Leya na wanage, kuchisogo Laheli
na mwanage Yosefu. 3 Yakobo mwenyewo
kawalongolela kwa kuhita yotumbala mavindi
mbaka chihanga chake chidalisa hasi miyanza
saba mbaka viyafikile habehi na sekulu wake.
4 Mbali Esau kahita yomkimbilila Yakobo, na
kamgeleka isingo na kamnonela, na wose waidi
walila. 5 Esau viyalolile na kuwawona iwanaake
na iwana, kauza, “Wanhu wano wouli nawo
welihi?”

Yakobo kamwidika, “Wano ni wana Mulungu
woyaning'hile msang'hani wake kwa ubazi
wake.” 6 Maabaho waja iwasang'hani na wana
wawo wafika habehi na wainama kwa hishima,
7 iviya Leya na wanage weza na wainama kwa
hishima, maabaho Yosefu na Laheli weza na
wainama kwa hishima.

8 Esau kauza, “Vino habali kuyatuma mabum-
bila yano kumwangu?”

Yakobo kamwidika, “Nilonda nitogoleke na
weye mwenevale wangu.”
9 Mbali Esau kalonga, “Nina vinhu va kufaya
sekulu wangu, vinhu viuli navo usigale navo.”
10 Yakobo kamulongela Esau, “Haidahika bule,
one kutogola kunihokela, nokulamba unihokele
vitumetume vangu. Kweli nodeng'helela
kukuwona weye fana viya niwona chihanga
cha Mulungu, kwaviya viunihokele kwa
unovu. 11 Nolamba utogole vitumetume vino
vonikugalile, kwaviya Mulungu kaninogela na
kanipatila chila chinhu chinili nacho.” Ivo Yakobo
kambembeleza Esau mbaka kahokela.
12 Esau kalonga, “Haya chigendelele na mwanza
wetu. Niye nizakulongolela.”
13 Yakobo kamwidika, “Mwenevale wangu kovi-
manya kuwa wana wano ving'hele, iviya no-
gesa ng'hondolo na ng'ombe wokong'heza na niye
nolondeka kuwalola goya. Fana chahawagen-
deza siku ngima, yodahika wezadanganika. 14 Ivo
nolonda mwenevale wangu ulongolele na niye
nizasondelela hachisogo ugaluga fana viya kwa
ugenzi wa iwanyama na iwana, mbaka vondani-
fike kwa mwenevale wangu uko Seili.”
15 Esau kalonga, “Leka nikulekele wanhu
wangu wamwenga.”
Mbali Yakobo kamwidika, “Sekeusang'hane
ivo. Vinoga kumwangu kutogoligwa na weye
mwenevale wangu.” 16 Siku iyo Esau kandusa
kwamha nzila yake kubwela Seili. 17 Mbali
Yakobo kahita Sukoti, uko kaizengela kaye
mwenyewo na vizewe kwa ichimu cha wanyama
wake. Ivo hanhu baho hatangigwa Sukoti.

18 Lusita viyabwelile kulawa Padani Alamu,
Yakobo kafika goya muna dibululu da Shekemu
muna iisi ya Kanaani na keka lago jake habehi na
dibululu. 19 Kagula hanhu baho ha lago kulawa
muna uwelesi wa Hamoli tati yake Shekemu kwa
vihande gana va hela. 20 Kazenga lupango hanhu
baho na kuhatanga Eli Elohe Isilaili, fambulo jake
Mulungu ni Mulungu wa Isilaili.

# 34

1 Siku dimwe Dina yoyelekigwe na Yakobo
na Leya, kahita kuwalaula wanaake wa isi iyo.
2 Shekemu mwana wa Hamoli Muhivi yoyakalile
mkulu wa isi iyo, viyamuwene Dina kamwamha
na kagona nayo kwa shuluti na kumtenda yawone
chinyala. 3 Mbali Shekemu kanogelwa ng'hani na
Dina mwana wa Yakobo, ivo kandusa kumbem-
beleza. 4 Ivo Shekemu kamulongela Hamoli tati
yake, "Uning'he mndele ino yawe muke wangu."

5 Yakobo kahulika kuwa Dina mwanage
katendigwa yambule mwiko na Shekemu, Mbali
kwaviya wanage wakala wodima wanyama,
kanyamala mbaka wanage viwabwelile. 6 Hamoli
tati yake Shekemu kahita kwa Yakobo muladi
yadahe kulonga nayo. 7 Ivo wanage Yakobo
wabwela kulawa kudima wanyama wawo,
viwahulike ivo wawona usungu na wehilwa
ng'hani kwa yoyatendile Shekemu, kwaviya
kawaliga wanhu wa Isilaili kwa kumbandama
kwa shuluti mwana wa Yakobo, kwaviya mbuli
iyo mwiko. 8 Hamoli kalonga, "Mwanangu
Shekemu kanogelwa ng'hani na mndele wenu,
ivo nolamba mumuleke yamsole. 9 Leka

chiisole, mweye mwizawasola wanetu na cheye
chizawasola wanenu. 10 Maabaho mwizakala
hano hana isi yetu hamwe na cheye, mwizakala
hohose homulonda na mwizakuwa na ulegeho
wa kugula na kuchuluza vinhu na kupata hanhu."

11 Maabaho Shekemu kamulongela tati yake
Dina na iwalumbu zake, "Nolamba munitende
nitogoligwe haulongozi wenu na niye nizawag-
oleleni chomulonda. 12 Munilongele yombe jojose
da zengele na chitumetume, hata yahawa ng'hulu
vilihi, niye nizalava muladi nimsole yawe muke
wangu."

13 Wanage Yakobo wamwidika kwa kumvwizila
Shekemu na tati yake Hamoli, kwaviya Shekemu
kamtenda lumbu jawo Dina yambule mwiko.
14 Walonga, "Haidahika bule lumbu jetu ku-
soligwa na munhu hengizigwe ulungwana, ku-
tenda ivo ni chinyala kumwetu. 15 Chodaha
kwiitogolela kwa chinhu chimwe muhala mwiz-
akuwa fana cheye kwa kumwingiza ulungwana
chila mulume mmwenu. 16 Baho niivo von-
damusole wandele zetu na cheye kusola wan-
dele zenu. Chizakala hamwe na kuwa wanhu
wamwe. 17 Mbali one hachiitogolela fana bumbila
na kwingizigwa ulungwana, ivo chizamsola mn-
dele wetu na kuhita."

18 Hamoli na Shekemu mwanage wanogelwa
kwa icho chilongigwe, 19 imbwanga hakalame
hata chidogo kufikiza chochilongigwe, kwaviya
viyanogiligwe ng'hani na mndele wa Yakobo.
Shekemu niiyo yoyahishimike kufosa wanhu
wose ukaye kwa tati yake.

20 Hamoli na Shekemu mwanage wahita

kuna ulwivi lwa dibululu hanhu ha mting'hano
kulonga na wanhu wa dibululu, 21 “Wanhu wano
mambwiya, waleke wakale muna iisi na kugula
na kuchuluza vinhu. Isi yofaya kukala cheye na
wawo. Wawo wasole wandele wetu na cheye
chiwasole wandele wawo. 22 Mbali wanhu wano
wahatogola kukala na cheye na kuwa wanhu
wamwe, kwa chilagano chino cha kumwingiza
ulungwana chila mulume vichili, fana viya wawo
viwengizigwe ulungwana. 23 Vino hamuwona
bule wanyama wawo na vinhu vawo vose
vizakuwa vinhu vetu? Lelo chiitogolele nawo
muladi wadahe kukala hamwe na cheye.”
24 Walume wose wa dibululu wowaiting'hane
hana ulwivi lwa dibululu ijo waitogolela na
Hamoli na Shekemu imwanage. Maabaho
walume wose wengizigwa ulungwana.

25 Siku yeketatu wengizigwe ulungwana
wang'hali wana masungu ng'hani, wana waidi
wa Yakobo, niiyo Simeoni na Lawi lumbu zake
Dina wasola ngugulila zawo wadihitila dibululu
ijo kwa kusinhukiza na kuwakoma walume wose.
26 Iviya wawakoma kwa ngugulila Hamoli na
Shekemu imwanage. Maabaho wamsola Dina
kulawa muna ikaye ya Shekemu na wahita nayo.
27 Viufosile ukomaji uwo, wana wamwenga wa
Yakobo wengila muna dibululu na kusola vinhu
kwaviya lumbu jawo katendigwa yambule mwiko
shuluti. 28 Wasola ng'hondolo na ng'ombe na
vihongwe na chila chinhu muna dibululu na
muna imigunda. 29 Wawagwila wana wawo wose
na wanaake wawo wose, na wasola utajili na chila
chinhu muna zikaye zawo.

30 Maabaho Yakobo kawalongela Simeoni na
Lawi, “Mweye munigalila magayo kwa kunitenda
nihiligwe na wanhu wa isi ino ya Wakanaani na
Wapelizi. Niye nabule wanhu wengi, na one wa-
haiduganya hamwe, wezaninanga niye hamwe
na ndugu zangu.”
31 Simeoni na Lawi wedika, “Vino vinoga lumbu
jetu kusang'haniligwa fana viya malaya?”

# 35

*Mulungu komtemela mate Yakobo uko Beseli*

1 Mulungu kamulongela Yakobo, “Segela hano,
uhite Beseli na ukale uko. Unizengele lupango
uko. Niye niiyo Mulungu yoyakulawilile vi-
umkimbile sekulu wako Esau.”
2 Ivo Yakobo kawalongela ndugu zake na wanhu
wose woyakalile nawo, “Segezeni zinyang'hiti za
milungu ya chigeni zimuli nazo, mwiisafye na
mwasakanye viwalo zenu. 3 Chosegela hano
na chohita Beseli, uko nizamzengela lupango
Mulungu yoyanitazile siku ya uzidilwa, Mulungu
yoyakalile na niye muna umwanza wangu.”
4 Chila munhu wamtulila nyang'hiti zose za
milungu ya chigeni zowakalile nazo, hamwe na
heleni zowakalile wozivala mmagutwi. Yakobo
kazihimbila hasi ya mbiki wa muwaloni ukalile
habehi na Shekemu.
5 Yakobo na wanage viwakalile wokwandusa
kusegela, Mulungu kawadumbiza ng'hani
wakaya wa mabululu yose ya habehi mbaka
hawadahile kuwasondelela. 6 Yakobo na wanhu
wake wafika Luzu, iviya yotangigwa Beseli,
muna iisi ya Kanaani. 7 Yakobo kazenga

lupango baho na kahatanga hanhu baho Eli
Beseli, kwaviya Mulungu kamulawilila baho
viyamkimbile sekulu wake. [8] Debola yaya wa
Lebeka kadanganika na kawandigwa hasi ya
mbiki wa muwaloni ubanzi wa kusi wa Beseli.
Ivo Yakobo kahatanga hanhu baho Aloni Bakusi,
fambulo jake “muwaloni wa ndilo.”

[9] Yakobo viyabwelile kulawa Padani Alamu,
Mulungu kamulawilila kaidi na kamtemela
mate. [10] Mulungu kamulongela, “Weye zina jako
Yakobo, mbali kwandusila sambi kwizatangigwa
Isilaili.” Ivo Mulungu kamtanga zina Isilaili.
[11] Mulungu kamulongela, “Niye Mulungu mwene
Udaho, uwe na welesi mwingi na mongezeke.
Wanhu wa makabila yose wezalawa kumwako,
na kwizakuwa wasaho wa wafalume. [12] Isi
yoniweng'hile Bulahimu na Isaka, nizakwing'ha
weye na welesi wako.” [13] Mulungu viyakomeleze
kulonga na Yakobo, kasegela. [14] Yakobo kasimika
mhanda hanhu haja Mulungu hoyalongile
nayo, kaigidila divai na mavuta fana nhosa ya
ching'waji. [15] Yakobo kahatanga hanhu baho
Mulungu hoyalongile nayo Beseli.

### *Ifa ya Laheli*

[16] Yakobo na wanhu wake wagendelela na
mwanza wasegela Beseli, viwakalile wang'hali
hawanafika Efulata, Laheli kapata usungu
ng'hani wa kuibasula. [17] Nayo viyakalile
muna usungu ng'hani wa kuibasula, imulala
kamulongela, “Sekeudumbe Laheli, kupata
mwana imwenga wa chilume.” [18] Mbali
Laheli viyakalile habehi na kudanganika,

kamwing'ha mwanage zina Benoni, mbali tati
yake kamwing'ha mwanage zina Benjamini.
19 Laheli viyadanganike kawandigwa mumgwazo
gwazo wa dikulugumbi dodihita Efulata, sambi
yomanyika Betelehemu. 20 Yakobo kasimika
mhanda uchanyha ya leme da Laheli, mbaka
diyelo mhanda iyo yauko. 21 Isilaili kasegela
baho, na keka lago jake viyafosile lingo da Edeli.

### *Wana wa Yakobo*

22 Isilaili viyakalile isi iyo, mwanage Lubeni
kagona na Biliha imwe wa watumwa wa chike
wakalile fana wake wa tati yake Isilaili na Isilaili
kahulika mbuli izo.

Yakobo kakala na wana longo na waidi.
23 Wanage Leya wakala Lubeni, yeli chaudele wa
Yakobo, na Simeoni na Lawi na Yuda na Isakali
na Zabuloni. 24 Wanage Laheli wakala Yosefu
na Benjamini. 25 Wana wa Biliha msang'hani wa
chike wa Laheli wakala Dani na Nafutali. 26 Wana
wa Zilipa msang'hani wa chike wa Leya wakala
Gadi na Asheli. Wana wano niiwawo woyaweleke
Yakobo uko Padani Alamu.

### *Ifa ya Isaka*

27 Yakobo kahita Mamule kwa Isaka tati yake,
habehi na Kiliasi Aliba, iviya yotangigwa Hebu-
loni, howakalile Bulahimu na Isaka. 28 Isaka
kakala na miyaka gana na malongo manane.
29 Isaka kadanganika mulala ng'hani na kakala na
deng'ho, kahita kuilumba na wasaho zake. Esau
na Yakobo wanage wamuwanda.

# 36

*Welesi wa Esau*

1 Uno uwo ludongo lwa welesi wa Esau, iviya
kotangigwa Edomu. 2 Esau kasola wanaake wa
Kanaani, Ada niiyo mndele wa Eloni Muhiti,
Oholibama mndele wa Ana na ni mzukulu wa
Sibewoni Muhivi, 3 na Basemati mndele wa Ishu-
maili, lumbu jake Nebayoti. 4 Ada kamwelekela
Esau Elifazi na Basemati kamweleka Leuweli.
5 Oholibama kamweleka Yeushi na Yalamu na
Kola. Wano wose wakala wana wa Esau, woy-
aweleke muna iisi ya Kanaani.

6 Maabaho Esau kawasola wake zake na
wanage wa chilume na wanage wa chike na
wanhu wose muna ikaye yake, ng'ombe wake
na wanyama wake wamwenga wose na vinhu
vake vose viyapatile muna iisi ya Kanaani, na
kahita isi imwenga kutali na Yakobo mdodo
wake. 7 Wasegela kwaviya isi yowakalile wokala
Esau na Yakobo ikala haiwafaiye bule. Wakala na
mifugo mingi na wapotwa kukala hamwe muna
iisi ija. 8 Esau kakala muna iisi ya mulima wa
Seili, zina dimwenga da Esau ni Edomu.

9 Uno niuwo ludongo lwa welesi wa Esau,
wasaho wa Waedomu muna iisi ya milima ya Seili.
10 Wana wa Esau watangigwa Elifazi, yoyelekwe
na Ada muke wake, na Leuweli yoyelekwe na
Basemati imuke wake imwenga. 11 Wana wa
Elifazi watangigwa Temani na Omali na Zefo na
Gatamu na Kenazi. 12 Elifazi kakala na muke
imwenga zina jake Timino, iyo kamwelekela
Esau mwana wa chilume zina jake Amaleki,
wawo wakala wazukulu wa Ada muke wa Esau.

13 Basemati muke wa Esau kamweleka Leuweli.
Wana wa Leuweli watangigwa Nahati na Zela na
Shama na Miza.
14 Muke wa Esau Oholibama, mndele wa Ana wa
Sibewoni kamwelekela Esau wana watatu, nawo
niiyo Yeushi na Yalamu na Kola.
15 Wano ni wakulu wowalawile muna uwelesi
wa Esau. Elifazi yoyakalile chaudele wa Esau
kaweleka Temani na Omali na Zefo na Kenazi
16 na Kola na Gatamu na Amaleki, wano wose
niuwo welesi wa Elifazi muna iisi ya Edomu, na
wazukulu wa Ada muke wake Esau.
17 Leuweli mwanage Esau kaweleka Nahati na
Zela na Shama na Miza. Wawo wose wakala
wakulu muna yamakabila yawo. Wano wose
wakala wana wa Leuweli muna iisi ya Edomu na
wazukulu na Basemati muke wa Esau.
18 Wano ni wana wa Oholibama muke wa Esau,
Yeushi na Yalamu na Kola. 19 Wano ni wawo wana
wa chilume wa Esau yani Edomu, chila imwe
wawo kawa mkulu wa kabila jake. Wawo wose
wana wa Oholibama, mwana wa Ana, muke wa
Esau.

*Welesi wa Seyili*

20 Wana wa Seili Muholi wowakalile muna iisi
iyo watangigwa Lotani na Shobali na Sibeyoni na
Ana, 21 na Dishoni na Eseli na Dishani. Wawo
niwawo wakulu wa Waholi wa welesi wa Seili
muna iisi ya Edomu.
22 Wana wa Lotani watangigwa Holi na Heman-
ina, lumbu jake Lotani katangigwa Timina.
23 Wana wa Shobali watangigwa Avani na Man-
ahati na Ebali na Shefo na Onamu.
24 Wana wa Sibeyoni watangigwa Aya na
Ana. Ana niiyo yatolile nzasa za mazi ya moto

kuchuwala viyakalile kowadima mhunda wa
tati yake Sibeyoni. 25 Wanage Ana watangigwa
Dishoni na mndele wake zina jake Oholibama.
26 Wana wa Dishoni watangigwa Hemidani na
Eshibani na Silani na Kelani.

27 Wana wa Eseli watangigwa Bilihani na Za-
awani na Akani.

28 Wana wa Dishani watangigwa Usi na Alani.

29 Wano wakala wakulu wa Waholi, Lotani na
Shobali na Sibeyoni na Ana, 30 na Dishoni na Eseli
na Dishani. Wano wakala wakulu wa kabila da
Waholi, kwa kusondelela ng'holo zawo muna iisi
ya Seili.

### *Wafalume wa Edomu*

31 Wano wakala wafalume watawale mwiisi ya
Edomu, yang'hali mfalume yoyose hanawatawala
bule Waisilaili 32 Bela mwana wa Bewoli kakala
mfalume wa Edomu. Bululu jake ditangigwa
Dinihaba. 33 Viyadanganike Bela, katawala
Yobabu mwana wa Zela kulawa bululu da Bosila,
34 Viyadanganike Yobabu, katawala Hushamu
kulawa isi ya Watemani. 35 Viyadanganike
Hushamu, Hadadi mwana wa Bedadi katawala,
niiyo yoyawatowile na kuwahuma Wamidiani
muna iisi ya Moabu, bululu jake ditangigwa
Aviti. 36 Viyadanganike Hadadi, katawala Samula
kulawa Masileka. 37 Viyadanganike Samula,
katawala Shauli kulawa Lehoboti bululu dili
habehi ya ulwanda lwa Efulati. 38 Viyadanganike
Shauli, katawala Baalihanani mwana wa Akiboli.
39 Viyadanganike Baalihanani, mwana wa
Akiboli, katawala Hadadi, bululu jake ditangigwa

Pawu na muke wake katangigwa Mehetabeli mndele wa Matiledi na mzukulu wa Mezahabu.
40 Yano ni mazina ya masekulu wa Esau kwa kusondelela ng'holo zawo na hanhu hawo, nawo ni Timina na Aliva na Yeteti
41 na Oholibama na Ela na Pinoni,
42 na Kenazi na Temani na Mibisali,
43 na Magidiyeli na Ilamu. Wawo ni wakulu wa makabila yoyalawile Edomu. Edomu niiyo Esau. Wamanyika kwa kusondelela ukazi wawo muna zisi zowakalile.

# 37

*Yosefu na Ndugu zake*

1 Yakobo kagendelela kukala muna iisi ya Kanaani hanhu hoyakalile tati yake fana mgeni.
2 Zino ni mbuli za ugima wa Yakobo. Yosefu viyakalile mbwanga wa miyaka longo na saba, kakala kodima ng'hondolo na luti hamwe na ndugu zake wana wa Biliha na Zilipa, wake wa tati yake. Yosefu kamulongela tati yake mbuli zihile za ndugu zake.
3 Isilaili kamulonda ng'hani Yosefu kufosa wanage wose, kwaviya kamweleka lusita lwa ulala wake. Ivo kamtendela Yosefu ng'hanzu ya chiiyeka yoihambigwe goya.
4 Baho ndugu zake viwawonile kuwa tati yawo kamnogela Yosefu kufosa wawo, wamwihila na hawalongile nayo vinogile bule.
5 Chilo chimwe Yosefu kalota nzozi, na viyawasimulile ndugu zake, wawo waiyoha kumwihila ng'hani.
6 Yosefu kawalongela, “Tegelezeni nzozi yonilotile.
7 Nilota kuwa cheye chikala kumgunda chofunga mikinza, na kwa

kusinhusa kinza jangu dinuka zugaga! Mikinza
yenu iiduganya kudizunguluka na kwiidulikila
kinza jangu."

8 Ndugu zake wamuuza, "Vino weye kochi-
longela kwiza chitawala?" Hebu kwizakuwa
na ukulu kumwetu? Ivo waiyoha kugendelela
kumwihila kwa ichimu cha nzozi na mbuli zake.
9 Maabaho Yosefu kalota nzozi imwenga na
kawalongela ndugu zake, "Nilota nzozi imwenga,
niwona zuwa na mwezi na nhondo longo na imwe
zinitumbalila mavindi."
10 Mbali viyawalongele tati yake na ndugu
zake, tati yake kambwakila kulonga, "Vino nzozi
yaki iyo yuulotile? Vino izatendeza mami yako
na ndugu zako na niye chikutumbalile mavindi
mpaka chidalise hasi kwa hishima haulongozi
wako?" 11 Ndugu zake wamuwonela migongo,
mbali tati yake kagendelela kuigesa mbuli iyo.

## *Yosefu kochuuzigwa na ndugu zake*

12 Siku dimwe ndugu zake Yosefu wahita
kudima mifugo ya tati yawo uko Shekemu.
13 Isilaili kamulongela Yosefu, "Nolonda weye
uhite uko Shekemu kowadimila mifugo ndugu
zako."

Yosefu kamwidika, "Ona nitogola."

14 Tati yake kamulongela, "Hita ukawalole
ndugu zako na mifugo one wawo wagima na
maabaho ubwele unilongele." Ivo tati yake
kamtuma kulawa muna zanda da Hebuloni.
Yosefu kafika Shekemu. 15 Munhu imwe kamu-
wona kowegela muichuwala na kamuuza, "Koza-
hila choni?"

16 Yosefu kamwidika, “Nozahila ndugu zangu
wowodima mifugo yawo. Kodaha kunilongela
haja haweli?”
17 Munhu ija kamwidika, “Wasegela wamala.
Kwaviya niwahulika wolonga wohita Dosani.”
Ivo Yosefu kawasondelela ndugu zake na
kawafika uko Dosani.
18 Viwamuwone kwa kutali, na yang'hali
kuwafikilila, wailungila kumkoma. 19 Wailongela,
“Lola ija nyamiloto kokwiza. 20 Leka chimkome
na chimwase muna disima dimwe. Na
chizalonga kadigwa na ng'onyo kali da muna
imbago. Maabaho chilole kuwa izo zinzozi zake
zizakuwaze.”
21 Mbali Lubeni viyahulike mbuli izo,
kamkombola Yosefu kulawa kumwawo,
kwa kulonga, “Sekechimkome.” 22 Lubeni
kawalongela, “Sekemwitile damu, mbali
mwaseni muna disima dino hano haichuwala,
mbali sekemumulumize.” Kalonga ivo muladi
yamkombole Yosefu muna yamakono yawo,
maabaho yambweleze kwa tati yake. 23 Yosefu
viyafikile kwa ndugu zake, wamvula ng'hanzu
yake ya chiiyeka yoiyawale. 24 Maabaho wamsola
na kumwasa muna disima dilibule mazi.
25 Viwakalile woja wawona bumbila da
Waishumaili wokwiza kulawa Gileadi kuhita
Misili. Ngamiya wawo wakala wapapile vilungo
na ubani na mavumba. 26 Yuda kawalongela
ndugu zake, “Chizapata choni chihamkoma
ndugu yetu, na kufisa ukomaji wake? 27 Chimgule
kwa Waishumaili, mbali sekechimulumize
kwaviya yeye ni ndugu yetu na iviya ni damu
imwe na cheye.” Ndugu zake waitogolela,

28 Wagula vinhu Wamidiani viwafikile hanhu
baho, ndugu zake wamulava Yosefu muna disima
na wamchuuza kwa Waishumaili kwa vihande
malongo maidi va hela, na Waishumaeli wamsola
Yosefu mbaka Misili.

29 Lubeni viyabwelile kuna disima dilibule
mazi, hamwone Yosefu bule, Lubeni kadega walo
jake kwa usungu. 30 Hamala baho Lubeni kawab-
welela ndugu zake na kalonga, “Mbwanga kahab-
ule hano! Choni chondanitende?”

31 Hamala baho wachinja mwana luti na
wachofeka ng'hanzu ya Yosefu muna idamu.
32 Waisola ing'hanzu mbaka kwa tati yawo
na walonga, “Chiiitola ino, lola vino ino niiyo
ng'hanzu ya mwanago?”

33 Yakobo kaimanya ing'hanzu kalonga, “Iyo
yake! Mng'onyo wa kumbago kamgwila na ka-
muja. Yosefu kanyomholigwa vihande vihande!”
34 Baho Yakobo kayadega yamawalo yake kwa
usungu, kaiyawaza mawalo ya maguniya muna
ichigudi. Kamulililа mwanage kwa siku nyingi.
35 Wanage wa chilume na wachike wamwizila
wadahe kumuliza, mbali Yakobo kalema kulizwa
kwa kulonga, “Nilekeni nizagendelela kulila kwa
chimu cha mwanangu, mbaka vondanihite kuz-
imu kuyeli.” Niivo tati yake viyagendelele ku-
mulilila Yosefu.

36 Chipindi icho uko Misili Wamidiani wamgula
Yosefu kwa Potifa imwe wa walangulizi wa
mfalume yoyakalile mkulu wa chibumbila cha
ukalizi.

# 38

*Yuda na Tamali*

1 Chipindi icho Yuda kawaleka ndugu zake
na kahita kukala na munhu zina jake Hila,
Mwadulamu 2 Uko Yuda kaiting'hana na mn-
dele Mkanaani tati yake zina jake Shuwa. Yuda
kamsola mndele iyo na kambandama, 3 Mndele
wa Shuwa kapata wimo na keleka mwana wa
chilume, Yuda kamtanga Eli. 4 Kapata wimo
umwenga kaidi na keleka mwana imwenga na
zina jake kamtanga Onani. 5 Kaidi kapata mwana
imwenga wa chilume, kamtanga Shela. Shela
viyelekwe, Yuda kakala uko Kezibu.

6 Yuda kamfungiza zengele Eli mwanage
chaudele, kwa muke yatangigwe Tamali.
7 Mbali Eli chaudele wa Yuda kakala na
mbuli za mdukula haulongozi wa Mndewa
Mulungu, ivo Mndewa Mulungu kamkoma.
8 Ivo Yuda kamulongela Onani ndugu wa Eli,
“Hita ukamwingilile muke wa sekulu wako
imgane, kwaviya niivo viulondeka utende udahe
kumwelekela sekulu wako wana.” 9 Mbali Onani
kavimanya kuwa sigambe iwe wanage bule, ivo
viyambandame muke wa sekulu wake, ketilila
hasi zimbeyu, sekeyampatile wana sekulu wake.
10 Choyachitendile Onani iviya chiwa chiha kwa
Mndewa Mulungu, iviya yeye nayo Mndewa
Mulungu kamkoma. 11 Yuda kamulongela Tamali
imkoyi wake wa chike, “Bwela kwa tati yako ukale
ugane mbaka mwanagu Shela vondayakule.”
Yuda kadumba Shela sekeyadanganike fana viya
ndugu zake. Ivo Tamali kabwela ukaye kwa tati
yake.

12 Lusita lukulu lufosa, muke wake Yuda
mwana wa Shuwa kadanganika. Yuda
viyakomeleze ndilo, kasegela na mbwiyake
Hila kulawa Mwadulamu wahita Timina kwa
wakanha mizoya ya ng'hondolo wake. 13 Tamali
kahulika kuwa mkoyi wake wa chilume kakala
yohita Timina, kuwakanha mizoya ng'hondolo
wake. 14 Tamali kayavula mawalo ya ukefilwa,
kaigubika mtandilo maabaho kakala hana
dikumba da kwingilila Enaimu, chibululu
chochikalile mwiinzila kuhita Timina. Katenda
ivo kwaviya kawona kuwa Shela kawa munhu
mkulu mgima mbali Tamali hasoligwe bule na
Shela.

15 Yuda viyamuwone Tamali kagesa kuwa
kakala yochuuza lukuli lwake, kwaviya
chihanga chake kakala yachigubike. 16 Baho
havimanyile bule iyo kakala muke wa mwanage
Yuda, kamuhitila baho hamgwazo ya inzila
kamulongela, “Nolonda nikubandame.”

Tamali kalonga, “Kwizaning'ha choni wahanibandama?”

17 Yuda kamwidika, “Nizakwing'ha mwana luti
kulawa bumbila jangu.”

Tamali kamulongela, “Yose yanoga, yodahika wike wingilizi kulagusa kwizanigalila iyo iluti.”

18 Yuda kamuuza, “Kolonda nikwing'he choni
fana wingilizi?”

Tamali kamwidika, “Ning'he chinhu chili na luzabi chili na chilaguso chako na mhome.” Yuda kamwing'ha vinhu ivo vose na kambandama, nayo kapata wimo.

19 Maabaho Tamali kasegela, kahambula
mtandilo woyaigubike, kayawala nyawalo zake
za ugane.

20 Yuda viyamtumile ija imbwiya Mwadulamu,
yamgalile ija mwanamke mwana luti muladi
yambwelezele wingilizi yoyamulekele, mbali
hamfikile bule. 21 Kawauza wanhu wa Enaimu,
“Kakulihi muke ija malaya yoyakalile hano hana
dikulugumbi yoyotenda umalaya fana nzila ya
kutosela nyang'hiti za milungu?”

Iwanhu wamwidika, “Hanhu hano hakalile na
muke malaya bule.”

22 Hila kambwelela Yuda na kalonga, “Simu-
wonile bule. Wanhu wa hanhu baho walonga
kuwa hano hahakalile na muke malaya.”

23 Yuda kalonga, “Leka yavisole vinhu ivo.
Sekeyachitendeze wanhu wachizehe. Weye
mwenyewo kuwona nimgalila mwana luti mbali
weye humfikile bule.”

24 Viifosile miyezi mitatu, Yuda kalongiligwa
kuwa, “Mkoyi wako Tamali muke wa mwanago
kapata wimo kwa ugoni wake.”

Yuda kalagiliza, “Msoleni yalavigwe kunze ya-
somigwe moto mbaka yadanganike.”

25 Viwakalile womulava kunze, Tamali katuma
usenga kwa mkoyi wake wa chilume: “Niye nina
wimo kwa munhu mwene vinhu vino. Umulole
na ummanye munhu mwene chinhu chili na luz-
abi chili na chilaguso chako na mhome ino.”

26 Yuda kavimanya vinhu ivo na kalonga,
“Tamali kanoga kufosa niye, kwaviya simsolele
mwanangu Shela.” Kusongela siku ijo Yuda
hambandame kaidi Tamali.

27 Viifikile chipindi cha Tamali kwiibasula,
kukala na mambasa mwiinda yake. 28 Usungu
vuumfikile wa kwiibasula, mbasa imwe kalava
mkono kunze, nayo imulala kamfunga kwa
lusingija ludung'u kuno kolonga, “Ino niiyo
yanduse kwelekigwa.” 29 Mbali imwana
viyaubweleze mkono mgati, ndugu yake kandusa
kwelekigwa. Imulala kalonga, “Hee weye kufosa
kwa nguvu kulawa kunze!” Ivo katangigwa zina
jake Pelesi, fambulo jake “Kulawa kwa nguvu.”
30 Maabaho sekulu wake nayo kelekigwa kuno
kana lusingija ludung'hu muna umkono wake,
nayo katangigwa Zela.

# 39

### *Yosefu na Muke wa Potifa*

1 Waishumaili viwamsolile Yosefu wamgala
mbaka Misili na wamchuuza kwa Potifa, imwe
wa wakulu wa mfalume, na niiyo mkulu wa
chibumbila chake cha wakalizi. 2 Mndewa
Mulungu kakala hamwe na Yosefu, nayo katenda
vinogile ng'hani kwa chila chinhu. Yosefu
kakala muna ikaye ya mwenevale wake Mmisili.
3 Mwenevale wake viyawonile kuwa Mndewa
Mulungu kakala hamwe na Yosefu na chila
chiyatendile katenda vinogile. 4 Ivo Potifa
kanogeligwa ng'hani na Yosefu, na kamtenda
msang'hani wake, ivo kamwika kuwa mulolesi
wa kaye yake na chila chinhu chiyakalile nacho.
5 Kwandusila lusita ulo, kwa ichimu cha Yosefu
Mndewa Mulungu kaitemela mate kaye ya
Mmisili iyo na chila chinhu choyakalile nacho
na migunda yake. 6 Potifa keka chila chinhu

chiyakalile nacho haulolesi na ukalizi wa Yosefu, na hagesile chochose ila kuja ndiya yake muhala.

Yosefu kakala mbwanga yanogile na chihanga
chinoga, 7 na lusita vilufosile muke wa Potifa
kandusa kummelela mate Yosefu na kamulamba
yahite yakaibandame nayo. 8 Yosefu kalema
na kamulongela, “Mwenevale wangu kabule
lugano jojose muna ikaye kwaviya niye nabaha,
na kanitulila chila chinhu chiyeli nacho.
9 Hano hakaye kabule mamulaka kufosa niye,
hanilemesa kwamha chochose ila weye muhala
kwaviya weye kwa muke wake. Ivo nodahaze
kutenda wihi fana uwo kwa kumuhasanya
Mulungu?” 10 Na muke wa Potifa kamulongela
Yosefu mbuli iyo chila siku, mbali Yosefu kalema
kumbandama na hata kuwa hamwe nayo.

11 Mbali siku dimwe Yosefu kengila mgati
mwiikaye kusang'hana sang'hano yake na
wasang'hani wamwenga hawakalile umo.
12 Muke wa Potifa kamgwila debwani jake
na kulonga, “Unyangale.” Mbali Yosefu
kasulupuka na kakimbilila kunze, kadileka
debwani jake mmakono yake. 13 Muke wa
Potifa viyawonile kuwa Yosefu kadileka
debwani jake na kukimbilila kunze ya ikaye,
14 kawatanga wasang'hani wa kaye yake na
kawalongela, “Loleni ino! Ino Muebulaniya
mulumangu yoyomgalile mwiikaye kochiguma
chinyala. Kengila muna ichiheleto changu
muladi yanyangale, mbali niye niguta nyangi.
15 Viyahulike noguta nyangi, kakimbilila kunze,
kadileka debwani jake hamwangu.”

[16] Mwanamke ija kadika debwani diya, mbaka
mwenevale wa Yosefu viyabwelile ukaye.
[17] Kamsimulila mbuli iyo, “Iyo msang'hani
Muebulaniya yoyumgalile hano kengila muna
ichiheleto kuniguma chinyala. [18] Mbali vinigutile
nyangi, kadileka debwani jake na kukimbilila
kunze.”
[19] Mwenevale wa Yosefu viyazihulike mbuli
izo za muke wake, kuwa ivo viyasang'hane
msang'hani wake, kawa na ludoko [20] na kamgwila
Yosefu na kumwika muna ichifungo hanhu
hawakalile wafungigwa wa mfalume. Ivo Yosefu
kalekigwa mwiichifungo. [21] Mbali hata umo
muichifungo Mndewa Mulungu kakala nayo
na kagendelela kumulagusa Yosefu ulondo
wake, mbaka mkulu wa chifungo kanogelwa
nayo. [22] Mkulu wa chifungo kamwika Yosefu
yawe mkulu wa wafungigwa wose na chila
chochitendeke umo muna ichifungo chitendeka
kwa ulangulizi wake. [23] Mkulu wa chifungo
hagesile chinhu chochose, Yosefu katuliligwa
chila chinhu kwaviya Mndewa Mulungu kakala
hamwe nayo na chila chinhu choyachitendile
katenda vinogile.

# 40

### *Yosefu kofambula Nzozi*

[1] Viyafosile yayo mwikagoya ving'waji
na mokaji magate wa mfalume wa Misili
wamuhasanya mfalume wa Misili. [2] Mfalume
kawawonela ludoko walangulizi wake waidi,
mwikagoya ving'waji na mokaji magate [3] na

kawaguma muna ichifungo muna ikaye ya
mkulu wa wakalizi, hanhu hoyafungigwe Yosefu.
4 Wanhu wawo wakala muna ichifungo kwa
lusita, na mkulu wa wakalizi kamwing'ha ukulu
Yosefu yawalolese.

5 Ikala chilo chimwe, mwikagoya ving'waji
na mokaji magate wa mfalume wa Misili
wowafungigwe muna ichifungo walota nzozi,
chila imwe kalota nzozi mbasakanyo na miyage,
nzozi zikala na fambulo mbasakanyo. 6 Yosefu
viyezile imitondo, kawawona kuwa wawa
luholozi. 7 Yosefu kawauza wakulu wawo wa
mfalume wowakalile hamwe nayo mwiichifungo
mwiikaye ya mwenevale wake, "Habali diyelo
muna vihanga va luholozi?"

8 Nawo wamwidika, "Chilota nzozi na habule
yodaha kuchifambulila nzozi zetu."

Yosefu kalonga, "Vino siyo Mulungu muhala
yoyodaha kufambula nzozi?" Nilongeleni nzozi
zenu.
9 Mwikagoya ving'waji wa mfalume
kamulongela Yosefu, "Muna inzozi yangu niwona
kuzubuku da mzabibu haulongozi wangu,
10 nawo ukala na matambi matatu. Lusita
viusukile mayani, maluwa yake yapumbuluka
na vilobota vake viwa zabibu zivile. 11 Mmakono
yangu nikala nokwamhilila nhungo ya mfalume.
Baho nisola zabibu nizikamula muna inhungo na
nimwing'ha mfalume." 12 Yosefu kamulongela,
"Dino niijo fambulo jake, matambi matatu ni
siku nhatu. 13 Zahafika siku nhatu, mfalume
kezakulava muna ichifungo na kukubweleza
kaidi muna ukulu wako. Kwizamwing'ha

mfalume nhungo fana viukalile kotenda baho
haumwanduso. 14 Mbali ung'humbuke baho
chila chinhu vondachihite goya kumwako, na
nolamba unitendele yanogile na unitambule
baho haulongozi wa mfalume na unitaze
nilawe muna ichifungo chino. 15 Kwaviya niye
nitolosigwa kulawa isi ya Waebulaniya na hano
sitendile chochose chinitendeze nigumigwe
muna ichifungo."

16 Mkulu wa mokaji magate viyawone fam-
bulo ijo dinoga da mwikagoya ving'waji, ka-
mulongela Yosefu, "Iviya naniye nilota nzozi,
nikala niitwikile vigelo vitatu va magate mditwi
jangu. 17 Muna ichigelo cha uchanyha kukala
na ndiya mbasakanyo zibanikigwe kwa ichimu
cha mfalume, mbali udege wazija muna ichigelo
uchanyha mditwi jangu."

18 Yosefu kamwidika, "Dino niijo fambulo jake:
Vigelo vitatu ni siku nhatu. 19 Muna zisiku nhatu
mfalume kezakulava mchifungo, na kukuchinja
ditwi jako. Kezakutumbika muna umbiki na
ndege wezakuja nyama yako."

20 Siku ya tatu, ikala siku ya kufikiza
kwelekigwa mfalume. Mfalume kawekila
dugila wakulu wake wose, kamulava muna
ichifungo mwikagoya ving'waji na mokaji magate
mkulu na kaweka haulongozi wa wakulu wake.
21 Mfalume kambweleza mwikagoya ving'waji
muna ukulu wake wa kung'wiza, muladi
yamwing'he nhungo mfalume muna yamakono.
22 Mbali mokaji magate mkulu katumbikigwa
fana viyalongile Yosefu. 23 Mbali mwikagoya

ving'waji, hamkumbuke bule Yosefu kamzimiza.

# 41

### *Yosefu Kofambula Nzozi za Mfalume*

1 Viifosile miyaka midi, mfalume wa Misili
kalota nzozi, kuwa kakala yemile muna ingema
ya lwanda lwa Naili, 2 lusita kawona ng'ombe saba
watelele na wanenehe walawa kunze ya ulwanda
lwa Naili na wandusa kuja mgina. 3 Maaabaho
ng'ombe saba wamwenga weza, wowakalile wa-
sisili na wasoka. Weza na wema habehi na waja
ng'ombe mumgwazo wa ulwanda luja lwa Naili,
4 Ng'ombe waja saba wasisili na wasokile, wawaja
ng'ombe waja watelele na wanenehe. Maabaho
mfalume kalamuka. 5 Kagona kaidi na kalota
nzozi zimwenga. Mimada saba ya uhemba imema
na ikangala, ikung'huna muna dibuwa dimwe.
6 Mimada saba ya uhemba imisisili yoinyazigwe
na mbeho ili na vuke ya ulawilo wa zuwa ilaw-
ilila. 7 Ivo mimada misisili iyaja ija imimada saba
yoinenehe. Mfalume kalamuka kavimanya kuwa
kakala kolota. 8 Imitondo kengilwa na lugano,
katuma wasawi wose na wanhu wabala wose
wa Misili. Na mfalume kawalongela nzozi zake,
mbali habule munhu yoyose yamfambulile.

9 Maabaho mkulu wa mwikagoya ving'waji
kamulongela mfalume, “Diyelo nokumbuka
ubananzi wangu woniutendile. 10 Lusita luja
viuchiwonele ludoko cheye wakulu wako, niye
na mkulu wa mokaji magate na kuchifunga muna
ichifungo muna ikaye ya mkulu wa wakalizi.
11 Chilo chimwe niye na yeye chilota nzozi, na

chila nzozi ikala na fambulo jake. 12 Mbwanga
iyo Muebulaniya msang'hani wa mkulu wa wakalizi kakala hamwe na cheye, Chimulongela
nzozi zetu, na yeye kachifambulila. 13 Chila
chinhu chilawilila fana viya viyalongile. Ukulu wangu nibweleziligwa mbali mokaji magate katumbikigwa."

14 Mfalume kalagiliza Yosefu yagaligwe, na wamgala kulawa muna ichifungo. Yosefu viyamalile kuwegula na kusaula nyawalo zake, kahita
kwa mfalume. 15 Mfalume kamulongela Yosefu,
"Nilota nzozi, mbali habule munhu yoyose yoyadahile kunifambulila. Nilongiligwa kuwa weye kodaha kuzifambula nzozi."

16 Yosefu kamwidika mfalume, "Sidaha bule, mbali Mulungu kezamfambulila mfalume vinogile."

17 Mfalume kamulongela Yosefu, "Nilota nima
muna ingema ya lwanda lwa Naili, 18 niwawona
ng'ombe saba wolawa muna ulwanda lwa Naili watelele na wanenehe na wandusa kuja mgina.
19 Maabaho ng'ombe wamwenga saba wasisili na
wasokile. Muna iisi yose ya Misili sinawawona
bule wowalingile fana wawo. 20 Ng'ombe wasisili
na wasokile weza na wawaja iwang'ombe saba
waja wanenehe, 21 mbali viwamalile kuwaja
ng'ombe waja wanenehe, munhu yoyose sigambe yavimanye kuwa wawaja wayawo, kwaviya wakala wasoka fana viya ichanduso. Maabaho
nilamka mzinhongo. 22 Maabaho muna zinzozi
zangu niwona mimada saba ya uhemba inogile na imema yokung'huna muna dibuwa dimwe.
23 Maabaho mimada saba ya uhemba, imisisili

inyazigwe na mbeho ili na vuke ya ulawilo wa
zuwa ilawilila, 24 na mimada iyo misisili imela ija
mimada saba inogile. Niwalongela waganga
nzozi izo, mbali habule munhu yoyadahile
kunifambulila.”
25 Yosefu kamulongela mfalume, “Nzozi zako
mbili zina fambulo dimwe, Mulungu kakulon-
gela chiya chondayatende. 26 Waja ng'ombe saba
wanenehe ni miyaka saba, na ija mimada saba
ya uhemba inogile iviya ni miyaka saba, fambulo
jake ni dimwe. 27 Waja ng'ombe saba iwasisili na
wasokile, waja wowasondelele waja wanenehe
na ija mimada saba ya uhemba, yoinyazigwe
na mbeho ya ulawilo wa zuwa, fambulo jake
ni miyaka saba ya nzala. 28 Fana viya vin-
imulongele mfalume, Mulungu kamulagusa yaja
yondayatende. 29 Kwizakuwa na miyaka saba
ya shibe muna iisi yose ya Misili. 30 Yahafosa
yayo, kwizalawilila miyaka saba ya nzala, na
miyaka ija inogile izazimizwa muna iisi ya Mis-
ili, kwaviya nzala izalumiza isi. 31 Chipindi cha
shibe hachizakumbukigwa, kwaviya nzala ikwiza
izakuwa ng'hulu. 32 Kwaviya nzozi ya mfalume
ibweleligwa miyanza midi, imulagusa kuwa Mu-
lungu kalamula na kezaifikiza mbuli ino ivino
sambi.

33 “Lelo mfalume kolondeka yamsagule munhu
yeli na umanyi na ubala, yawe mulolezi muna
iisi ya Misili. 34 Kaidi yeye mfalume, yawatome
walolesi wamwenga hano mwiisi, yawalagilize
waduganye hanhu ha tano ha ndiya ya miyaka
saba ya shibe muna iisi ya Misili. 35 Yawalagilize

waduganye ndiya zose chipindi cha miyaka in-
ogile ikwiza, na kumwing'ha udahi mfalume wa
kwika ndiya muna yamagulu kwa ichimu cha
ndiya ya mabululu yose, ikalizwe kwa kwikigwa
goya. 36 Ndiya iyo izakuwa ngama ya isi chipindi
cha miyaka saba ya nzala yondaiwe muna iisi ya
Misili. Kwa nzila ino wanhu hawezadanganika
kwa nzala bule."

### *Yosefu kokwing'higwa ukulu Misili*

37 Mbuli iyalongile Yosefu imnogeza mfalume
na wakulu wake. 38 Ivo mfalume kawauza
wakulu wake, "Vino chompatahi munhu fana ino
Yosefu yeli na muhe wa Mulungu mgati yake?"
39 Mfalume kamulongela Yosefu, "Kwaviya Mu-
lungu kakulagusa yano yose, habule munhu yeli
na ubala fana weye. 40 Nokwika weye muna
ulolesi wa isi yangu, na wanhu wangu wose weza-
kutegeleza. Ukulu wako wizakuwa wekaidi ku-
lawa niye. 41 Mfalume kamulongela Yosefu, Lelo
nokwing'ha ukulu wa kutawala isi yose ya Mis-
ili." 42 Mfalume kavula chinhu chili na luzabi
chili na chilaguso chake muna ichidole chake,
na kachiguma muna ichidole cha Yosefu. Ka-
muyawaliza walo da mgolole na kumvaza mkufu
wa zahabu mwiiisingo yake. 43 Mfalume kamk-
weza muna umtuka wake wekaidi wa falasi, na
wakalizi walongolela haulongozi wa Yosefu, kuno
wolandula madizi yawo na kulonga, "Tumbaleni
mavindi!" Ivo niivo mfalume viyamwing'hile
ukulu Yosefu muna iisi yose ya Misili. 44 Maabaho
mfalume kamulongela Yosefu, "Niye mfalume,

na habule munhu yoyose muna iisi yose ya Mis-
ili yondayenule mkono hebu mgulu bila ya ku-
longiligwa na weye.” 45 Mfalume kamwing'ha
Yosefu zina da Chimisili, Zefanati Paneya, na
kamwing'ha muke, Asenati mwana wa Potifela,
mkulu wa nhambiko wa bululu da Oni. Yosefu
kahita uko na uko muna iisi ya Misili 46 Yosefu
kakala na lika da miyaka malongo matatu viyan-
duse kumsang'hanila mfalume wa Misili. Yosefu
kahasegela haulongozi wa mfalume na kahita
kuna iisi yose ya Misili. 47 Ivo muna imiyaka
ija saba ya shibe, migunda muna iisi ilava ndiya
mvunyo, 48 Yosefu kaduganya ndiya kwa miyaka
saba muna iisi ya Misili na keka kuna yamabul-
ulu. Chila bululu keka ndiya kulawa mmigunda
yoizunguluka. 49 Yosefu keka ngama ya ndiya
mvunyo fana viya msanga wa mwiibahali mbaka
kapotwa kuipeta kwaviya haipeteka.

50 Ing'hali hainakwandusa miyaka saba ya
nzala, Yosefu kawa kapata wana waidi kwa imuke
Asenati mwana wa Potifela mkulu wa nhambiko
wa Oni. 51 Yosefu kamtanga mwanage chaudele
zina jake Manase, kwaviya kalonga, “Mulungu
kanitenda nizimize manhesa yangu yose na kaye
ya tati yangu.” 52 Mwana magati kamtanga
zina Efulaimu, fambulo jake, “Mulungu kaning'ha
wana muna iisi ya manhesa yangu.”

53 Miyaka saba ya shibe iwa imala muna iisi ya
Misili, 54 na miyaka saba ya nzala yandusa, fana
viya Yosefu viyalongile. Kukala nzala muna zisi
zimwenga zose, mbali muna iisi ya Misili kukala
na ndiya. 55 Wamisili viwanduse kuwa na nzala,
wamulilila mfalume yaweng'he ndiya. Mbali

mfalume kawalongela Wamisili wose, “Muhite
kwa Yosefu na mutende chondayawalongele.”
56 Nzala yenela muna iisi yose, Yosefu kayavugula
madungu yose na kawachuluzila ndiya Wamisili,
kwaviya nzala ikala ng'hulu muna iisi ya Misili.
57 Wanhu kulawa zisi zose weza Misili kugula
ndiya kwa Yosefu, kwaviya nzala ikala ng'hulu
ng'hani chila hanhu.

# 42

### *Ndugu zake Yosefu wohita Misili kugula uhemba*

1 Yakobo viyamanyile kuwa uko Misili kuna
ndiya, kawalongela wanage, “Habali mweye
moilola mweye kwa mweye muhala? 2 Nihulika
uko Misili kuna ndiya, hiteni uko mukagule
ndiya muladi sekechidanganike kwa nzala.”
3 Ivo ndugu longo wa Yosefu wahita Misili kugula
ndiya. 4 Mbali Yakobo hamulekele bule Benjamini
mdodo wake Yosefu kuhita na ndugu zake,
kwaviya kadumba chinhu chihile kumulumiza.

5 Wana wa Isilaili wafika Misili, wagula ndiya
fana viya wamwenga, kwaviya uko kwiisi ya
Kanaani kukala na nzala. 6 Chipindi icho, Yosefu
niiyo yoyakalile mulolesi wa isi ya Misili, yoy-
awachuuzile ndiya wanhu walawile zisi zose.
Ivo ndugu zake Yosefu weza na wamtumbalila
mavindi mbaka vihanga vidalisa hasi. 7 Yosefu
viyawawone ndugu zake kawatambula, mbali
kaitenda fana viya hawamanyile bule. Kawauza
kwa ukali, “Mweye mulawa kulihi?”

Nawo wamwidika, “Chilawa isi ya Kanaani, chiza kugula ndiya.”

8 Yosefu kawamanya sekulu zake, mbali wawo
hawammanyile bule. 9 Yosefu kaikumbuka
nzozi yoyailotile na kalonga, “Mweye mwiza kupelemba unyonyonde wa isi yetu.”

10 Ndugu zake wamwidika, “Siyo mwenevale.
Cheye ni wasang'hani wako chiza kugula ndiya.
11 Cheye chose ni ndugu, cheye siyo wapelembaji,
cheye wasang'hani wako ni wanhu hachilonda uvwizi.”

12 Mbali Yosefu kagendelela kulonga, “Siyo! Mwiza kupelemba unyondenyonde muna iisi yetu.”

13 Wamulongela, “Cheye wasang'hani wako, chose cha ndugu longo na waidi, wana wa munhu imwe mkaya wa Kanaani. Ndugu yetu imwe kadanganika, na mdodo wetu kasigala na tati yetu.”

14 Yosefu kawedika, “Fana viya viniwalongele,
mweye mwa wapelembaji. 15 Vino niivo von-
damugezigwe, noilaha kwa zina da mfalume, hano hamwizahalawa mbaka mdodo wenu von-
dayeze hano. 16 Mtumeni imwe wenu yamson-
delele ndugu yenu imdodo na kuno wamwenga wogozela muna ichifungo baho hondaumanyike ulonzi wenu kweli yake, la sivo noilaha kwa zina da mfalume, mweye mwa wapelembaji.”
17 Maabaho kawaguma muna ichifungo kwa
siku nhatu. 18 Siku yetatu Yosefu kawalon-
gela, “Kwaviya niye nomdumba Mulungu, ten-
deni vino na mweye mwizakala. 19 One mweye
mwa wanhu siyo wauvwizi, imwe wenu yasigale

muna ichifungo, wamwenga wawagalile ndiya
ndugu zenu ukaye weli na nzala. 20 Maabaho
mumgale mdodo wenu kumwangu. Iyo yolagusa
ukweli wa ulonzi wenu, na hamwizakomigwa
bule.” Waitogolela ivo. 21 Maabaho walonganya,
“Lelo cheye cha muna yamagayo kwa ichimu cha
yaja yochimtendele Yosefu ndugu yetu, chimu-
wona kakala na luholozi mkulu hata viya viy-
achilambile nhazo, mbali cheye hachimtegeleze
bule. Lekamana magayo yano yose yochilaw-
ilila.”
22 Lubeni kawedika, “Siwalongele bule
kuwa sekemumulumize mbwanga? Mbali
mweye hamunitegeleze bule! Lelo damu
yake yolondigwa kumwetu.” 23 Yosefu kakala
yovimanya yose yowakalile wolonga, mbali
wawo hawavimanyile bule kuwa kavimanya,
kwaviya viyalongile kalonga nawo kwa nzila
ya mfambulaji. 24 Yosefu kasegela hoyakalile
na kandusa kulila. Kabwela na kulonga nawo,
kamgwila Simeoni na kamfunga haulongozi
wawo.

### *Ndugu wa Yosefu wobwela Kanaani*

25 Yosefu kalagiliza maguniya yawo ya
kusumila yamemezigwe ndiya na kumbwelezela
chila imwe wawo hela muna diguniya jake
na ndiya ya mzila. Ivo niivo itendeke.
26 Wawapapiza mbahasha zawo vihongwe, na
maabaho wasegela. 27 Viwafikile hanhu ha
kugona nyambenyambe, imwe wawo kafungula
lobota jake yadahe kumdima chihongwe wake,
kazanywa kuwona hela yake muna diguniya
jake. 28 Kawalongela ndugu zake, “Hela yangu

ibwelezigwa.” Aino hano hanadiguniya jangu! Viwahulike yayo mizoyo yawo igwa na wakala wogudema kwa ludumbo na kwiiuzagiza wenyewo, “Chinhu chaki chino Mulungu choyachitendele?”

29 Viwafikile kwa tati yawo Yakobo uko kuna iisi ya Kanaani, wamulongela mbuli zose zozilaw-
ilile. 30 “Mkulu wa isi ya Misili kalonga na cheye
kwa ukali na kuchilonga cheye cha wapelembaji
muna iisi yake. 31 Mbali cheye chimwidika, ‘Cheye
siyo wapelembaji, cha wanhu hachilonga uvwizi.
32 Chimulongela kuwa cheye cha ndugu longo na
waidi, wana wa tata imwe. Ndugu yetu imwe ni mwene kwaga, mdodo wetu kauko kuna iisi ya
Kanaani hamwe na tati yetu.’ 33 Mbali mkulu
